EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

HUDUMA ZA KIJAMII NA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI KWA AJILI YA MKUZA WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI, SEHEMU YA TANZANIA

MPANGO KAZI WA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI MKOA WA KAGERA

TOTAL EAST AFRICA MIDSTREAM B.V.

SEPTEMBA 2020

Wakandarasi wa RAP

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki

Huduma za Kijamii na Uhamishaji Watu na Makazi kwa Ajili ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania

Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi Katika Mkoa wa Kagera

Total East Africa Midstream B.V.

Septemba, 2020

Septemba 2020 – Ripoti hii ni Tafsiri ya Ripoti Halisi (*Final Disclosed Resettlement Action Plan (RAP) for Pipeline and AGIs in Tanga Region*) Iliyoandikwa na Kuchapishwa kwa Lugha ya Kiingereza.

Ripoti hii imeandaliwa na Muungano wa Makampuni ya Digby Wells.

Ripoti:	**Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) Katika Mkoa wa Kagera**
Jina la Mradi:	**Huduma za Kijamii na Uhamishaji Watu na Makazi kwa Ajili ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania**
Msimbo wa Mradi:	**TOT5212**

Matoleo

Namba ya Toleo	Marekebisho	Tarehe ya Ripoti
V1	Rasimu ya Mwisho ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) kwa ajili ya Mkuza wa Bomba na miundombinu ya juu ya Ardhi katika Mkoa wa Kagera iliyotolewa kwa Serikali ya Tanzania (GoT) kwa ajili ya kipindi cha maoni.	Februari, 2020
V2	Ripoti ya Mwisho Kutolewa ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) kwa ajili ya Mkuza wa Bomba na miundombinu ya juu ya Ardhi katika Mkoa wa Kagera	Septemba 2020

Utangulizi

Huduma za Kijamii na Uhamishaji Watu na Makazi kwa Ajili ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania

Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi Katika Mkoa wa Kagera

Total East Africa Midstream B.V.

Septemba, 2020

Septemba 2020 – Ripoti hii ni Tafsiri ya Ripoti Halisi (*Final Disclosed Resettlement Action Plan (RAP) for Pipeline and AGIs in Tanga Region*) Iliyoandikwa na Kuchapishwa kwa Lugha ya Kiingereza.

MUHTASARI

1. UTANGULIZI

Sura ya utangulizi ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika Mkoa wa Kagera inaelezea muktadha, eneo na lengo la nyaraka. Inabainisha wadau wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi wa Afrika Mashariki (EACOP), na timu inayohusika katika kupanga na kuandaa RAP ya Mkoa wa Tanga. Orodha ya Sura hizi (List of chapters) imewekwa bayana ili kuwaogoza wasomaji katika usomaji wa nyaraka hii.

Mradi wa Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi wa Afrika Mashariki (EACOP Project) unajumuisha ujenzi pamoja na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya Mashariki mwa Tanzania. Sehemu ya Mkuza wa bomba katika upande wa Tanzania ina urefu upatao kilomita 1,147 na kwamba mkuza huu utapita katika mikoa minane (8) ya Tanzania ikijumuisha pamoja na ardhi iliyo chini ya usimamizi wa Tawala za Halmashauri za Wilaya 27. Nyaraka hii ni RAP sehemu ya Mkuza wa bomba la mafuta lenye urefu wa kilomita zipatazo 174.58 linalopita kwenye maeneo ya Tawala za Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba and Biharamulo zilizopo katika mkoa wa Kagera. Mpango kazi wa Uhamishaji watu na Makazi katika mkoa wa Kagera ni mojawapo ya mpango kazi ya Mipango tisa (9) ya Mradi huu nchini Tanzania.

Wadau wakuu watatu katika mkondo wa juu wanayo maslahi ya leseni ya rasilimali ya petroli nchini Uganda. Hivyo, serikali ya Uganda (GoU) na Tanzania (GoT), pamoja na wadau wa mkondo wa juu, wanatarajia kutandaza bomba na miundombinu husika. Hatua za awali za maandalizi ya utekelezaji wa Mradi zitasimamiwa na kampuni ya kitanzania ya Total East Africa Midstream B.V. (TEAM B.V).

Mradi huu unatekelezwa kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, viwango vya Mradi kama vilivyoelekezwa kwenye Makubaliano ya Serikali Mbili na matakwa ya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa (IFI). Kulingana na viwango hivi, Sera mama ya mfumo wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RPF) imeandaliwa kwa ajili ya Mradi kwa sehemu ya Tanzania, na Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) mahususi utaandaliwa kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa kwenye Sera mama ya mfumo wa Uhamishati wa Watu una Makazi (RPF) kwa ajili ya Maeneo ya Awali

(PAs) pamoja na Mipango Kazi ya Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) za mikoa minane (8) iliyopitiwa na Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi.

Uwanda na Madhumuni ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera

Mradi nchini Tanzania utahitaji ardhi zaidi ya ekari 9, 884 (au hekari 4,000) ukijumuisha na sehemu ya ardhi ya mradi ya Mkoa wa Kagera. Takribani asilimia 90 ya ardhi itakayochukuliwa inajumuisha mkuza wa bomba na miundombinu ya juu ya ardhi. Katika Wilaya ya Muleba kuna Kituo namba 3 cha Kusukuma mafuta (PS-3) pamoja na njia za kukifikia na eneo la kufanyia kazi lisilolakudumu, vyote vipo katika Kijiji cha Kikagate, Kata ya Mabunda. Pia, Kambi kuu mbili (2) za makazi na kutunzia vifaa vya ujenzi zitajengwa katika Mkoa wa Kagera kama sehemu ya shughuli za awali kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa bomba. Ikiwemo: kambi namba 5 iliyopo katika Kijiji cha Kyaka, Kata ya Bulifani, Wilayani Missenyi; kambi namba 6 iliyopo ndani ya Kijiji cha Kiguzi, Kata ya Karambi, Wilayani Muleba. Kituo namba 3 cha Kusukuma mafuta ni sehemu ya huu Mpango Kazi ya Uhamishaji Watu na Makazi na Kambi kuu mbili (2) za makazi na kutunzia vifaa vya ujenzi ni sehemu ya maeneo ya awali katika Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa mkoa wa Kagera.

Uchaguzi wa mkuza wa Mradi umezingatia kupunguza athari za kimazingira na kijamii, hata hivyo baadhi ya miundo mbinu iliyohamishwa (kupoteza makazi) na changamoto za kiuchumi (Kuharibikiwa kiasi au kwa ujumla kwa ustawi wa maisha) kwa jamii hakuwezi kuepukika. Watu binafsi na kaya wameguswa kwa viwango tofauti.

Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi wa Mkoa wa Kagera unaonyesha, jumla ya watu walioguswa na Mradi wapatao 2,0941, makazi na taasisi zimebainishwa, ikiwemo wamiliki wa ardhi 1,786, wapangaji wa ardhi 277, vijiji 29 na taasisi moja (1) ya serikali.

[1] Hii inajumuisha Waguswa wa Mradi watano (5) ambao wana vipande vya ardhi katika vijiji zaidi ya kimoja.

Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera unafafanua sera, kanuni, taratibu, majukumu na wajibu wa kusimamia athari za uhamishaji utakaosababishwa na utwaaji wa ardhi ya Mradi kwenye Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo Mkoani Kagera.

Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera unalenga kuanzisha na kueleza:

- ☐ Muhtasri wa mfumo wa sheria;
- ☐ Watu binafsi na kaya ambazo zitaguswa na zoezi la uhamishaji wa watu na makazi na / au shughuli za kiuchumi, na jamii zitakazopata athari zinazohusiana na mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya Mradi;
- ☐ Namna ambavyo viwango vya fidia kwa ajili mali zilizopotea vilivyoafikiwa;
- ☐ Vigezo na stahiki kwa watu binafsi, kaya, na taasisi zilizoguswa na Mradi (ikiwa ni pamoja na chaguzi za fidia ya vitu au fedha);
- ☐ Mchakato uliotumika kubaini watu na vikundi vilivyo katika mazingira magumu;
- ☐ Viwango vya usaidizi kwa kaya zilizoguswa na Mradi wakati wa uhamishaji watu na makazi (ikiwa ni pamoja na watu na vikundi vilivyo katika mazingira magumu);
- ☐ Jitihada za urejeshaji wa ustawi wa maisha ya watu na kaya zilizoguswa;
- ☐ Majukumu na wajibu wa ufanyaji na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi;
- ☐ Mwongozo wa Mradi katika ushirikishaji wa wadau na mashauriano na waguswa wa Mradi pamoja na wadau wengine muhimu, ikiwa ni pamoja na Utaratibu wakutatua Malalamiko yanayohusiana na Mradi; na
- ☐ Shughuli zinazopaswa kutekelezwa, na kusimamia utwaaji wa ardhi, ulipaji wa fidia na urejeshwaji wa ustawi wa maisha ya watu waliomo katika Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi.

Mpango kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera umeandaliwa na Muungano wa Makampuni ya Digby Wells (DWC) kwa niaba ya na kwa usaidizi wa TEAM B.V kwa ajili ya sehemu ya Tanzania katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Muungano wa Makampuni haya unajumuisha Digby wells environmental (DWE) pamoja na makampuni ya kitanzania ambayo ni Whiteknights Real Estate Investment Analysts Co. Ltd. (WK), na PaulSam Geo-Engineering na Safety Training and Consulting Limited (STCL).

Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi wa Mkoa wa Kagera una jumla ya sura 13, ambapo kila moja ina sehemu muhimu ya mchakato wa Upangaji wa Uhamishaji Watu na Makazi. Mpangilio wa sura umeonyeshwa kwenye kielelezo namba moja (1) hapo chini;

Kielelezo namba ES 1: Sura za Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi – Kagera.

2. MAELEZO YA MRADI

Sura ya 2 inaeleza juu ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, ikiwa na lengo mahususi la kutoa maelezo ya utekelezaji kwa sehemu ya Tanzania. Kwa lengo la Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi wa Mkoa wa Kagera, sura hii inafafanua vipengele vya Mradi na mahitaji yanayohusiana na ardhi katika Mkoa wa Kagera na maeneo ya mamlaka za Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo.

Mradi unajumuisha Mkuza wa urefu wa kilomita zipatazo 1,443 na miundombinu inayohusiana na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Kituo cha kusukuma mafuta cha Kabaale kilichopo Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi kwenye miundombinu ya kusafirisha Mafuta ghafi kwenda nchi za nje kilichopo katika Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Kiasi cha bomba la inchi 24 lililofunikwa ili kuweza kutunza joto na kuchimbiwa ardhini lenye urefu wa kilomita zipatazo 296 litakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 litakuwa nchini Tanzania. Kwa ujumla Mradi utakuwa na miundombinu muhimu ambayo ni vituo sita (6) vya kusukuma Mafuta (viwili (2) vitakuwa nchini Uganda na vingine vinne (4) nchini Tanzania), vituo viwili (2) vya kupunguza kasi ya mafuta vitakuwa nchini Tanzania na kituo cha kuhifadhi mafuta kilicho pembezoni mwa bahari ya hindi (MST). Bomba litachimbiwa ardhini kwa kina cha mita 1.8 hadi mita 2.

Mkuza umesanifiwa ili kukidhi kusafirisha mapipa yapatayo 216,000 ya mafuta ghafi kwa siku moja (216 kbpd). Mafuta ghafi ya Uganda kwa asili ni kimiminika mnato. Ili mafuta yaweze kusafirishwa kwa ufanisi, linahitajika joto la zaidi ya nyuzi joto 50°C. Mfumo wa ufuatiliaji wa Joto la Umeme uliofungwa sambamba na bomba la mafuta ghafi utahakikisha kwamba joto linalotakiwa ni endelevu. Mfumo huu utapasha joto mafuta ghafi wakati bomba linafanya kazi na wakati wa vipindi vya kupungua kwa kasi ya mtiririko wa mafuta. Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika mashariki litakuwa bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa kutumia umeme.

Utandazaji wa bomba uliopendekezwa unaonyeshwa katika kielelezo cha pili cha ES - 2 ambapo Mikoa na Wilaya zilizoguswa zimeonyeshwa.

Mambo yanayohusu Mradi nchini Tanzania ni pamoja na miundombinu ya awali ambayo ni lazima itayarishwe kabla ya ujenzi wa bomba kuanza, na masuala yanayohusika na miundombinu ya Bomba lenyewe. Vipengele vya shughuli za awali

vimetajwa katika Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika maeneo ya vipaumbele, ambao umekamilika. Bomba na miundombinu yake inajumuisha:

- ☐ Upana wa mita 30 wa Ujenzi wa Mkuza wa Njia ya Bomba utatumika ambapo ndani yake, eneo la ukanda lenye upana wa mita 10 litahitajika moja kwa moja kwa ajili ya usalama wa shughuli na matengenezo ya njia ya bomba;
- ☐ Miundombinu ya Juu ya Ardhi nchini Tanzania ikiwemo: ujenzi wa vituo vinne (4) vya kusukuma mafuta na vituo viwili (2) vya kupunguzia kasi ya mtiririko wa mafuta;
- ☐ Kituo cha Kuhifadhia Mafuta kilicho pembezoni mwa Bahari (MST) na muundo mbinu wa Kupakia Mafuta (LOF) kwa ajili ya kuhamishia Mafuta Ghafi kwenda kwenye meli maalumu (tankers) na gati inayounganisha Kituo cha Kuhifadhia Mafuta kilicho pembezoni mwa Bahari (MST) na muundo mbinu wa Kupakia Mafuta MST na LOF.

Mchakato wa utwaaji wa ardhi ambao utakamilika kwa ajili ya miundombinu na maswala mengine ya Mradi umekua ni mada ya mjadala kati ya Mradi na Serikali ya Tanzania. Kufuatia majadiliano na Serikali na mapitio ya mkataba wa umiliki wa ardhi na mfumo wa kisheria wa Tanzania, mita 30 za mkuza wa njia ya bomba na Miundo Mbinu ya Juu ya Ardhi, itatwaliwa kwa kipindi cha kudumu. Inakusudiwa kwamba, ardhi yote inayohitajika na Mradi itahamishiwa kwenye Ardhi ya Jumla[2].

Ardhi inayohitajika ya mita 30 kwa ajili ya mkuza wa bomba na Miundo Mbinu ya Juu ya Ardhi itatwaliwa na Serikali ya Tanzania na baadaye kukodishwa kwa Kampuni ya Mradi.

[2] Isipokuwa ubadilishaji wa aina fulani ya miundombinu inayokatisha Mradi (kama hifadhi za barabara na njia za umeme). Matumizi ya ardhi ya eneo la mkuza inayokatiza miundombinu kama hiyo yataamuliwa na wakala husika na Serikali ya Tanzania.



Kielelezo cha 2 cha ES: Mkuza wa njia ya Bomba na maeneo yaliyoguswa na mradi

Vipengele vya Mradi na Mahitaji ya Ardhi Katika Mkoa wa Kagera

Mpango kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera umejikita katika mindombinu ya Mradi katika maeneo ya Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo. Miundombinu hiyo itahitaji ardhi yenye eneo la kilomita 1,430[3] na takribani ekari 1,197 ambazo zitakazothaminiwa na kufidiwa. Jedwali hapo chini linaonyesha muhtasari wa mahitaji ya ardhi.

Vidokezo muhimu kabla ya jedwali:

- ☐ Athari za moja kwa moja kata 20 kati ya 109 katika mkoa wa Kagera, pamoja na vijiji 31;

[3] Inajumuisha miundombinu inayokatiza katika mkuza na kipande kidogo kilichobaki katika ardhi iliyoguswa (ardhi yatima)

- ☐ Sehemu ya bomba katika Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba and Biharamulo inapita katika ardhi ya Vijiji na katika maeneo yaliyohifadhiwa;
- ☐ Katika vijiji vinavyoguswa, mradi unaathiri vipande vya ardhi vipatavyo 2,172;
- ☐ Maeneo ya Mapori Tengefu ya Minziro, Mto Ruiga na Biharamulo yanapitiwa na bomba katika Mkoa wa Kagera kwa akari 223;
- ☐ Mkuza wa bomba utakatisha katika barabara zipatazo 13 na nguzo za umeme 13 katika wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo;
- ☐ Mkuza wa Bomba katika Mkoa wa Kagera utakatiza katika njia 68 za vijiji, njia saba (7) za mifugo, mifumo mbalimbali ya maji (ikiwemo mto Kagera), njia za wapita kwa miguu na mabwawa mawili (2).

Jedwali ES - 1: Kata na Makazi Kandokando ya Mkuza wa Bomba

Wilaya	**Kata**	**Kizio cha kilomita cha karibu zaidi (KP)**		**Urefu wa Bomba (km)**	**Ukubwa wa eneo la ardhi (Ekari)[4]**
		Kuanza	**Kumaliza**		
Missenyi	Mutukula	296	301.5	5.49	41.37
	Nsunga	301.5	314	12.76	95.11
	Kassambya	314	324	10	75.46
	Kyaka	324	327.5	3.53	26.41
	Kilimilile	327.5	335.5	7.66	57.42
Bukoba	Kyamulaile	335.5	342.5	7.35	56.09
	Mugajwale	342.5	353	5.04	82.89
	Kyaitoke	353	359	5.93	48.85
	Izimbya	359	361	1.86	13.91
	Kyaitoke	361	363.5	2.86	21.63
	Kibirizi	363.5	371	7.13	56.12
	Rukoma	371	373.5	2.88	22.43
Muleba	Ngenge	373.5	394.5	20.9	169.03

[4]Hii inajumuisha sehemu za ardhi zilizorekodiwa kama kipande kidogo kilichobaki katika ardhi iliyoguswa (ardhi yatima) wakati wa shughuli za kuthamini ardhi, hifadhi za barabara na nguzo za umeme ambazo Mradi hautazichukua.

Wilaya	Kata	Kizio cha kilomita cha karibu zaidi (KP)		Urefu wa Bomba (km)	Ukubwa wa eneo la ardhi (Ekari)[4]
		Kuanza	Kumaliza		
	Burungura	394.5	401.5	6.81	53.54
	Mubunda	401.5	407.5	6.25	94.40
	Bisheke	407.5	410	2.45	29.67
	Kasharunga	410	419	8.85	79.46
	Karambi	419	435	5.29	125.8
	Kyebitembe (ikiwemo hifadhi ya msitu wa mto Ruiga na pori la akiba la Biharamulo)	435		444.5	79.77
Biharamulo	Nyarubungo (pori la akiba la Biharamulo)	444.5	463	18.13	142.79
Chato[5]	*Bwongera*	*463*	*466.5*	*3.43*	
Biharamulo	Nyarubungo (pori la akiba la Biharamulo)	466.5	467.5	1.00	7.32
Chato[6]	*Ichwankima, Nyamirembe, Ichwankima, Ilemela, Katende*	*467.5*	*503*	*35.82*	
Biharamulo	Nyamigogo	503	510	6.73	50.85

[5] Mkuza wa Bomba unapita wilaya ya Chato (Kata ya Bwongera) kwa kilomita 3.43 kabla ya kurudi wilaya ya Biharamulo, kata ya Nyarubungo.

[6] Mkuza wa Bomba ndani ya mipaka ya pori la akiba la Biharamulo unapita wilaya ya Chato (Kata ya Ichwankima) kwa kilomita 9.4 kabla ya kutoka pori la akiba la Biharamulo kuingia wilaya ya Chato zaidi kwa kilomita 26.42 na kuingia tena wilaya ya Biharamulo.

Wilaya	Kata	Kizio cha kilomita cha karibu zaidi (KP)		Urefu wa Bomba (km)	Ukubwa wa eneo la ardhi (Ekari)[4]
		Kuanza	Kumaliza		
Jumla kwa mkoa wa Kagera				**174.58**	**1 430**

3. MUKTADHA WA SHERIA NA SERA

Sura ya 3 inaelezea muktadha wa sheria na Sera ya Mradi. Sura inawasilisha kwa mapana sheria, sera, viwango na miongozo inayohusiana na RAP ya Mkoa wa Kagera. Mambo hayo yametokana na Mfumo wa sheria za Tanzania, Viwango vya Washiriki wa Mradi pamoja na Viwango vya Uwezeshaji wa Kifedha vya Kimataifa vinavyohusiana na utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi.

Mradi huu utapaswa kukidhi matakwa ya sheria ya Tanzania ya utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi. Mradi umedhamiria kuzingatia Viwango vya fedha vya Kimataifa (IFS) vilivyopo katika kanuni za Ikweta Namba III na Viwango vya Utendaji (PS) vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC).

Mfumo wa Sheria ya Tanzania

Tanzania ina sheria anuai na sera zinazohusiana na aina za ardhi, umiliki wa ardhi, utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi.

Kwa mujibu wa sheria za Tanzania, ardhi ipo katika aina zifuatazo:

- ☐ **Ardhi ya hifadhi**: Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya wanyama pori, misitu, hifadhi za baharini, hifadhi za barabara na maeneo yanayofanana na hayo;
- ☐ **Ardhi ya Kijiji:** Ardhi ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa, ambapo Halmashauri za vijiji na mkutano mkuu ya kijiji una mamlaka ya usimamizi wa ardhi; na
- ☐ **Ardhi ya Jumla:** Ardhi ambayo haijahifadhiwa wala sio Ardhi ya kijiji na kwa hiyo iko chini ya usimamizi wa Kamishna wa Ardhi.

Ardhi iliyoguswa katika Mkoa wa Kagera ni Eneo la ardhi ya vijiji na ardhi iliyohifadhiwa.

Sheria na sera zinazoongoza zoezi la utwaaji wa ardhi na taratibu za fidia nchini Tanzania zipo katika makundi makubwa matatu:

- ☐ **Sheria Mama na Miongozo**: inayojumuisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1997), Sera ya Taifa ya Ardhi (1997, kama ilivyorekebishwa) na Sheria ya Petroli (Na .8 ya 2015);

- ☐ **Sheria ya Ardhi:** inayojumuisha sheria zinazohusiana na maswala ya ardhi, utwaaji wa ardhi, kanuni za ardhi, uondoaji na uhamishaji makaburi, mali kale, uthamini na wathamini, misitu, usimamizi wa barabara, mbuga za taifa na hifadhi bahari; na
- ☐ **Sera Husiani:** inayojumuisha sera zinazoelezea maendeleo ya makazi ya watu, misitu, kilimo, mifugo na maji.

Mazingira ya Ushirika, Viwango vya Kijamii na Kujitolea.

Washirika wa Mkondo wa juu, Total Exploration and Production (E&P) Uganda B.V. (TEPU), Tullow Uganda Operations Pty Ltd (TUOP) na China National Offshore Oil Corporation (CNOOC) Uganda Limited (CUL) wanazo sera za ushirika zinazohusu majukumu ya kijamii. Majukumu hayo ni pamoja na mambo yanayohusiana na mazingira, afya na usalama, maadili, ulinzi wa bioanuwai na shughuli katika mazingira nyeti.

Makubaliano baina ya Serikali Mbili (IGA) na Makubaliano ya Serikali Mwenyeji (HGA)

Mkataba wa Makubaliano baina ya Serikali mbili ulisainiwa na Serikali za Uganda na Tanzania mnamo tarehe 26 Mei, 2017. Ndani ya mkataba huu, Ibara ya 3 inaweka mfumo wa haki za ardhi katika Mradi.

Mikataba ya Serikali Mwenyeji baina ya wadau wa Mkondo wa juu na Serikali ya Uganda pamoja na Serikali ya Tanzania yatafuata baada ya Makubaliano baina ya Serikali mbili (IGA). Wakati mikataba ya Serikali Mwenyeji iko katika maandalizi na ikiwa bado haijasainiwa, Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) wa mkoa wa Kagera ulitumia kanuni za mkataba wa makubaliano baina ya serikali mbili, kuhakikisha uzingatiaji wa michakato iliyotumika kuandaa RAP katika mkoa wa Kagera. Michakato hii inajumuisha tafiti za kiuchumi-jamii na rasilimali, mbinu za uthamini na uamuzi wa fidia wa fedha na mali.

Mwongozo na Viwango vya Kimataifa.

Katika muktadha wa Viwango na Mwongozo wa Kimataifa, Mradi na RAP ya mkoa wa Kagera vinazingatia masharti ya kanuni za Ikweta Namba III na Viwango vya Utendaji (PS) vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC):

- ☐ Kanuni za Ikweta ni nyenzo iliyokubaliwa na taasisi mbalimbali za kifedha kwa ajili ya kutambua, kutathmini na kusimamia hatari zinazoweza kutokea katika mazingira na jamii. Kwa kuwa Mradi unaweza kuomba fedha kutoka katika Taasisi za kifedha zinazotumia misingi ya fedha ya Ikweta, misingi na miongozo ya Ikweta juu ya utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi ni muhimu na inatumika; na
- ☐ Viwango vya Utendaji Vya Shirika la Fedha la Kimataifa hutoa miongozo na viwango juu ya usimamizi wa miradi inayoendana katika masuala ya athari zinazoweza kutokea katika jamii na mazingira na uboreshaji wa fursa za maendeleo.

Kati ya kanuni nane (8) za Viwango vya Utendaji cya Shirika la Fedha la Kimataifa, nne (4) kati ya hizo zinahusiana moja kwa moja na RAP ya mkoa wa Kagera hasa zifuatazo:

- ☐ **Kiwango cha Utendaji (PS) 1 Tathmini na Usimamizi wa hatari na athari za kimazingira na kijamii:** Kiwango cha utendaji hushauri, pamoja na mambo mengine, juu ya usimamizi fanisi wa hatari ya athari za kijamii, hatari zingine na fursa;
- ☐ **Kiwango cha Utendaji (PS) 5 Utwaajiwa Ardhi na kuhamishwa watu na makazi kwa lazima**:PS hutoa mwongozo hatua kwa hatua juu ya upangaji na utekelezaji wa shughuli ili kupunguza athari za uhamishaji watu na makazi na uhamaji ili kurejesha na kuboresha ustawi wa maisha na viwango vya kuishi;
- ☐ **Kiwango cha Utendaji (PS) 7 Wazawa wa Asili**: PS inaelezea usimamizi wa athari za kijamii baina ya makundi yenye tamaduni tofauti zinazohusishwa na ardhi asili na maliasili zake pamoja na vitu vingine; na
- ☐ **Kiwango cha Utendaji (PS) 8 Urithi wa Kiutamaduni**: PS hushauri juu ya uhifadhi wa urithi wa Kitamaduni ambao upo hatarini kupotea kutokana na athari za kijamii.

Kama sehemu ya mfumo wa Makubaliano baina ya serikali mbili, Mradi umekubali kushughulikia Viwango vya Haki za Binadamu katika ngazi za kitaifa na kimataifa, ukiongozwa na matendo mema pamoja na kanuni na misingi ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu.

Uchambuzi wa Pengo

Uchambuzi wa pengo baina ya mahitaji ya kisheria ya Tanzania na viwango vya IFC umefanyika. Mapungufu yamebainishwa katika muktadha wa uthamini, tafiti za kiuchumi -jamii, stahiki na stahiki ya tarehe ya katazo, fidia, msaada wa uhamishaji watu na makazi, watu walio katika mazingira magumu na muda wa malipo ya fidia. Pale ambapo mapungufu yamebainishwa, RAP ya mkoa wa Kagera (na RAP nyingine zote za Mradi) zitatumia viwango vyenye nguvu zaidi kati ya hivi viwilii.

4. MUHTASARI WA MPANGO WA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI, KANUNI NA MICHAKATO

Sura ya 4 ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera unaelezea kwa kina vipengele vikuu vya mchakato wa utwaaji wa ardhi na mchakato wa mpango wa uhamishaji wa watu na makazi. Mpango wa Uhamishaji wa watu na makazi na utekelezaji wake ni mgumu, unahitaji mchakato unaoeleweka na uliopangiliwa pamoja na shughuli na matokeo yake. Hatua za mchakato umefafanuliwa na kuelezewa, na mlolongo wa hatua zake kuelezewa.

Mchakato wa Utwaaji wa Ardhi na Uhamishaji Watu na Makazi

Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi katika mkoa wa Kagera utazingatia ipasavyo mchakato uliosanifiwa wa utwaaji wa ardhi na uhamishaji watu na makazi wenye hatua 3. Mchakato umeelezwa katika kielelezo ES – 3 na kufafanuliwa katika sura ya nne (4). Kielelezo namba ES- 4 kinaonyesha mchakato wa hatua uliochukuliwa kwenye kila hatua;



Kielelezo ES-3: Muhtasari wa Mchakato wa Utwaaji wa Ardhi na Uhamishaji Watu na Makazi.



Kielelezo ES - 4: Mchakato wa Utwaaji wa Ardhi

Maudhui ya hatua hizi yamefafanuliwa hapo chini:

Hatua ya 1: Uendelezaji wa Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi

Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi unaelezea kanuni kuu za utwaaji wa ardhi, fidia na mpango wa uhamishaji watu na makazi na kuhakikisha mwendelezo wa shughuli zote za Mpango wa Uhamishaji watu na makazi kwa kujumuisha jumla ya Mipango yote tisa ya Uhamishaji Watu na Makazi na Ripoti za Uthamini (VRs) zinazohusiana. Mfumo wa Sera ya Uhamishaji watu na Makazi umeandaliwa na kupitia Kipindi cha ukusanyaji maoni toka Serikali ya Tanzania, mchakato uliokamilika mnamo Septemba 2018 baada kupokea maoni ya Serikali ya Tanzania. Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi ulitolewa kwa umma mnamo Oktoba 2018.

Hatua ya 2: Kukamilika kwa Shughuli za Awali za Utwaaji wa Ardhi (Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi)

Jedwali hapo chini linaeleza muktadha na maudhui ya shughuli za Hatua ya 2 na hatua ya maendeleo yake (katika kipindi cha majumuisho ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera).

Jedwali la ES-2: Shughuli za Hatua ya 2

Shughuli za Hatua ya 2	Mkutadha na Maelezo
Uteuzi wa njia ya mkuza	Mkuza wa Bomba la Mafuta uliwekwa bayana na timu ya wahandisi wa Mradi wa EACOP inayofanya kazi na wataalamu wa taaluma zingine pamoja na wakandarasi. Vigezo vya uteuzi wa maeneo ya Mradi vilizingatia maswala ya kiufundi, kimazingira, na mambo muhimu ya kiuchumi-jamii na urithi wa kiutamaduni. Maeneo nyeti yalikwepwa (kama vile hifadhi zilizotengwa za kimataifa) na uhamishaji wa watu na makazi ulipunguzwa kadiri ilivyowekana.
Uchunguzi wa Kina na Uthamini	Upangaji na Maandalizi Mpango wa uchunguzi wa kina ulitumika katika kuelezea Ripoti za Uthamini na RAP. Upangaji na Maandalizi vilijumuisha uandaaji wa vifaa bora vya uchunguzi, mafunzo kwa timu za watafiti na upangiliaji wa timu. Katika timu zote za uchunguzi walikuwemo pia Watanzania, wenye taaluma maalumu kulingana na lengo la kundi la uchunguzi (Mfano uhamasishaji wa jamii, uainishaji ardhi na uthamini wa mali)

Shughuli za Hatua ya 2	Mkutadha na Maelezo
	Uundaji wa Viwango Wathamini waliosajiliwa (RV) kwa ajili ya Mradi walifanya utafiti wa soko katika mkoa wa Kagera ili kujua thamani na gharama ya fidia ya vitu mbadala. Ripoti ya viwango vya thamani iliandaliwa na kukabidhiwa kwa Mthamini Mkuu (CV) kwa ajili ya kupata idhini.
	Utekelezaji wa Uchunguzi Uchunguzi, kwa kiwango kikubwa ulifanywa kwa utaratibu ufuatao: ☐ Uhamasishaji wa Jamii, pamoja na majadiliano na viongozi wa serikali za mitaa, mikutano ya uhamasishaji jamii na kutangazwa kwa mwanzo wa tarehe za makatazo za uchunguzi wa kina na uthamini; ☐ Utambuzi wa ardhi na uamuzi wa kesi za ardhi, ikiwa ni pamoja na kutunza taarifa za mipaka ya vipande vya ardhi, kupiga picha, na kutoa Fomu ya Ardhi Namba 69 itakayosainiwa na Afisa Ardhi wa Wilaya (DLO); ☐ Uthamini wa mali, ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu kwa uangalifu wa taarifa za mali zilizoguswa na maeneo ya kiutamaduni, kufanya majumuisho ya orodha ya mali, kupiga picha na kurekodi maeneo na kuhakikisha nyaraka husika zimetiwa saini na Mthamini aliyesajiliwa (RV), Watu Walioguswa na Mradi (PAPs) na wawakilishi wa serikali za mitaa; ☐ Taarifa za kiuchumi-jamii, ikiwa ni pamoja na hali ya kiuchumi na kijamii za watu na kaya zilizoguswa na Mradi; na ☐ Kutangaza orodha ya Mali
Taarifa ya Uthamini na Jedwali la fidia	Uthibitishaji wa mali Kufuatia orodha ya taarifa ya mali iliyotangazwa, Watu Walioguswa na Mradi (PAPs) walipewa fursa ya kutoa maoni na matakwa yao juu ya utambuzi wa mali. Marekebisho yalifanyika pale ilipobidi, baada ya uthamini wa mali kufanyika na fidia kupangwa.
Taarifa ya Uthamini na Jedwali la fidia	Majumuisho ya Ripoti za Uthamini Baada ya mchakato wa uthibitishaji wa mali kukamilika, Wathamini waliosajiliwa walikamilisha nyaraka za taarifa ya uthamini na Fidia kwa Mkoa wa Kagera kwa kila Wilaya. Kila

Shughuli za Hatua ya 2	Mkutadha na Maelezo
	taarifa ya Uthamini na jedwali la fidia vilitayarishwa kwa ajili ya kulipa fidia ya vitu kwa upande wa Tanzania na stahiki za nyongeza kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya fedha vya Kimataifa.
	Uonyeshwaji wa taarifa za majedwali ya Fidia Sheria ya Tanzania inahimiza uwekaji wazi wa majedwali ya Fidia na maelezo ya fidia kwa waguswa wa Mradi. Kipindi cha siku (7) cha ukaguzi hujumuishwa katika mchakato wa utoaji taarifa. Katika RAP ya mkoa wa Kagera, hatua za usambazaji taarifa zifuatazo zilitumika: ☐ Kushirikiana na vyombo vya serikali kueleza mchakato wa kutoa taarifa kwa uwazi; ☐ Kukutana na vijiji pamoja na watu walioguswa na Mradi ili kuwasilisha matokeo ya uthamini. Katika mchakato huu iliamuliwa kuwa maelezo kamili ya majedwali ya Fidia yawekwe wazi kwa kila mguswa; na ☐ Kukamilisha shughuli zozote za uthamini ikiwa ni pamoja na kupitia madukuduku kama yalivyotolewa na watu walioguswa wa Mradi. Shughuli za uthamini zilizofanywa wakati wa mchakato wa uwekaji wazi taarifa katika Mkoa wa Kagera zilizingatia tarehe ya uthamini wa maslahi ya mali za mguswa wa mwisho.
	Utiaji saini, Uwasilishaji na Uhakiki wa Ripoti za Uthamini Mara tu baada ya Ripoti za Uthamini (VRs) na majedwali ya Fidia kukamilika ikiwa ni pamoja na majibu ya mrejesho wa watu walioguswa na Mradi, orodha ya mwisho ya Fidia lazima iidhinishwe na Mthamini wa uwandani, Mthamini kiongozi, Afisa mtendaji wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Ardhi aliyeidhinishwa, mthamini aliyeidhinishwa na Mkuu wa Wilaya. Mthamini mkuu ndiye mwenye dhamana ya mwisho wa kuidhinisha, baada ya hapo fidia inaweza kulipwa.
Uchunguzi wa Kichumi, kijamii na Ustawi wa Maisha	Upangaji na Maandalizi Uchunguzi wa Kiuchumi-jamii na ustawi wa maisha wa RAP katika mkoa wa Kagera ulitoa taarifa zilizowezesha uandaaji wa maswala mengi katika RAP, ikiwa ni pamoja na hali ya watu waishio katika mazingira magumu, namna ya kuzuia hatari na chaguzi za namna ya kurejesha wa ustawi wa maisha. Uandaaji wa kikosi cha uchunguzi wa kiuchumi-jamii na ustawi wa maisha

Shughuli za Hatua ya 2	Mkutadha na Maelezo
	ulihusisha utambuzi wa Mradi, mafunzo na uundaji wa zana za utafiti, na mafunzo katika eneo la Mradi.
	Utekelezaji wa Utafiti Shughuli za Uchunguzi wa Kiuchumi-jamii na ustawi wa maisha katika maeneo husika kwenye RAP ya mkoa wa Kagera zilifanyika kati ya tarehe 30 October mpaka 31 Januari 2019.
	Mbinu za ushirikishi: Mbinu za ushirikishi wa Makundi Lengwa na Mahojiano ya Watoa Taarifa Wakuu zilitumika. Mbinu ya awali ilitumika hasa katika muktadha wa jamii, na mbinu nyingine ilitumika kwa watu wenye ushawishi katika jamii na viongozi wa serikali za mitaa. Ufuatiliaji wa majadiliano katika vikundi vidogo ulitoa fursa ya washiriki katika Makundi Lengwa kufanya majadiliano bila hofu na katika mazingira rafiki.
	Matokeo na Utoaji Taarifa Matokeo ya Uchunguzi wa kiuchumi, kijamii na ustawi wa maisha yaliongeza data za kiuchumi-jamii na hivyo kuchangia katika kuboresha maendeleo katika Mpango wa uboreshaji wa ustawi wa maisha, na Mpango kwa watu waishio katika mazingira magumu walioguswa na Mradi, na kutoa uelewa wa kimazingira kwa kabila zilizo katika mazingira hatarishi.
Uchunguzi wa Ardhi na Makazi Mbadala	Uchunguzi wa kina wa makazi mbadala umefanyika katika muktadha wa ujenzi kwenye maeneo ya kipaumbele (PA), yaliyoandaliwa kwa ajili ya RAP kwa mtazamo wa kuongeza shughuli za uchunguzi kwenye maeneo yote yaliyoguswa na Mkuza. Vifuatayo ni vipengele muhimu vya uchunguzi: ☐ Timu inayojumuisha wasanifu majengo waliosajiliwa na wathamini majengo (Watanzania na wa Wakimataifa) ☐ Uhakiki wa miundombinu iliyoguswa katika maeneo ya Mradi pamoja na mambo mengine kama vile idadi ya miundombinu, ukubwa, mpangilio, vifaa, matumizi ya eneo, idadi ya wakazi na utwaaji wa huduma za jamii; ☐ Ziara kwa wasambazaji wa vifaa vya ujenzi;

Shughuli za Hatua ya 2	Mkutadha na Maelezo
	☐ kuendeleza wazo la Usanifu; na ☐ Utayarishaji wa ubunifu wa wazo la usanifu kwa mikoa minane (8) iliyoathiriwa na Mkuza.
Uandaaji wa RAP	Matokeo ya shughuli za awali za utwaaji wa ardhi (Hatua ya 2) yameandikwa katika RAP ya mkoa wa Kagera. RAP ya mkoa wa Kagera itawasilishwa katika Serikali ya Tanzania, baada ya kukamilika kwa rasimu ya mwisho itakayojumuisha maoni yote ya serikali ya Tanzania. RAP ya mkoa wa Kagera itakayotolewa na kupatikana kwa urahisi na waguswa wa Mradi na wadau wakuu wa Mradi. RAP ya mkoa wa Kagera itawekwa wazi kwenye tovuti ya Mradi wa EACOP.

Hatua ya 3 ya (Utekelezaji wa Mpango kazi wa Uhamishaji wa watu na makazi (RAP), haujafafanuliwa katika kipengele hiki hivyo rejea sehemu ya 11 ya Muhtasari huu kwa maelezo zaidi.

5. MUHTASARI WA WATU NA MALI ZILIZOGUSWA

Sura ya 5 inaelezea Maeneo, Makazi (Vijiji), Kaya na Watu Walioguswa na Mradi kwa kuzingatia athari za uhamaji zinazohusiana na Mradi. Shughuli zinazofafanuliwa katika Sura ya 5 ni muhimu katika RAP ya mkoa wa Kagera, kwa kuwa unabainisha stahiki, fidia, na watu wanaoishi katika mazingira magumu, na kuweka vigezo vya ufuatiliaji na tathimini.

Sura ya 5 ni muhtasari wa mali na watu walioguswa na Mradi katika Mkoa wa Kagera. Sura hii inatoa muhtasari wa:

- ☐ Mkoa wa Kagera;
- ☐ Wilaya zilizoguswa na Mradi (Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo);
- ☐ Jamii zilizoguswa na Mradi; na
- ☐ Kaya zilizoguswa na Mradi.

Muundo uliotumiwa katika mwongozo wa Kiuchumi-jamii katika taarifa za awali kwenye sura ya 5 umeonyeshwa kwenye kielelezo ES- 5 kifuatacho:



Kielezo ES - 1 : Maeneo Yaliyoguswa na Mradi

Ni muhtasari wa kundi la pili pekee ambao umefafanuliwa katika muhtasari huu. Athari kuu za uhamaji (zilizotengwa kikata) zimeonyeshwa katika jedwali Na. ES – 3.

Jedwali ES - 2 : Muhtasari wa athari za uhamishaji mkoani Kagera

District	Ward	Pipeline Length (km)	Land Parcels (No.)	Land Area (acres)	PAPs (No.)	PAHs (No.)	Vulnerable PAHs (No.)	Vulnerable Ethnic Group PAHs (No.)	PAHs Losing Dwellings	Buildings and Structures Affected (No.)			Crops Affected			Economic Trees and Other Trees (No.)	Graves
										Residential Dwellings	Other Structures	Incomplete Structures	Crops Acres	Intercropping Acre	Crops Stems		
Missenyi	Mutukula	5.49	76	41.20	62	56	14	1	2	3	7	1	2.97	4.16	6021	6769	6
	Nsunga	12.52	67	94.94	63	52	18	0	2	2	1	0	17.67	0.86	1352	18806	0
	Kassambya	9.91	184	70.53	192	163	63	0	15	15	23	3	12.64	6.13	30936	20614	30
	Kyaka	3.53	45	26.07	53	46	24	0	0	0	1	0	4.27	1.84	3753	3968	19
	Kilimilile	7.66	75	56.76	64	61	27	0	3	3	0	0	14.12	1.59	5431	4814	6
Bukoba	Kyamulaile	7.35	23	55.89	21	19	9	0	2	3	2	1	0.31	0.00	640	709	0
	Mugajwale	10.36	215	82.31	216	196	76	0	10	11	5	6	7.18	11.0	22371	16088	8
	Kyaitoke	5.93	145	47.41	146	138	38	0	12	12	16	5	1.80	14.51	7009	17955	18
	Izimbya	1.86	4	13.91	2	1	0	0	0	0	0	0	0.00	0.00	0	0	0
	Kyaitoke	2.86	3	21.63	2	1	0	0	1	1	0	0	0.00	0.00	0	0	0
	Kibirizi	7.13	71	55.24	64	55	20	0	1	1	0	2	0.93	8.80	1169	3411	3
	Rukoma	2.88	5	22.29	18	16	6	0	0	0	0	0	3.70	0.01	19	0	0
Muleba	Ngenge	20.9	484	167.81	455	410	175	0	23	24	41	3	19.23	35.6	8039	16378	42
	Burungura	6.81	139	53.54	122	113	76	0	8	8	1	1	7.72	10.15	1697	3385	10
	Mubunda	6.25	61	94.3	61	56	28	0	7	10	13	1	7.6	3.48	693	280	2
	Bisheke	2.45	26	29.58	33	30	19	0	3	4	6	0	4.62	3.06	1011	540	0
	Kasharunga	8.85	217	78.98	213	201	61	0	8	8	20	0	20.41	10.7	8191	3502	9
	Karambi	15.86	279	125.4	257	239	109	0	8	8	14	1	22.96	13.99	8458	5860	9
	Kyebitembe	1.06	13	8.14	12	11	5	0	0	0	1	0	1.92	0.17	122	35	0
Biharamulo	Nyamigogo	6.73	40	50.85	38	37	15	0	2	3	1	0	12.93	2.90	392	130	3
TOTAL: KAGERA REGION		**146.39**	**2172**	**1196.97**	**2094**	**1901**	**783**	**1**	**107**	**116**	**152**	**24**	**162.98**	**128.95**	**107304**	**123244**	**165**

Maelezo ya Jumla ya Kaya Zilizoguswa na Mradi

Maelezo ya jumla ya idadi na sifa za Kaya zilizoguswa na Mradi (PAH's) katika Kata zote zilizoguswa (katika kila wilaya) zimeonyeshwa kwenye jedwali ES - 4 lifuatalo:

Jedwali ES - 4: Muhtasari wa Kaya Zilizoguswa na Mradi kwa kila Kata

Wilaya	Kata	Idadi ya PAHs[7]	Idadi ya PAPs[8]	Uwiano (%) wa Kaya zilizoguswa kwa PAC	Wastani wa Ukubwa wa PAH	Mkuu wa Kaya (%)		PAHs zinaoishi katika eneo kwa kudumu (%)
						Me	Ke	
Missenyi	Mutukula	62	56	1.5	7	77	23	Wakudumu
	Nsunga	63	52	1.0	6	88	12	Wakudumu
	Kasambya	192	163	2.5	5	71	29	Wakudumu
	Kyaka	53	46	1.5	6	66	34	Wakudumu
	Kilimilile	64	61	2.4	6	84	16	Wakudumu
Bukoba	Kyamulaile	21	19	0.6	6	79	21	Wakudumu
	Mugajwale	216	196	8.3	5	80	20	Wakudumu
	Kyaitoke	148	139	5.9	5	75	25	Wakudumu
	Izimbya	2	1	0.02	3	100	0	Wakudumu
	Kibirizi	64	55	3.1	6	89	11	Wakudumu
	Rukoma	18	16	0.6	6	100	0	Wakudumu
Muleba	Ngenge	455	410	9.7	6	85	15	Wakudumu
	Burungura	122	113	4.1	6	90	10	Wakudumu
	Mubunda	42	39	1.6	7	95	5	Wakudumu
	Mabunda (inc. PS-3)	19	17					
	Bisheke	33	30	0.8	7	93	7	Wakudumu

[7] Inahusisha taasisi za kiserikali na uongozi wa vijiji.

[8] Kati ya hizi, 66 PAHs hawakukamilisha utafiti wa kiuchumi-jamii.

Wilaya	Kata	Idadi ya PAHs[7]	Idadi ya PAPs[8]	Uwiano (%) wa Kaya zilizoguswa kwa PAC	Wastani wa Ukubwa wa PAH	Mkuu wa Kaya (%)		PAHs zinaoishi katika eneo kwa kudumu (%)
						Me	Ke	
	Kasharunga	213	201	3.8	6	78	22	Wakudumu
	Karambi	257	239	6.3	6	86	14	Wakudumu
	Kyebitembe	12	11	0.2	7	91	9	Wakudumu
Biharamulo	Nyamigogo	38	37	1.7	9	78	22	Wakudumu
JUMLA		**2 094**	**1 901**	**2.6**	**6**			-

Kati ya Waguswa wa Mradi wapatao12,094[9] walioguswa, makazi na taasisi zimekwishatambulika na Mradi, ikiwemo wamiliki wa ardhi 1,786, wapangaji 416, vijiji 29 na taasisi ya kiserikali moja (1).

Kuna PAH 1,901, Sehemu kubwa ya PAHs ipo katika Wilaya ya Muleba (1,060), ikifuatiwa na Wilaya ya Bukoba (426) na Wilaya ya Missenyi (434). Wilaya ya Biharamulo ina PAHs 37. Kati ya kaya hizo, moja (1) inajitambulisha kama wabarabaig.

Shughuli kuu kwa asilimia kubwa ya Kaya zilizoguswa na Mradi za Mkoa wa Kagera ni kilimo, wastani wa asilimia 76 ya PAHs walioeleza kuwa wanategemea uuzaji wa mazao ya kilimo kama shughuli kuu ikifuatiwa na wastani wa asilimia 15 ya kaya zinazotumia kilimo kwa ajili ya kujikimu tu. Kwa ujumla, Kaya zilizoguswa na Mradi zilizoeleza kuuza mazao kama shughuli yao kuu, wanafanya shughuli nyingine kama kuuza mazao ya mifugo, biashara ndogo ndogo na vibarua ili kujikidhi kiuchumi. Vilevile iligundulika kuwa PAHs wanaotegemea kazi za mishahara na vibarua kama shughuli kuu, walikuwa pia wanategemea uuzaji wa mazao na kilimo cha mazao ya chakula chao kama shughuli za ziada za kuwaingizia kipato.

[9] Hii inahusisha waguswa wa Mradi watano (5) wenye vipande vya ardhi katika vijiji zaidi ya kimoja

PAHs wa wilaya ya Missenyi walitoa taarifa za mazao makuu ikiwa ni mahindi (26%), maharage (22%), kahawa (19%) na ndizi (14%). Kahawa ndilo zao muhimu Zaidi katika wilaya ya Bukoba (29%). Katika wilaya ya Muleba, mazao muhimu yanayolimwa na PAHs yalitajwa kuwa mihogo (25%), mahindi (23%), maharage (18%), Kahawa (10%) na mchele (7%). Katika wilaya ya Biharamulo, mazao muhimu yanayolimwa na PAHs yalitajwa kuwa Katani (38%), mahindi (25%), mihogo (19%) na mchele (16%).

Kwa kuwa uwezo wa kupata umeme katika gridi ya Taifa ni mdogo, kaya nyingi zinatumia vibatari na taa za kutumia betri kwa madhumuni ya kujipatia mwanga. Kuni zinatumiwa sana na PAHs kwa kupika, isipokuwa PAHs wa Kata za Mutukula, Kasambya and Kyebitembe ambao wanatumia mkaa. Kutokana na ukosefu wa maji ya bomba, kuna vyanzo mbalimbali vya maji ikiwemo visima vya jamii, vyanzo vya maji vilivyofadhiliwa na serikali, wauza maji na mito na maji yanayotiririka, PAHs wengi wanatumia zaidi mito na maji yanayotiririka, ambavyo vina maji yasiyo salama.

Msaada wa Maendeleo

Kaya zilizoguswa na Mradi zilibainisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kama mchango mkubwa katika kupata chakula cha kutosha na maendeleo ya kiuchumi. PAHs wengi hawana mbinu ya kupata mbegu, dawa za wadudu na mbolea bora. Kuhusu nyenzo, nusu ya PAHs walionyesha kutumia kilimo cha kutumia plau na moja ya tatu ya PAHs wanatumia jembe la mkono. PAHs wachache sana wenye uwezo wa kutumia trekta. Wafugaji wataja changamoto zinazowakabili ikiwemo ukosefu wa maeneo ya kuoshea mifugo, chanjo za mifugo, dawa na huduma za madaktari wa mifugo na ukosefu wa maeneo ya malisho.

Kwa ujumla, changamoto zilizotajwa ni pamoja na ukosefu wa maji na umbali wa vyanzo vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kilimo. Upatikanaji wa maji ya kumwagilia ilionekana kama hitaji muhimu sana. PAHs walitoa dukuduku lao kuhusu mradi kuchangia ukosefu wa maji kwenye maeneo yao. Pia kundi kubwa la PAHs liliorodhesha uboreshwaji wa barabara kama sehemu ya kipaumbele cha maendeleo ili kufikia masoko kwa urahisi.

Kabila zilizo katika hali hatarishi

Makabila yaliyo katika mazingira magumu, ambayo baadhi yake yanaweza kujitambulisha kama wazawa wa asili, hubainishwa kama kikundi cha watu wazawa wa asili wa eneo fulani na ambao wana tabia za kijamii na kitamaduni tofauti na makundi mengine. Tamaduni za makabila yaliyo katika hali hatarishi yana uhusiano

mkubwa na mazingira na maliasili zake. Kimsingi, shughuli za kimila, uchumi, kijamii na kisiasa katika makabila haya zinatofautiana na jamii nyingine.

Katika muktadha wa Tanzania, makabila manne (4) yaliyo katika mazingira magumu yanatambuliwa kimataifa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu kama wazawa wa asili. Makabila haya ni Wahadzabe, Wamasai, Wabarabaig na Waakie. Ijapokuwa Wasandawe pamoja na Wahadzabe walichukuliwa kuwa ni vikundi vya wawindaji na wakusanyaji nchini Tanzania, kwa sasa Wasandawe wameacha maisha ya kutegemea shughuli za uwindaji na ukusanyaji asili, wameanza kuendesha maisha yao kwa kilimo. Kwa sasa Wahadzabe wanatambulika kimataifa kama wazawa asilia, wakati Wasandawe sio[10]. Mpango huu una msimamo wa kihafidhina ikiwemo ya Wasandawe kwa kuendelea kuwajumuisha kwenye kundi la makabila yaliyo katika mazingira magumu.

Takwimu zilizotokana na uchunguzi wa kiuchumi-jamii zinaonyesha kwamba kuna kaya moja tu (1) katika mkoa wa Kagera inayojitambulisha kama wazawa wa asili wa Kibarabaig. Mradi utamfidia PAHs kwa ardhi yenye ukubwa wa ekari 0.203 na miti 148. Ardhi haijapimwa na inatumika kwa ajili ya kilimo. Huyu PAH hatahamishwa kimakazi

Kaya zilizo katika hali hatarishi

Watu na kaya zilizo katika hali hatarishi wanaweza kuguswa na shughuli za Mradi, ambazo ni pamoja na hizi zifuatazo: uhaba wa chakula na fedha kutokana na ardhi iliyochukuliwa na Mradi, hasa kwa kaya zilizokuwa na ardhi duni kabla ya kuwasili kwa Mradi; watoto na jamaa kufanya maamuzi ya makazi au kukubaliana fidia kwa niaba ya wazee walioguswa na Mradi bila idhini yao; na wanawake na watoto watakaoachwa bila makazi ambapo mkuu wa kaya hutoroka na fidia. Katika Mkoa wa Kagera Jumla ya kaya 783 (sawa na asilimia 41 ya kaya zote) zipo katika mazingira hatarishi.

Athari za Uhamaji

Jedwali ES - 5 linaonyesha kwa muhtasari athari za uhamaji wa muda mfupi na wa kudumu. Athari za muda mfupi zinatarajiwa kuwa za kipindi kifupi (kwa kawaida kipindi hiki hudumu tu kwa muda wa awamu ya kwanza ya ujenzi) na zinaweza kutatulika. Athari za kudumu zinatarajiwa kuwa za kipindi kirefu na zinaweza kudumu

[10] http://www.africa.kyoto_u.ac.jp/kiroku/asm_normal/abstracts/pdf/36-1/yatsuka.pdf

kwa kipindi chote cha Mradi. Baadhi ya athari za kudumu haziwezi kutatulika na kwa hivyo kaya zitakazoguswa na mradi na kupata athari za kudumu zitalipwa fidia kulingana na sheria za Tanzania na sheria za kimataifa za matendo mazuri (international good parctices).

Jedwali ES – 5: Muhtasari wa Athari

Athari	Vitendo vya Usimamizi
ATHARI ZA MUDA MFUPI	
Kuharibika kwa Njia za Waenda kwa Miguu na Magari	Mkandarasi atahakikisha anafahamu maeneo yote ya njia za waenda kwa miguu na nyingine zitakazoathiriwa. Mkandarasi atawajibika kuwasiliana na Jamii iliyoguswa na Mradi kwa wakati unaofaa kuhusu kufungwa kwa njia yoyote ya waenda kwa miguu na vivuko na kuwapatia watu njia mbadala, inapobidi.
Usumbufu katika Shughuli za Kilimo	Kuhakikisha kuwa mzunguko wa uzalishaji katika kilimo hauvurugiki kwa kiasi kikubwa, kwa namna iwezekanavyo Mradi utatekeleza na kusimamia yafuatayo wakati wa ujenzi: ☐ Kulipa fidia kwa kaya zilizoguswa na Mradi mapema iwezekanavyo ili waguswa wawe na muda wa kutosha wa kununua ardhi nyingine; ☐ Kaya zilizoguswa na Mradi ziruhusiwe kadri inavyowekezekana kuvuna mazao yao; ☐ Kusaidia Kaya zilizoguswa na Mradi kupata ardhi mbadala, pale inapobidi; ☐ Kusaidia Kaya zilizoguswa na Mradi kusafisha na kuandaa ardhi mbadala kwa ajili ya shughuli za kilimo, pale inapobidi; ☐ kutoa msaada wa chakula katika kipindi cha

	mpito.
Ulanguzi wa Ardhi	Kuanzisha dawati mahususi la msaada kwa kushirikiana na Ofisi ya Ardhi lenye jukumu la kushughulika na kaya zilizoguswa na Mradi zinazotaka kununua ardhi; dawati la msaada pia linaweza kujumuisha kanzidata ya watu walio tayari kuuza ardhi kwa PAH kwa viwango vya bei ya ardhi vya serikali. Kuzingatia matokeo ya utafiti wa EACOP juu ya mchanganuo wa Hali ya Uhamaji utakosababishwa na Mradi Julai 2019.
Athari za Kijamii katika PAC	☐ Rejea hatua za kupunguza madhara zilivyobainishwa katika ripoti ya Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (ESIA) na Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu za Mradi
Kukosekana kwa Upatikanaji wa Maliasili	☐ Ikiwa ujenzi wa sehemu ya bomba utachukua muda mrefu zaidi ya mwezi katika hifadhi ya misitu, mradi utaruhusu wanajamii kuvuna rasilimali asili kwa masaa machache kwa wiki (kwa kutumia vibali/vizuizi vya kisheria). ☐ Hakikisha kuwa watu wanaendelea kupata huduma ya sehemu ya msitu ambayo haijaathiriwa kwa kuanzisha njia za waenda kwa miguu mbali na eneo la ujenzi. ☐ Kutumia hatua za kupunguza athari zilizobainishwa katika ripoti ya ESIA kuhusu madhara yatakayohusiana na mazingira. ☐ Kuhakikisha kuwa wakandarasi wote wanafuata masharti yaliyowekwa katika Mipango ya Usimamizi wa Wakandarasi wa Mradi wa EACOP
Athari za Kudumu	
Kupoteza ardhi	Kufidiwa
Kupoteza Majengo (makazi na yasiyo ya makazi)	Kufidiwa

Kupoteza Mazao na Miti ya Kibiashara na mingine	Kufidiwa
Usumbufu wa Makaburi	Kuhamishwa

6. MFUMO WA STAHIKI, HAKI NA FIDIA

Sura ya 6 Inaelezea Mfumo wa Stahiki, Haki na Fidia. Sura hii inaelezea vigezo vya stahiki kwa Watu Walioguswa na Mradi namna ya kupata fidia na msaada wa wakati wa zoezi la uhamishaji watu na makazi, kubainisha stahiki zilizopendekezwa kwa kila aina ya athari ya uhamaji inayosababishwa na utekelezaji wa Mradi, na kuonyesha viwango na thamani ya fidia inayotumika.

Sura hii inajadili mambo yafuatayo:

- ☐ **Stahiki:** Inatambua na kueleza “nani” anayestahiki kupata fidia na msaada wa Uhamishaji watu na makazi;
- ☐ **Haki:** Kipengele hiki kinafafanua “fidia gani na msaada gani” ambao kila mtu aliyeguswa na Mradi anastahili kupata, na msaada wa urejeshaji wa ustawi wa maisha na stahiki za watu walio katika mazingira magumu, vyote viwili vikiwa ni matakwa ya Viwango vya Fedha vya Kimataifa IFC. Kipengele hiki kinaeleza kwa kina mfumo wa haki na:
- ☐ **Uthamini na Fidia:** Sehemu hii inafafanua “namna” ambavyo mali mbalimbali zilizoguswa zimethaminishwa pamoja kubainisha viwango na aina ya fidia watakayopata watu walioguswa na Mradi.

Stahiki

Vigezo vya stahiki viliamuliwa mwanzoni mwa Mradi, kama ilivyoainishwa katika Sera ya Mfumo wa Uhamishaji Watu na Makazi (RPF). Vigezo hivyo vimetolewa kwa kuzingatia mahitaji ya PS5 IFC na sheria za Nchi. Kategoria za stahiki zinazohusiana na Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera zimebainishwa na kufupishwa katika makundi kama ilivyo hapo chini (Sura ya 6 ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera inatoaa maelezo haya kwa undani zaidi):

- ☐ Watu ambao wanamiliki ardhi kisheria au umiliki wa kimila,
- ☐ Mguswa ambaye anamiliki majengo na miundombinu iliyoguswa na Mradi kama makazi, majengo mengine ya nyumbani kama vile vyoo, jiko na majengo ya kilimo;
- ☐ Mali iliyoguswa na njia ya bomba ikiwa ni pamoja na vipande vya ardhi vinavyosimamiwa na Halmashauri za Vijiji;
- ☐ Taasisi ambazo zinamiliki ardhi na/au majengo na/au miundombinu ya umma pamoja na Mashirika ya Kidini na Mamlaka za Serikali;

- ☐ Wamiliki wa mazao ya kudumu, ya mwaka na ya msimu (yanayopandwa na kuvunwa kila msimu);
- ☐ Wamiliki wa miti ya biashara iliyo katika maeneo yaliyoguswa na mradi, iwe kwenye ardhi yao au kwenye ardhi ya wengine;
- ☐ Wamiliki au wasimamizi wa mali za urithi wa kiutamaduni kama vile makaburi;
- ☐ Wapangaji ardhi – watu ambao, japokuwa hawamiliki ardhi, wanamakubaliano na wamiliki wa ardhi kutumia ardhi hiyo;
- ☐ Watumiaji wa ardhi wasio rasmi - kwa mfano, watu wanaojipatia kuni, dawa za asili, wawindaji na wale wanaovuna maliasili zingine;
- ☐ Biashara zisizo rasmi na wachuuzi kama vile maduka, maduka ya nyama, pembejeo za kilimo (kama vile majengo ya mashine za kusagia nafaka), migahawa, wasusi, mafundi cherehani/ washonaji nguo, watengenezaji wa samani, vioski n.k;
- ☐ Wafugaji wanaotumia ardhi kwa ajili ya kulishia mifugo; na
- ☐ Watu waishio katika mazingira magumu yaani watu ambao upoteaji wa mali na rasilimali na/au kuvurugika kwa mifumo ya upatikanaji wa mali au raslimali, unaweza kusababisha mvurugiko mkubwa katika ustawi wa maisha na athari zaidi kutokana na mazingira yao magumu na/au utegemezi shughuli zao katika ustawi wa maisha.

Tarehe ya Katazo

Tarehe ya Katazo hutegemea na kuanza kwa uchunguzi wa uthamini wa mali. Watu wanaokaa au kuhamia eneo la Mradi baada ya tarehe ya katazo hawastahiki fidia na/au usaidizi wa Uhamishaji Watu na Makazi. Tarehe ya Katazo imepangwa kwa kila kijiji kilichoguswa na mkuza wa njia ya bomba. Taarifa ya tarehe hizi zilitolewa kwa waguswa wa Mradi katika kila kijiji na zimewasilishwa katika sura ya 4.

Uhalali wa Uthamini

Kwa mujibu wa kifungu cha 52 (3) cha Sheria ya Bunge ya Usajili wa Uthamini na Wathamini, Ripoti za uthamini lazima ziidhinishwe na Mthamini Mkuu wa Serikali (CV) ndani ya miezi sita tangu tarehe ya uthamini kwa kuzingatia maslahi ya mguswa wa mwisho. Ripoti za uthamini zitakuwa halali kwa kipindi cha miaka miwili tangu tarehe ya kuidhinishwa na Mthamini Mkuu. Tarehe ya uthamini kwa kuzingatia maslahi ya mguswa wa mwisho kwa wilaya ya:

- ☐ Missenyi ni tarehe 24 Octoba 2019;
- ☐ Bukoba 24 Octoba 2019;

- ☐ Muleba 25 Septemba 2019; na
- ☐ Biharamulo tarehe 3 Septemba 2019.

Haki

Matokeo ya uchunguzi wa Kiuchumi-jamii na uthamini wa mali pamoja na vigezo vya stahiki vimetumika kutayarisha mfumo wa haki. Mfumo huo unafafanua kanuni na mbinu za fidia kwa kushirikisha stahiki za fidia kwa kutegemea aina na kiwango cha mtu aliyeguswa. Fursa za uchaguzi wa aina ya fidia au msaada stahiki zimewasilishwa kupitia vikao vya wadau.

Sura ya sita inaeleza mfumo wa stahiki katika mkoa wa Kagera (Njia ya Bomba na Miundombinu ya juu). Jedwali lifuatalo linaonyesha kwa muhtasari muundo na maudhui ya jumla ya mfumo wa stahiki katika mkoa wa Kagera;

Jedwali ES - 6 : Maudhui ya Jumla ya Mfumo wa Haki katika Mkoa wa Kagera

Athari	Madhara	Haki ya Mguswa	Haki[11]	
			Fedha na/au Vitu mbadala	Ureshaji wa Ustawi wa Maisha
Ardhi				
Kategoria saba za upotezaji wa Ardhi zimezingatiwa (Makazi na Kilimo).	Upotevu wa Kudumu	Wamiliki wa Kisheria na Kimila, wamiliki wa kitaasisi na watumiaji wengine wanaotambulika.	Hatua mchanganyiko wa fidia za vitu mbadala na fedha. Mchanganyiko huu hutofautina kutegemea ukubwa wa athari	Machaguo mchanganyiko katika urejeshaji wa ustawi wa maisha (pamoja na mipango ya mguswa mmoja mmoja au makundi). Mchanganyiko huu hutofautina kutegemea

[11] Stahiki zimefafanuliwa kwa kina. Kwa sababu za kisheria na za kiutendaji, ushauri wa kina wa jumla kamili ya stahikiki unapaswa kutafutwa.

Athari	Madhara	Haki ya Mguswa	Haki[11]	
			Fedha na/au Vitu mbadala	Ureshaji wa Ustawi wa Maisha
				ukubwa wa athari
Upotevu wa Makazi kwa Mmliki				
Unabainishwa kama upoteaji wa makazi na miundombinu mingine (kama makazi, choo, jiko n.k).	Upotevu wa kudumu (vyote au baadhi).	wamiliki (miundombinu na majengo, makazi na isiyo makazi), na vyombo vya serikali.	Mchanganyiko wa fidia ya vitu mbadala na fedha.	Mchanganyiko wa namna ya urejeshaji wa ustawi wa maisha (Ikiwemo makundi na watu binafsi) Haiko wazi kwa aina zote
Upotevu wa Raslimali Fedha au Vitu Vinavyoongeza Kipato				
Upotevu wa raslimali zinazopatikana katika jamii kama vile misitu, ardhi oevu na miti isiyo ya biashara.	Upotevu wa kudumu na wa muda mfupi. (Kwa baadhi ya maliasili za jamii).	Watumiaji wa Raslimali au watu wanaopoteza mnyororo wa mapato.	Hatua mchanganyiko za kumiliki na msaada. Hatua za kifedha za Upotevu wa ardhi na mali ya jumuiya	-
Upotevu wa Miundombinu Inayomilikiwa Kitaasisi au Kijumuiya				
Kategoria tano za upotevu (ikiwa ni pamoja na ardhi ya machungio, barabara, njia mifereji na Gridi za umeme)	Upotevu wa kudumu na wa muda mfupi.	Wanakijiji wamiliki, taasisi (kama vile mashirika ya kidini), wilaya na serikali za mitaa, makampuni ya huduma.	Mchanganyiko wa fedha, msaada na kupata mbadala. Muunganiko unatofautiana kulingana na kategoria	-
Miti na Mazao				
Kategoria saba za upotevu (ikiwa ni pamoja na	Upotevu wa kudumu, au upotevu/kuzuiliwa kwa	Ardhi na mazao/ wamiliki wa miti, watumiaji wa miti, Wakulima	Hatua mchanganyiko za fidia ya fedha, posho	Hatua mchanganyiko za urejeshaji wa

Athari	Madhara	Haki ya Mguswa	Haki[11]	
			Fedha na/au Vitu mbadala	Ureshaji wa Ustawi wa Maisha
upotevu wa mazao, miti na mali za kilimo)	upatikanaji.	wapangaji ardhi, wanakijiji wamiliki na wamiliki wasio rasmi.	na msaada. Muunganiko unatofautiana kulingana na kategoria	ustawi wa maisha, kwa watu walioguswa na Mradi kwa kuhamishwa kwa vitu na kuyumbishwa kichumi.
Mali za Kitamaduni				
Makaburi	Upotevu wa kudumu.	Mguswa binafsi au vikundi wanaowasilisha malalamiko kuhusu makaburi.	Uondoaji rasmi na mchakato wa uhamishaji makaburi. Fidia ya fedha kulingana na matakwa ya kisheria	Hakuna.

Uthamini na Fidia

Mradi unalazimika kukidhi mahitaji ya sheria ya Tanzania ya utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi kama ilivyo katika viwango vya IFC PS5 kwenye utwaaji na Uhamishaji Watu na Makazi usio wa hiari. Ili kutimiza mahitaji haya, mchakato wa uthamini umekamilika kwa vipengele vitatu (kama ilivyofupishwa hapo chini):

- ☐ **Viwango vya Ripoti:** Chini ya Vifungu vya Kanuni ya Uthamini na Wathamini (jumla) ya Mwaka 2018, Mthamini aliyesajiliwa kwa ajili ya Mradi alifanya utafiti wa bei ya soko katika mkoa wa Kagera. Utafiti ulilenga kuainisha thamani ya masoko inayowiana na gharama za malipo mbadala zilizopo katika soko kwa vitu vinavyofidiwa.
- ☐ **Ripoti ya Uthamini na Jedwali la Fidia chini ya Sheria za Tanzania**. Ripoti hii ya uthamini (pamoja na jedwali la Fidia) inahusisha vitu vinavyofidiwa vilivyoorodheshwa chini ya mfumo wa sheria ya nchi. Ripoti imewasilishwa kama fidia ya fedha taslimu; na itapelekwa kwa Mthamini Mkuu kwa ajili ya

kuidhinishwa. Vipengele vyote vya mchakato huu wa uthamini vimeelezewa kwa kina katika sura ya 6 ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera. Utiaji saini na uidhinishwaji wa Ripoti za Uthamini na majedwali ya fidia utazingatia Sheria ya Tanzania ya Uthamini na Usajili wa Wathamini (jumla) ya mwaka 2018.

- **Uthamini wa Fidia kwa Stahiki za Ziada chini ya IFC.** Ripoti ya Tathmini na jedwali la Fidia linashughulikia stahiki za ziada chini ya IFC ili kukidhi gharama zote za vitu mbadala na stahiki ya fidia ya vitu kama vile ardhi mbadala, nyumba mbadala, urejeshaji wa ustawi wa maisha na msaada kwa watu walio katika mazingira magumu. Sheria hizi zinahitajika ili kuhakikisha kuwa fidia ya Mradi inakidhi mahitaji na majukumu ya IFC vya ziada. Wakati mambo haya yote yanapozingatiwa na mthamini mkuu, haikusudiwi kwamba yote yataidhinishwa na mthamini mkuu kwa kuwa yanajumuisha stahiki mahususi za ziada za Mradi na maamuzi ya aina ya fidia, kulingana na matakwa ya viwango vya fedha vya Washirika (IFC).

- Stahiki za watu walioguswa na Mradi katika mkoa wote wa Kagera zimeorodheshwa na kuwekwa katika majedwali. Maelezo ya kina yameonyeshwa katika sura ya sita.

7. MBADALA WA MAKAZI NA ARDHI

Sura ya 7 ya Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi katika mkoa wa Kagera inaonyesha mkakati wa nyumba na ardhi mbadala ambao utatumika kwa Watu na Kaya zilizoguswa na Mradi ambazo zinazostahili. Hatua zinazoongoza mkakati huu zimefafanuliwa (pamoja na dhana ya uchunguzi sanifu) na utaratibu utakaotumika kwa usanifu wa nyumba mbadala na ardhi mbadala zimeelezwa kwa kina.

Miundo Mbinu Iliyopo.

Uchunguzi[12] sanifu ulifanyika ili kusaidia kutambua aina za nyumba zilizopo sasa iliziweze kutumika kama msingi wa usanifu kwa ajili ya nyumba mbadala. Uchunguzi ulihusisha mapitio ya ripoti za awali, taarifa za usuli na takwimu za kiuchumi-jamii kabla ya eneo lengwa kufikiwa na timu ya wasanifu inayojumuisha wasanifu na wathamini majengo. Matokeo ya uchunguzi na taarifa za usuli wa utafiti zimetumika kwa ajili ya usanifu hasa kubaini sura na ukubwa wa jengo kulingana na vifaa vinavyopatikana katika eneo husika. Miundo mbinu mingi iliyoguswa katika Mkoa wa Kagera ni nyumba za jadi zilizojengwa kwa vifaa vinavyopatikana katika jamii husika.

Katika Mkoa wa Kagera, kaya 107 zinazomiliki miundo mbinu ya makazi 116 zitahamishwa makazi. Kati ya miundo mbinu 116; 113 imebainika kuwa inastahili malipo ya fidia ya nyumba mbadala. Hii ni kwa sababu kuna kesi tatu (3) ambapo kaya husika zinamiliki miundombinu miwili (2) inayojumuisha eneo la ukubwa usiozidi mita za mraba 25 ($25m^2$). Katika kesi hizi, waguswa wa mradi wanastahili tu fidia ya nyumba mbadala moja ($25m^2$) na watalipwa fidia ya fedha kwa ajili miundombinu mingine midogo zaidi.

Sehemu ya eneo la nyumba iliyopo sasa itaonyesha sifa stahiki zitakazotumika kusanifu nyumba mbadala. Idadi ya mwisho ya miundo mbinu mbadala itakayojengwa itategemea idadi ya waguswa wa mradi ambao watachagua nyumba mbadala badala ya fidia ya fedha taslimu.

Idadi kubwa ya majengo yaliyoathirika mkoani Kagera ni nyumba za kitamaduni zilizojengwa kwa kutumia vifaa vya asili vipatikanavyo kwa urahisi.

[12] Dhana ya Ripoti ya Usanifu wa Makazi Mbadala: Mkuza (2019) (Digby Wells Consortium).

Misingi ya Usanifu

Usanifu majengo wa ndani ulitumika kusanifu makazi mbadala ya watu katika mkoa wa Kagera. Mikakati ya usanifu ilizingatia ufanano wa nafasi ya sakafu/hatua za miguu; shughuli na mpangilio wa eneo; uimara na urahisi wa ujenzi; nafasi ya sakafu inayotoshea utulivu; afya; usalama; mahitaji ya kijamii na kitamaduni.

Usanifu wa Nyumba mbadala na Miundombinu Saidizi

Aina nane za usanifu wa nyumba mbadala umetekelezwa na Mradi. Nyumba hizo zina ukubwa kati ya mita za mraba 25 (25m^2) (kategoria A) na mita za mraba 145 (145m^2) (kategoria H). Miundo mbinu mingi (asilimia 54) inayostahili mbadala wa nyumba katika mkoa wa Kagera ni chini ya mita za mraba 25 (25m^2) na zipo katika kategoria A ya nyumba.

Jedwali ES - 7: Aina za Nyumba na Makazi Stahiki katika Mkoa wa Kagera

Nyumba	Makazi Stahiki Mkoa wa Kagera	Eneo la Sakafu	Aina ndogondogo	Idadi ya Vyumba
Nyumba kategoria A	61	25m^2	A1	2
			A2	3
			A3	3
Nyumba kategoria B	27	33m^2	B1	3
			B2	4
Nyumba kategoria C	11	39m^2	C1	3
			C2	4
Nyumba kategoria D	6	47m^2	D1	4
			D2	5
Nyumba kategoria E	3	58m^2	E	5
Nyumba kategoria F	3	75 m^2	F	5
Nyumba kategoria G	1	105 m^2	G	6
Nyumba kategoria H	1	145 m^2	H	8

Maelezo zaidi yametolewa katika Sura ya 7 na Kiambatisho D ambacho kinajumuisha usanifu wa nyumba zote za Mradi (kategoria A hadi H).

Miundombinu Saidizi

Katika kuboresha hali ya maisha kwa kila nyumba mbadala, Waguswa wa Mradi watajengewa jiko na choo kimoja cha kisasa cha shimo. Pale ambapo waguswa wa mradi wanastahili zaidi ya nyumba mbadala moja (1), wanaweza kuchagua:

- ☐ Choo cha kisasa (chenye ukuta wa faragha mahali pa kuingilia) na jiko moja kwa kila nyumba mbadala; au
- ☐ Choo kimoja cha kisasa pamoja na bafu, jiko na stoo kwa kila nyumba.

Usanifu wa miundombinu saidizi umeonyeshwa katika Sura ya 7 na kiambatisho D.

Ardhi Mbadala

Waguswa wa Mradi ambao wanastahili ardhi mbadala watapewa nafasi ya kuchagua kati ya Ardhi au fedha taslimu (au vyote kwa pamoja). Kanuni hiyo hiyo itatumika pia katika suala la uhamishwaji makazi. Waguswa wa Mradi wanaostahili watapewa fursa ya kuchagua kati ya fidia ya fedha taslimu na ardhi/makazi mbadala wakati wa muhtasari wa utekelezaji wa Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP). Mahitaji ya awali ya ardhi mbadala yatazingatia matarajio ya Mradi kwamba Waguswa wa Mradi wanaostahili ardhi mbadala na/au makazi watachagua kulipwa fidia ya vitu kuliko fedha taslimu.

Mbadala wa Ardhi kwa Ardhi itakayochukuliwa na mradi

IFC PS5 vinabainisha kwamba pale maisha ya watu yanategemea ardhi, inafaa kwamba ardhi mbadala angalau iwe ni sawa na ardhi iliyopotea kwa maana ya uwezo wa uzalishaji na mahali ardhi ilipo. Katika Mkoa wa Kagera, sehemu ya ardhi isiyofaa kwa kilimo ni ndogo sana (kati ya asilimia 6 hadi 28 kwenye wilaya nne). Hivyo, kwa kuzingatia hayo, ni vyema kuhakikisha kwamba mkakati sahihi wa mbadala wa "ardhi kwa ardhi" unatumika.

Rasimu ya Kitabu cha Matendo Mazuri cha IFC[13] inapendekeza kwamba mbadala wa "ardhi kwa ardhi" unaweza kufanyika pale ambapo kaya zinatafuta ardhi mbadala zenyewe (kwa kusaidiwa na Mradi na/au mamlaka za eneo husika), au pale ambapo Mradi unapata ardhi kwa ajili ya mgao. Baadhi ya waguswa wa mradi wanaweza kuwa na ardhi katika eneo moja, na wangependelea ujenzi wa nyumba zao ufanyike hapo. Hata hivyo, uchunguzi wa kuona ufaafu wa eneo hilo utafanyika.

Utekelezaji wa Nyumba na Ardhi Mbadala

Uamuzi sahihi zaidi wa ardhi na nyumba mbadala zinazohitajika utafanywa mara tu waguswa wa mradi watakapofanya uamuzi wa aina gani ya fidia wangependelea kufidiwa na kisha kutia saini makubaliano ya fidia. Mradi utahakikisha kuwa waguswa wa mradi waliohamishwa wamehamia moja kwa moja kwenye sehemu zao za ardhi mbadala, bila kuruhusu hitaji la malazi ya muda. Pale ambapo changamoto za utekelezaji zitajitokeza, Mradi utashirikiana na waguswa wa mradi pamoja na mamlaka husika kutoa msaada katika kipindi hiki cha mpito.

Lengo la Mradi ni kutoa ardhi mbadala katika kijiji au kata hiyohiyo kwenye maeneo ya awali mahali ilipokuwa ardhi inayomilikiwa na waguswa wa mradi. Viwanja mbadala mara nyingi vitakuwa ni ardhi ya kijiji iliyo chini ya mamlaka ya kijiji hicho. Mradi utasaidia mchakato wa kupata hati kwa waguswa wa mradi ili kujihakikishia usalama wa umiliki wa ardhi hiyo.

[13] IFC Draft of the Good Practice Handbook: Land Acquisition and Resettlement (2019).

8. MPANGO WA UREJESHAJI WA USTAWI WA MAISHA

Sura ya 8 ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera inaeleza mbinu za Mradi katika urejeshaji wa ustawi wa maisha. Shughuli hizi zinafanyika katika muktadha wa Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP). Mpango huu unazingatia stahiki wa urejeshaji wa ustawi wa maisha, muktadha wa mikakati ya mkoa ya ustawi wa maisha, programu zilizopo zinazohusiana na ustawi wa maisha, stahiki wa msaada wa ustawi wa maisha na fursa zitakazotolewa.

Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha unalenga urejeshaji na uboreshaji wa ustawi wa maisha ya kaya zilizoguswa na Mradi. Mpango huu utatumika pale ambapo fidia pekee haitahakikisha uwezekano wa urejeshaji wa ustawi wa maisha ya kaya zitakazohamishwa.

Lengo kuu la Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP) ni kuhakikisha kuwa jamii inapata mabadiliko makubwa katika maisha na ustawi wa maisha ya kaya stahiki zilizoguswa na Mradi. Lengo hili linajumuisha:

- ☐ Utoaji wa mambo yote endelevu ya ustawi wa maisha ambayo yanamwezesha mguswa na kaya zilizoguswa na Mradi kuondokana na utegemezi;
- ☐ Utoaji wa mbinu za kukuza fursa zaidi kwa wale wanaopokea fidia ya fedha;
- ☐ Kutumia ujuzi na maslahi yaliyopo wakati huohuo katika kipindi cha kuweka mazingira kwa ajili ya maendeleo na uwezeshaji wa ujuzi mpya; na
- ☐ Ukuzaji na uwezeshaji wa kujitegemea kiuchumi-jamii.

Kanuni zinazohimiza Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP) zinaenda sambamba na mahitaji pamoja na mbinu zilizowekwa kwenye sheria za nchi zinazotumika pamoja na viwango vya IFI. Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha unajumuisha fursa za jumla ambazo zitatolewa kwa watu na kaya zilizoguswa na mradi. Viwango vya msaada vitazingatia viwango vya madhara katika kaya na mazingira yao magumu. Kaya zilizotambuliwa kuwa zinaishi katika mazingira magumu Sana zitashirikishwa, na kupewa msaada muhimu wa ziada.

Awamu za Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha

LRP utafanyika katika awamu mbili:

- ☐ Awamu ya Kwanza - urejeshaji wa Ustawi wa Maisha na msaada wa haraka. Lengo likiwa ni urejeshaji haraka wa ustawi wa maisha yaliyoguswa moja kwa moja, na uboreshaji wa usalama wa chakula.
- ☐ Awamu ya Pili – Uboreshaji wa ustawi wa maisha wa ziada. Mipango mingine muhimu ya ziada inayolenga kuboresha ustawi wa maisha.

Muktadha na Mikakati ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha katika Mkoa wa Kagera

Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP) unatambua na kuzingatia muktadha ambao jitihada za urejeshaji hupangwa na kutekelezwa. Masuala ya muhimu ya kimuktadha ni haya yafuatayo:

- ☐ Tabia nchi
- ☐ Sifa za kitamaduni
- ☐ Desturi za ustawi wa maisha
- ☐ Upatikanaji na utumiaji wa masoko
- ☐ Tabia nchi, na hali ya mavuno isiyotabirika

Tathmini ya Athari za Ustawi wa Maisha

Athari za ustawi wa maisha zimetathiminiwa katika muktadha endelevu wa Mfumo wa Ustawi wa Maisha wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID). Kwa kutumia Mfumo wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), athari kuu za ustawi wa maisha ambazo zimebainishwa katika Mkoa wa Kagera ni:

- ☐ Za kiasili – upoteaji wa ardhi, miti na mazao;
- ☐ Kimaumbile – upoteaji wa makazi, na rasilimali za kijiji;

- ☐ Kijamii – Athari ya maliasili za kitamaduni na miundombinu ya kitaasisi;
- ☐ Kibinadamu – Athari za watu na makundi yaliyo katika mazingira magumu; na
- ☐ Kifedha – Athari za fedha kwa mguswa binafsi na kaya.

Mpango wa uboreshaji wa Maisha unaeleza kwa muhtasari aina mbalimbali za taratibu za uhamaji na athari zake katika mipango ya ustawi wa maisha ya Watu na kaya zilizoguswa na Mradi katika Mkoa wa Kagera.

Stahiki ya Msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha

Mradi utatoa usaidizi wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kulingana na ukubwa wa athari za ustawi wa jamii kwa Watu na kaya zilizoguswa na Mradi, na uhimilivu wao pamoja na uwezo wa kuboresha ustawi wa maisha. Kutokana na mapitio ya athari yaliyofanyika kuhusu mikakati ya ustawi wa maisha, vigezo vya kuamua aina ya msaada wa ustawi wa maisha vimepangwa.

Uboreshaji wa ustawi wa maisha umeandaliwa kimakundi kwa kuzingatia ukubwa wa athari kwa Watu walioguswa na Mradi. Aidha, baadhi ya Watu walioguswa na Mradi wanahitaji kupata msaada wa kuboresha ustawi wa maisha katika ngazi ya mguswa mmoja mmoja. Kwa mfano, kuhamishwa kwa Watu walioguswa na Mradi na wenye mazingira magumu, kwa kuwa hawawezi kurejesha ustawi wao wa maisha kulingana na kiwango cha athari cha Mradi na/au ukosefu wa uhimilivu au hali yao katika jamii. Hatua zote za urejeshaji wa ustawi wa maisha zinazozingatia msingi wa ardhi zimejumuishwa katika Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP).

Mipango ya Sasa ya Uboreshaji wa Ustawi wa Maisha

Mradi utahamasisha na kuwekeza kwenye mpango wa uboreshaji wa ustawi wa maisha unaotekelezwa katika eneo husika kadri inavyowezekana. Ustawi wa maisha na jitihada zake zilizobainishwa katika Mkoa wa Kagera ni:

- ☐ Programu katika Mikoa Iliyoguswa na Mradi Itaongozwa na Asasi Zisizo za Kiserikali na Asasi Zinazoendesha Shughuli zake bila Faida. Hii ni pamoja na uhamasishaji wa ulinzi wa mazingira na endelevu, ushauri wa kilimo na ujasiriamali, msaada wa ushauri kwenye kilimo, maliasili na usambazaji wa mbegu bora.
- ☐ Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Tanzania. Mkakati huu kabambe unalenga kuchangia katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025,

ambao unakusudia kuinua viwango vya maisha kwa nchi za kipato cha kati ifikapo mwaka 2025; na

- ☐ Miradi ya maendeleo inayofanywa na Serikali ya Tanzania (GoT), au Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine. Kwa mfano ushirikiano kati ya Halmashauri za wilaya na taasisi za muunganiko wa mataifa (UN) zinazohusika na chakula na kilimo ili kukomaza mfumo wa kilimo, kutoa mikopo ya muda mfupi kusaidia shughuli za kilimo, kutangaza na kutoa mifuko ya kutunzia nafaka na maendeleo ya viwanda vya ndani.

Mpango wa Urejeshwaji wa Ustawi wa Maisha

Chaguo za Urejeshwaji wa Ustawi wa Maisha zilizopo katika Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP) katika mkoa wa Kagera ni:

- ☐ LRA 1 – Utayarishaji wa ardhi mbadala na upandaji wa mazao ya kilimo;
- ☐ LRA 2 - Mpango wa uboreshaji mahindi na mchele;
- ☐ LRA 3 – Mpango wa mazao mseto;
- ☐ LRA 4 – Mpango bora wa ufugaji wa kuku;
- ☐ LRA 5 – Mpango bora wa ufugaji wa mifugo;
- ☐ LRA 6 – Mipango bora wa ufugaji nyuki;
- ☐ LRA 7 – Maendeleo ya biashara; na
- ☐ LRA 8 – Kupanga bajeti ya kaya na mafunzo ya utumiaji wa pesa.

LRA 2 na LRA 3 zinahusiana na mkoa wa Kagera, LRA2 inatumika kuimarisha na kusaidia mbinu za ustawi wa maisha, na LRA3 inatumika katika kuboresha kilimo kwa kuhimili ukame na mabadiliko ya tabia nchi. LRA 1 ni muhimu ambapo ardhi imebadilishwa, LRA 7 na LRA 8 ni muhimu katika kujenga uwezo na kujitegemea.

Wabia katika Utekelezaji

Mradi unaweza kusimamia utekelezaji wa mipango ya urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kusaidiana na wadau mbalimbali kama vile Azaki (taasisi zisizo za kiserikali na taasisi za kijamii), watoaji wa huduma, na makundi ya kijamii, idara za serikali na halmashauri za mitaa. Baadhi ya washirika muhimu wamebainishwa, ikiwa ni pamoja na Azaki za ndani na nje (za nje zinazofanya kazi Tanzania).

Msaada wa Mpito na wa Muda Mfupi

Msaada wa mpito utatolewa kwa Watu na kaya zilizoguswa na Mradi kwa kuhamishwa makazi na kuyumbishwa kiuchumi ili kukamilisha malipo ya fidia na kuhakikisha kuwa kaya zinaweza kukidhi mahitaji yao ya msingi na kudumisha hali yao ya maisha mara tu baada ya kupoteza ardhi na hadi watakapopata nafasi ya kurejesha ustawi wa maisha yao katika ngazi za awali za Mradi. Vipengele hivi vya msaada vya awali ni pamoja na:

- ☐ Msaada wa mpito wa chakula (au mfumo wa vocha) na masharti mengine ili kuhakikisha kaya zinapata chakula wakati wa kipindi cha mpito;
- ☐ Mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa ajili ya kaya zote zinazopokea fidia ya fedha ili kuwapatia wana kaya mbinu za kutumia vizuri fedha walizopokea; na
- ☐ Kaya zinazoishi katika mazingira magumu na zilizoguswa na Mradi zitafuatiliwa kwa ukaribu ili kuhakikisha kama msaada uliotolewa unatosha na kuzingatia marekebisho yoyote pale inapobidi. Kaya zitapimwa ili kubaini kama zinastahili kuendelea kubakia kwenye Mpango wa Msaada wa Mpito. Tathimini itafanyika kwa muda wa miezi sita (6) hadi miezi kumi na mbili (12) kama itahitajika.

9. MPANGO WA WAWAGUSWA WALIO KATIKA HALI HATARISHAI

Sura ya 9 inafafanua Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha (LRP) waguswa wenye hali hatarishi ambao unawapa kipaumbele waguswa wasiojiweza au walio katika hali hatarishi katika mkutadha wa mchakato wa uhamishaji watu na makazi katika mkoa wa Kagera. Mpango huu unaeleza hali hatarishi na kategoria za hali hatarishi, Unaonesha idadi ya kaya kwa kila kategoria, kudokeza kwa muhtasari mikakati inayoweza kutumika katika kuboresha ustawi wa maisha kwa watu walio katika hali hatarishi na kueleza njia ya ushirikishaji wa makundi yaliyo katika hali hatarishi.

Mpango kwa waguswa walio kwenye hali hatarishi unalenga kuthibitisha uhatarishi wa Waguswa wa Mradi (PAPs) wanaoweza kuwa katika hali hatarishi kama inavyobainishwa wakati wa mchakato wa uchunguzi, na kushughulikia hali hatarishi iliyotambuliwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa watu walioguswa na Mradi wanapata taarifa kuhusu shughuli za Mradi na kusaidiwa kwa usahihi kushughulikia hali hatarishi yoyote zaidi inayotokana na shughuli za Mradi.

Malengo ya Mpango wa watu waliokatika hali hatarishi ni:

- ☐ Kuhakikisha kuwa waguswa na kaya zinazoweza kuwa katika hali hatarishi zaidi zinatambuliwa na kufuatiliwa wakati na baada ya mchakato wa uhamishaji watu na makazi;
- ☐ Kutoa msaada stahiki wa kuboresha ustawi wa maisha kwa kaya zinazotambulika kuwa ziko katika hali hatarishi;
- ☐ Kubaini fidia na mahitaji ya urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa watu walio katika hali hatarishi ikiwa ni pamoja na aina mbalimbali ya misaada;
- ☐ Kuwasaidia watu waliotambuliwa kuwa katika hali hatarishi ili waweze kuelewa na kuamua aina za fidia za uhamishaji watu na makazi;
- ☐ Kuzingatia kwa makini mitandao ya kijamii inayohusiana na muundo wa familia na jamii (kabila) na jinsi inavyoweza kuundwa upya wakati wa uhamishaji wa watu na makazi; na
- ☐ Kubaini hatua zaidi za kusaidia watu walio katika hali hatarishi kuweza kukabiliana na athari zilizosababishwa na Mradi wakati wa kuhama makazi.

Maana na Aina za Hali Hatarishi

Dhana ya hali hatarishi ni changamani na yenye sura nyingi. Ili kueleza kwa ufasaha masuala yote kwa pamoja ya hali hatarishi, Mradi umeandaa vigezo vitakavyotumika kubaini watu au kaya zilizo katika hali hatarishi kwa kuzingatia sababu ambazo zinaweza kupunguza ustahimilivu wa kaya kupata ardhi na mistuko na athari zinazosababishwa na Uhamishaji watu na makazi.

Vigezo hivyo ni kama vile umri wa mkuu wa kaya na jinsia, kiwango cha elimu ya mkuu wa kaya, Uwepo wa walememavu wa akili na maumbile katika kaya, wategemezi na kiasi cha rasilimali za msaada zilizopo, na watoto wasiosoma shule. Kwa kuzingatia muunganiko wa aina mbalimbali za hali hatarishi katika kaya, aina tatu za hali hatarishi zimepitishwa katika mpango wa Uhamishaji watu na makazi katika mkoa wa Kagera:

- **Aina ya 1: (Hali Hatarishi),** Kaya zitawekwa kwenye orodha ya walio katika hali hatarishi mara tu zitakapobainishwa na kukidhi vigezo vya kupewa msaada wa vitu na kwa ajili ya ustawi wa maisha kwa mguswa mmojammoja.
- **Aina ya 2** (**Uwezekano wa Hali Hatarishi),** kaya zitastahili msaada wa vitu na msaada wa kuboresha ustawi wa maisha lakini zitahitaji uthibitisho zaidi kabla ya kuwekwa kwenye orodha ya walio katika hali hatarishi.
- **Aina ya 3 (katika Hatari)**, kaya hizi zitawekwa kwenye orodha ya uangalizi na lazima ziingizwe kwenye kila tathimini au uchunguzi ili kufuatilia watu walioathitika na Mradi.

Muhtasari wa Kaya Zilizoguswa na Mradi kwa kila kata umewekwa katika jedwali ES-8, ikumbukwe kuwa, sura ya 9 ya Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika Mkoa wa Kagera unatoa taarifa kwa kina za kata na vijiji.

Jedwali ES- 8 : Muhtasari wa Kaya Kulingana na Kategoria ya Hali Hatarishi kwa Kata

Kata	Aina ya 1	Aina ya 2	Aina ya 3
Missenyi			
Mutukula	4	10	18
Nsunga	6	12	5
Kassambya	31	32	31
Kyaka	8	16	11

Kata	Aina ya 1	Aina ya 2	Aina ya 3
Kilimilile	10	17	15
Bukoba			
Kyamulaile	3	6	6
Mugajwale	29	47	51
Kyaitoke	16	22	24
Izimbya	-	-	-
Kibirizi	9	11	12
Rukoma	2	4	4
Muleba			
Ngenge	59	116	90
Burungura	27	49	17
Mubunda	8	20	13
Bisheke	6	13	6
Kasharunga	31	30	45
Karambi	49	60	28
Kyebitembe	-	5	4
Biharamulo			
Nyamigogo	9	6	9

Asili na kiwango cha hali hatarishi kitatofautiana kutoka kaya moja hadi nyingine, na misaada itatolewa kulingana na tatizo lilivyo.

Hali Hatarishi Mahususi

Kama sehemu ya Mpango wa watu walio katika hali hatarishi mahususi **(**VPP), ya kaya za wanawake, kaya za wazee, kaya zenye wanafamilia walemavu na makabila yaliyo katika hali hatarishi yalichunguzwa. Jedwali ES - 9 linadokeza muhtasari wa matokeo.

Jedwali ES - 9 : Upimaji wa Hali Hatarishi Mahususi

Mazingira magumu	Mawanda ya Hali Hatarishi
Wanawake	☐ Ni rasilimali watu yenye majukumu yasiyolipwa ambayo ni pamoja na utunzaji wa watoto, kuandaa chakula na kuchota maji na kuni. ☐ Pale wanawake wanapokuwa wakuu wa kaya majukumu huongezeka. Hata hivyo, kwa kawaida wanawake hawashirikishwi katika maamuzi na hivyo kutengwa katikauongozi na mchakato wa utoaji maamuzi ya kijiji. ☐ Hali hatarishi mengine yanayoweza kuongeza ugumu wa maisha ya wanawake walio wakuu wa kaya, ni kama vile kuwepo kwa wanafamilia walemavu na upatikanaji hafifu/finyu wa ardhi).
Kaya za Wazee	☐ Umasikini au ukosefu wa mapato Kifedha ☐ Maswala ya kiafya yanayoleteleza ugumu wa kujikimu na kujikinga ☐ Kiwango kidogo cha uchangamano wa kijamii na kutegemea zaidi msaada wa watoto, ndugu na majirani ☐ Changamoto za kujongea na kufikia maeneo yanayotoa ustawi wa maisha na huduma za kijamii
Kaya zenye Wanafamilia Walemavu	☐ Kupungua kwa Ulinzi wa ustawi wa maisha, mjongeo na mapato ya kaya ☐ Kuongezeka kwa matumizi ya huduma ya afya
Makundi ya Kikabila yaliyo katika Mazingira Magumu	☐ Haki ambazo hazitambuliki kila wakati na serikali. ☐ Athari kwa shughuli za ustawi ya wafugaji kutokana na kuhamishwa. ☐ Kuingiliwa kwa ardhi ya jadi na Miradi ya kibiashara na hifadhi za wanyamapori. ☐ Ushahidi kwamba mahudhurio ya shule miongoni mwa kabila zilizo katika hali hatarishi ni wa chini na viwango vya utoro na kuacha shule ni vya juu zaidi kuliko watanzania wengine.

Mikakati ya Ustawi wa Maisha kwa Kaya zilizo katika Hali Hatarishi

Kaya nyingi zilizoathiriwa na ukanda wa mkuza katika Mkoa wa Kagera hutegemea ardhi kwa ajili ya kujikimu na kupata kipato. Kaya zilizo katika hali hatarishi zitaguswa hasa kwa kupoteza ardhi. Mpango wa kushughulikia hali hii kwa mguswa mmoja mmoja utajumuisha:

☐ Mipango ya uboreshaji wa mazao;

- ☐ Mipango ya uboreshaji wa ufugaji wanyama na kuku, hasa kuku wanaoweza kufugwa kwa wingi katika eneo dogo na kuzalisha faida kubwa Zaidi; na
- ☐ Mipango isiyohitaji ardhi kama biashara na ukuzaji ujuzi.

Inawezekana ustawi wa maisha ukaguswa baada ya kuhamishwa, kwa mfano mazao kuharibika kutokana na sababu za tabia ya nchi. Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera umebaini hatua za kuzuia hatari zilizopo kwa watu walio katika hali hatarishi wanaoguswa na Mradi kama ifuatavyo:

- ☐ Kutoa msaada na kujenga uwezo wa kuendeleza ardhi na uzalishaji;
- ☐ Kutoa mafunzo ya kusaidia watu walioguswa na Mradi kusimamia fedha zao zilizopatikana wakati wa fidia;
- ☐ Ufuatiliaji wa kaya zilizoguswa na Mradi baada ya kuhamishwa, na;
- ☐ Msaada kwa kaya zilizo katika mazingira magumu zilizoguswa na Mradi ili kuweza kuendeleza upya mashamba kwa sababu ya uhaba wa wafanyakazi.

Mchakato wa Ushirikishwaji wa Makundi yaliyo katika Hali Hatarishi

Jambo la msingi la kusaidia makundi yaliyo katika hali hatarishi ni kuhakikisha kuwa wanapata fursa katika mchakato wa ushirikishwaji na hivyo; kupewa taarifa ya kutosha kuhusu Mradi, pamoja na athari na fursa wanazoweza kupata; wanaweza kuitikia na kutoa mrejesho ili kusaidia kuboresha michakato na shughuli ambazo wanashiriki na mchakato wa maendeleo unaolinda kwa ukamilifu haki za binadamu, utu, matamanio, utamaduni, na ustawi wa maisha utokanao na maliasili

Katika muktadha wa jumla wa ushirikiswaji wa kaya zilizoguswa na Mradi, Mradi umekuwa makini sana kuhakikisha upatikanaji wa habari na ushirikishwaji wa wanawake na wenzi wao, pia kutekeleza hatua zilizolengwa za kuhakikisha uwezekano wa uwepo wa ushirikishwaji wa kutosha wa kiutamaduni wa kabila zilizo katika hali hatarishi (ambao wanaweza kuwa katika hali hatarishi kutoka na athari za uhamishwaji zinazotokana na Mradi.)

Utekelezaji wa Msaada kwa Makundi Yaliyo katika Hali Hatarishi.

Watu na Kaya mbalimbali zitahitaji viwango mbalimbali vya msaada na usaidizi wakati wa utekelezaji wa uhamishaji watu na makazi kwa kutegemea hali hatarishi mahususi ya mazingira yao. Mipango mahususi ya kulinda na kusaidia makundi yaliyo katika hali hatarishi itazingatiwa wakati wa utekelezaji.

Mpango wa kusaidia waguswa walio katika hali hatarishi (VPP) unaenda sambamba na utekelezaji wa Mpango kazi wa Uhamishaji wa watu na makazi (RAP) na

utahitimishwa pale tu ambapo ustawi wa maisha wa watu walio katika hali hatarishi utaboreshwa angalau kwa viwango kama ilivyokuwa kabla ya Mradi. Mpango wa urejeshaji wa maisha kwa waguswa waliokatika hali hatarishi (Vulnerable People Plan) unaweza kuboreshwa wakati wa utekelezaji wa Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP)

10. MASHAURIANO NA UWAZI

Sura ya 10 Inaeleza Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) katika Mkoa wa Kagera kwa kufafanua namna majadiliano na wadau yalivyofanyika. Inaelezea utambuzi wa wadau, muundo na mbinu za ushirikishwaji wadau na mashauriano yaliyofanyika.

Mradi umezingatia ushirikishaji wenye tija kwa wadau wote kwa kuzingatia kanuni za uwazi na ushiriki, kusikilizana na majadiliano, uwezeshaji kupitia ushiriki, utoaji taarifa unaozingatia muda muafaka, ushirikishaji usio danganyifu wala usiotumia nguvu ya kulazimisha wadau, matumizi ya zana bora za ushirikishaji, kuheshimu haki za binadamu, jinsia na utamaduni wa watu.

Utambuzi wa Wadau

Wadau wenye nia na walioguswa na wanaohusika katika Mpango kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) ya mkoa wa Kagera wametambuliwa na wako katika kategoria zifuatazo: Wadau wanaoguswa moja kwa moja ikiwa ni pamoja na waguswa,kaya na jamii zinazohusika; Wadau wengine wenye nia ni pamoja na Serikali ya Tanzania na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, Asasi za Kiraia ikiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Mashirika ya Kijamii (CBOs).

Miundo ya Ushirikishwaji katika Mradi

Miundo kadhaa inahusika katika uandaaji wa mipango ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) ya mkoa wa Kagera. Miundo hii imeonyeshwa katika kielelezo**Error! Reference source not found.** kifuatacho hapo chini:



Kielelezo ES - 6: Timu ya Mradi ya Kupanga na Kutekeleza RAP

Mashauriano Wakati wa awamu ya Utekelezaji wa Uhamishaji Watu na Makazi

Ushirikishwaji ulijikita katika mahitaji ya vikundi mbalimbali vya wadau kwa kuzingatia hali ya utwaaji wa ardhi na awamu za uhamishaji watu na makazi. Aina za mikutano ni pamoja na:

- ☐ Mikutano ya Kikundi Kazi Cha Utwaaji Ardhi na Uhamishaji Watu na Makazi (LARWG), Mikutano na idara maalum za serikali, Serikali ya Mkoa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs);
- ☐ Mikutano ya Wilaya, Mabaraza ya Kata (WDC), Mabaraza Vijiji (VDC) na Mikutano Mikuu ya Vijiji;
- ☐ Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGDs) na vikundi vya Wachache/vikundi maalum vya wadau kama vile makabila yaliyo katika hali hatarishi, wanaume, wanawake na Waguswa / Kaya Zilizoguswa na Mradi; na

- ☐ Majadiliano ya ana kwa ana yaliyo rasmi na yasiyo rasmi na mmoja mmoja wa Kaya / Watu Walioguswa na Mradi pamoja na kabila zilizo katika hali hatarishi.

Mara nyingi mikutano ya Wadau iliendeshwa kwa Kiingereza na Kiswahili. Tafsiri kwa lugha zingine kama vile Kimasai zilifanyika ikiwa tu pale ambapo wadau walionekana kukosa ufahamu na/au wameshindwa kuzungumza Kiswahili.

Jedwali ES – 10 Linaonyesha idadi ya mikutano rasmi ya Awamu za vikao vya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) vilivyofanyika (hadi kipindi cha kuandaa RAP) na wadau waliohudhuria (ukiondoa timu ya watu kutoka kwenye Mradi na Washauri wa Mradi kwenye maswala ya RAP).

Jedwali ES - 10: Idadi ya Mikutano na Mahudhurio

Aina ya Mkutano	Mikutano ya uhamasishaji haji	Mikutano ya Uthibitishaii	Mikutano ya makazi	Mikutano ya Utoaji Taarifa	Mikutano ya utoaji taarifa	JUMLA
Mikutano ya Ngazi ya Mkoa	1	3	hakuna	hakuna	2	**6**
Mikutano ya Ngazi ya Wilaya	5	7	38	3	8	**61**
Mikutano ya Ngazi ya Kata	19	19	5	hakuna	17	**60**
Mikutano ya Ngazi ya Kijiji	49	20	107	hakuna	35	**211**
JUMLA	**74**	**49**	**150**	**3**	**62**	**338**
Mahudhurio Ngazi ya Mkoa	42	111	hakuna	hakuna	110	**263**
Mahudhurio Ngazi ya Wilaya	18	16	157	9	21	**221**
Mahudhurio Ngazi ya Kata	144	368	94	hakuna	245	**851**
Mahudhurio Ngazi ya Kijiji	412	298	1509	hakuna	321	**2 540**
Mahudhurio ya mkutano wa kijiji	2 700	374	hakuna	hakuna	995	**4 069**
JUMLA	**3316**	**1167**	**1 760**	**9**	**1 692**	**7944**

Masuala na Malalamiko

Rejista ya masuala na malalamiko imejumuishwa katika sura hii. Idadi ya maswali na masuala yanayohusiana na ardhi na uhamishaji watu na makazi ilipungua kwa kiasi kikubwa wakati wa mikutano ya uhamasishaji, uthibitishaji na SELI. Hili linathibitisha kwamba, kwa sehemu kubwa, uwazi katika mchakato wa utoaji habari wakati wa uhamasishaji ilitoa ufafanuzi wa kina na wa kueleweka juu ya ardhi na uhamishaji watu na makazi.

Utaratibu wa Usimamizi wa Malalamiko na nyaraka zinazohusika zimeandaliwa na kufanyiwa kazi katika ngazi ya Mradi. Jumla ya lalamiko Moja (1) linayohusiana na utwaaji wa ardhi na uhamishaji watu na makazi yalipokelewa na mtaalamu wa RAP katika Mkoa wa Kagera.

11. UTEKELEZAJI WA UTWAAJI WA ARDHI NA UHAMISHAJI WATU NA MAKAZI

Sura ya 11 Inatoa muhtasari wa shughuli muhimu na michakato inayohitajika katika utekelezaji wa RAP katika mkoa wa Kagera na ukamilishaji wa utwaaji wa ardhi pamoja na utoaji wa hati. Hii ni pamoja na majukumu ya msingi ya wadau muhimu, na Kampuni ya Mradi na Serikali ya Tanzania.

Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera utafanyika kwa awamu tatu (kama zilivyoonyeshwa hapo chini). Mbinu ya kutumia awamu itawezesha uandaaji wa bajeti na ratiba kufanyika kwa usahihi, pamoja na ushirikishwaji wa wadau unaowahusisha wadau na vilevile kuhakikisha shughuli na michakato muhimu inafanyika kwa ukamilifu katika mtiririko na mantiki sahihi.

Awamu tatu za utekelezaji zinaelezwa kwa kifupi hapa chini (baadhi ya shughuli zinafanyika sambamba na nyingine kwa mfuatano):

- ☐ **Upangaji wa Utekelezaji wa RAP**. Katika awamu hii kazi zitajikita katika mahitaji ya kisheria ya utwaaji na ubadilishaji wa ardhi. Ushiriki wa mwisho utazingatiwa wakati wa uamuzi wa utoaji stahiki na vigezo vya fidia.
- ☐ **Utekelezaji.** Awamu hii itashughulikia uandaaji na utiaji saini wa makubaliano ya fidia ya kaya na utekelezwaji wa matakwa ikiwa ni pamoja na malipo ya fidia, ujenzi au makazi mbadala, uhamishwaji na msaada katika kipindi cha mpito; na
- ☐ **Shughuli Saidizi katika Mradi**. Hii itajumuisha shughuli za uanzishaji na uendelezaji wa uboreshaji wa shughuli mbalimbali za urejeshaji wa ustawi wa maisha (kama ilivyoelezwa katika Sura ya 8), hali kadhalika utekelezaji wa programu ya ufuatiliaji na tathmini (kama ilivyelezwa katika Sura ya 13).

Ushirikishwaji wa wadau na usimamizi wa malalamiko utaendelea kipindi chote cha Mradi.

Wajibu na Majukumu ya Utekelezaji

Ili kuhakikisha kuwa Mradi unazingatia umiliki na uwajibikaji katika mchakato mzima, shughuli za utekelezaji wa RAP kwa mujibu wa mchakato wa utwaaji wa ardhi (taz. ES-5 na Sura ya 4) zitasimamiwa na Timu ya Mradi wa EACOP na Serikali ya Tanzania. Majukumu na wajibu katika awamu ya utekelezaji wa RAP katika mkoa wa Kagera yameandikwa kwa kifupi katika jedwali ES - 11 hapo chini.

Jedwali ES - 11: Majukumu na wajibu katika awamu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera.

Shughuli	Majukumu ya Kampuni ya Mradi / PPT	Majukumu ya Serikali ya Tanzania
[Hatua ya 5] Kuchapisha Rasmi katika Gazeti la Serikali, na Ubadilishaji Ardhi kuwa Ardhi ya jumla]	☐ Kutoa ramani na taarifa (inayojumuisha orodha ya vijiji vilivyoguswa) ya mahitaji ya ardhi ya Mradi kwa kila kipengele ☐ Kupitia sehemu za gazeti rasmi na maagizo yoyote na/au notisi kabla ya kuchapishwa kwenye gazeti. ☐ Kutoa muda kwa Serikali na mchango wa notisi ya maneno kwa nia ya kutwaa ardhi ikiwa inawezekana.	☐ Kuandaa, kutoa na kuchapisha maagizo na/au notisi katika gazeti rasmi la Serikali kwa mujibu wa sheria ya utwaaji ardhi (LAA) ☐ Kuchukua hatua na vitendo stahiki ili kukidhi masharti ya sheria ya utwaaji wa ardhi (LAA), ikiwa ni pamoja na uchapishaji katika gazeti rasmi la serikali na utwaaji wa ardhi, na ubadilishaji wa ardhi (kwa wakati uliokubaliwa na Mradi) kuwa ardhi ya jumla kama ilivyokubaliwa na Mradi[14]
[Hatua ya 6] Makubaliano ya Fidia		
Maelezo Mafupi ya Stahiki na Fidia.	☐ Toa maelezo mafupi ya ziada juu ya stahiki katika ngazi ya kijiji kueleza na kujadili stahiki kwa Watu Walioguswa na Mradi	☐ Msaada wa ziada unaotolewa na Serikali ya Tanzania kwa mamlaka za Wilaya, Kata na Vijiji.

[14] Hii itajumuisha, bila kufungwa na: idhini zote zinazohitajika kutoka katika mamlaka za Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na mamlaka za Serikali: azimio la mambo yote yanayohusiana na mipango; uchunguzi muhimu na ripoti; na notisi kama ilivyoelekezwa chini ya mfumo wa sheria na uchapishaji wa haya, kama inavyotakiwa katika gazeti la serikali. Tangazo la ardhi kwa ajili ya matumizi ya umma na ubadilishaji ardhi ya Kijiji na ya hifadhi kuwa ardhi ya jumla itafanyika wakati huo huo.

Shughuli	Majukumu ya Kampuni ya Mradi / PPT	Majukumu ya Serikali ya Tanzania
Kuandaa na Kusaini Makubaliano ya Fidia	☐ Kuongoza ushiriki wa Watu Walioguswa na Mraidi (PAP) na jamii ili kufikia makubaliano ya fidia. ☐ Watia saini katika makubaliano ya fidia chini ya majadiliano na Serikali ya Tanzania. ☐ Kutambua visa vitakavyohitaji ushirikishwaji wa mamlaka ya serikali ya Tanzania katika utwaaji wa ardhi wa lazima na uwezeshaji wa mchakato kadri inavyowezekana	☐ Watia saini katika makubaliano ya fidia chini ya majadiliano na serikali ya Tanzania. ☐ Kutoa msaada ikiwa mchakato wa ushiriki utashindwa kufikia makubaliano juu ya fidia
[Hatua ya 7] Malipo ya Fidia, Uhamishaji na Utekelezaji wa Programu za Urejeshaji ustawi wa Maisha na Utoaji msaada		
Malipo ya Fidia	☐ Malipo ya fidia (Utayarishaji wa malipo stahiki kwa mujibu wa sheria za Tanzania ni suala la majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Mradi)	☐ Mamlaka ya Utwaaji wa ardhi (Utayarishaji wa malipo stahiki kwa mujibu wa sheria za Tanzania ni suala la majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Mradi) ☐ Usimamizi wa fidia na utaratibu wa uhamishaji.
Ujenzi wa Nyumba Mbadala.	☐ Maandalizi ya viwanja mbadala kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbadala. ☐ Kuwezesha usajili wa ardhi mbadala na malipo ya gharama zote yatakayotokana na mchakato wa kupata ardhi na ujenzi wa nyumba mbadala.	☐ Utwaaji rasmi wa ardhi, uhamishaji na usajili utazingatiwa kama ilivyo katika sheria za Tanzania.

Shughuli	Majukumu ya Kampuni ya Mradi / PPT	Majukumu ya Serikali ya Tanzania
Uhamishaji na Msaada katika kipindi cha mpito.	☐ Kutoa muda na makubaliano ya namna ya kuwapa Watu Walioguswa na Mradi notisi ya kuhama. ☐ Kutoa msaada wa kipindi cha mpito (pale inapobidi).	☐ Kwa makubaliano na kampuni ya Mradi/PPT, andaa mambo kwa wakati unaotakiwa na kampuni ya Mradi / PPT na uchapishe notisi ya kupata umiliki ardhi kisheria (kuondoka) kwa PAP (na Vijiji vilivyoguswaa na Mradi, kwa mujibu wa LAA).
Utekelezaji wa Programu za Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha na Utoaji Msaada.	☐ Uendelezaji wa Programu za Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha na Utoaji msaada kwa Watu Walioguswa na Mradi. ☐ Majadiliano kwa kushirikiana na wataalamu katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, taasisi zisizo za kiserikali na za kijamii. ☐ Kutathmini watoa huduma wa ndani wenye uwezo wa kutoa msaada wa mafunzo wakati wa utekelezaji wa programu na baada ya utekelezaji. ☐ Uhamasishaji wa rasilimali watu, fedha na vifaa vingine vitakavyohitajika	☐ Msaada na ushirikiano na Ofisi ya Kilimo ya Wilaya. ☐ Mradi kuwa na mawasiliano na wataalamu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.
[Hatua ya 8] Utoaji wa Haki na [Hatua ya 9] Hati ya Ardhi.		☐ Serikali ya Tanzania itachukua hatua zote muhimu kutoa kwa mamlaka husika Haki ya Kutoa ardhi inayohitajika kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa na IGA.

Shughuli	Majukumu ya Kampuni ya Mradi / PPT	Majukumu ya Serikali ya Tanzania
		☐ Mamlaka inayohusika itoe hati kwa Mradi kwa muda unaohitajika ambao unatoa haki ya ardhi kwa Mradi kwa kufuata kanuni zilizowekwa katika IGA (na makubaliano mengine yanayohusika kwa wakati huo kati ya Nchi na PPT).

Ushiriki wa Wadau wakati wa Utekelezaji wa RAP katika Mkoa wa Kagera

Ushiriki wa wadau katika hatua zote za upangaji na utekelezaji wa uhamishaji watu na makazi ni muhimu. Jedwali ES – 12 linaonyesha mpango kazi wa ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishiji Watu na Makazi (RAP) katika Mkoa wa Kagera.

Jedwali ES - 3: Mpango Kazi wa Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa RAP katika Mkoa wa Kagera

Kundi la Wadau	Maelezo ya shughuli	Matokeo
Ushirikiano na Mamlaka za Mkoa na Wilaya	Mrejesho wa mara kwa mara na mikutano ya ushauri na mamlaka za mkoa na wilaya kwa: ☐ Kutoa taarifa za maendeleo ya shughuli zilizokamilika; ☐ Kujadili kuhusu shughuli zitakazofuata; ☐ Kutafuta mwongozo juu ya mahitaji ya kisheria; ☐ Kutoa mrejesho juu ya malalamiko yaliyopokelewa na kutatuliwa; na ☐ Kupata mrejesho na kuhusisha kwenye mipango ya Mradi ipasavyo.	Muhtasari wa vikao. Mahudhurio. Mialiko ya vikao.

Kundi la Wadau	Maelezo ya shughuli	Matokeo
Ushiriki wa Kikundi Kazi cha Utwaaji Ardhi na Uhamishaji Watu na Makazi (LARWG).	Mrejesho wa mara kwa mara na mikutano ya ushauri na LARWG kwa: ☐ Kutoa taarifa za maendeleo ya shughuli zilizokamilika; ☐ Kujadili kuhusu shughuli zitakazofuata; ☐ Kutafuta mwongozo juu ya mahitaji ya kisheria; ☐ Kutoa mrejesho juu ya malalamiko yaliyopokelewa na kutatuliwa; na ☐ Kupata mrejesho na kuhusisha kwenye mipango	Muhtasari wa vikao. Mahudhurio. Mialiko ya vikao.

Ushiriki wa PAP (pamoja na kaya na jamii zilizoguswa na Mradi - PAHs and PACs).	Ushiriki utajumuisha: ☐ Kuonyesha taarifa za makubaliano ya uhamishaji watu na makazi na taarifa kwa Watu Walioguswa wa Mradi (PAP) na kaya husika kuhusu fursa ya kuchagua fidia stahiki ya uhamishwaji watu na makazi; ☐ Mikutano ya mara kwa mara ya jamii husika ili kuweka wazi taarifa muhimu na kutoa ushauri kwa waguswa juu ya fursa za uhamishaji watu na makazi na pia kutoa taarifa ya kinachoendelea juu ya maendeleo ya mchakato wa uhamishaji watu na makazi; ☐ Rekodi ya chaguzi/ mapendekezo ya Watu/Kaya Zilizoguswa na Mradi; ☐ Taarifa kwa waguswa juu ya shughuli muhimu zinazohusiana na malipo ya fidia na kuanza kwa ujenzi wa nyumba mbadala; ☐ Kuambatana na Watu Walioguswa na Mradi kwenda katika (ma) eneo ambapo nyumba mbadala zinajengwa (kulingana na jedwali ya ziara); ☐ Ushirikiano wa ana kwa ana na watu walioguswa na mradi ili kusaidia uelewa wa makubaliano juu ya fidia /msaada; ☐ Ufuatiliaji wa mara kwa mara na tathmini kuhusiana na ushiriki wa waguswa, washirika wa utekelezaji wa RAP na wadau wengine wanaohusika; na ☐ Majadiliano na shughuli zinazohusiana na urejeshaji wa ustawi wa maisha.	Nukuu / Muda wa majadiliano/ mikutano. Mialiko ya vikao. Makubaliano yaliyosainiwa.

12. UTEKELEZAJI WA BAJETI NA RATIBA

Utekelezaji wa bajeti na ratiba ya Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera umeelezwa katika **Sura ya 12.** Vipengele vyote vilivyozingatiwa katika utayarishaji wa bajeti vimeelezewa na uzingatiaji wa ratiba umewasilishwa.

Makisio ya bajeti ya utekelezaji wa RAP yameandaliwa kwa kuzingatia uzito wa taarifa ya uhamaji iliyotolewa katika Sura ya 6. Fidia zote za fedha zilizomo kwenye taarifa ya waguswa walio katika hali hatarishi na jedwali la fidia vimejumuishwa kwenye bajeti. Fidia zilizo katika mfumo wa vitu mbadala na stahiki zingine zitathaminishwa katika fedha kwa ajili ya uandaaji wa bajeti. Makadirio ya bajeti katika hatua hii ni elekezi na yatahitaji uboreshaji zaidi. Vipengele vikuu vya bajeti ni kama vifuatavyo:

- ☐ Gharama ya **ardhi** ni thamani ya eneo la ardhi litakalochukuliwa na Mradi.
- ☐ Wamiiliki wa **nyumba na makazi kamili yaliyoguswa** kwa kuchukuliwa na Mradi watachagua kati ya fidia ya fedha na mbadala wa miundombinu;
- ☐ Fidia ya fedha kwa **mazao na miti ya biashara** imejumuishwa kwenye bajeti, kwa kuzingatia viwango vya uthamini vilivyoamuliwa wakati wa uchunguzi wa uthamini;
- ☐ **Posho za kujikimu** zimekadiriwa ikiwa ni pamoja na posho ya usumbufu, uhamishaji wa vitu na uchumi kwa kaya zilizohamishwa na posho ya usafiri kwa watu waliohamishwa;
- ☐ Fidia ya **kuhamisha makaburi**;
- ☐ Bajeti ya hatua za **urejeshaji wa ustawi wa maisha** inajumuisha mambo makuu matatu, gharama inayohusiana na, msaada katika kipindi cha mpito; gharama zinazohusiana na mguswa binafsi; na kiwango cha kaya cha urejeshaji wa ustawi wa maisha na gharama zinazohusiana na hatua za urejeshaji ustawi wa maisha katika kiwango cha Jamii au Kijiji;
- ☐ Msaada wa ziada unahitajika kwa **watu au kaya zilizo katika hali hatarishi.** Posho itawekwa katika bajeti ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) kwa msaada na itafuatiliwa kwa ukaribu zaidi; na
- ☐ Bajeti kwa ajili ya rasilimali zinazohitajika katika **utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP).**

Ratiba ya Mwongozo wa Utekelezaji

Mpango Kazi wa Uhamisahaji wa Watu na Makazi (RAP) una ratiba ya mwongozo wa utekelezaji. Inatarajiwa kwamba kukamilika kwa shughuli muhimu za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamisahaji wa Watu na Makazi (RAP) katika Mkoa wa Kagera utachukua takribani miezi 21 kutoka Uamuzi wa Mwisho wa Uwekezaji ulipofanyika.

Pamoja na shughuli muhimu za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamisahaji wa Watu na Makazi (RAP) kuna jitihada kadhaa ambazo zitaendelea hata baada ya kipindi cha miezi 21. Hizi ni pamoja na ushirikishwaji wa wadau, urejeshaji wa ustawi wa maisha na mipango ya usaidizi na upimaji na tathimini.

13. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Sura ya 13 Inaelezea mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na mfumo utakaotumika katika RAP ya mkoa wa Kagera. Sura hii inafafanua malengo ya ufuatialiji na tathmini, inaelezea asili, malengo na kusudi la aina mbalimbali za ufuatiliaji na tathmini na pia inaonyesha mahitaji ya taarifa zilizounganishwa na ufatiliaji na tathmini.

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi utajumuisha michakato ya ndani, na nje ya ufuatiliaji shirikishi na utoaji taarifa ili kuhakikisha kuwa taarifa kamili na lengwa inatolewa.

Viashiria vitachaguliwa kupima kazi, matokeo, na athari kwa ajili ya shughuli za uhamishaji watu na makazi na vitalenga kutoa mrejesho kwa Mradi na vile vile kwa wadau wanaohusika na utekelezaji wa mchakato wa RAP katika mkoa wa Kagera. Mchakato wote wa Ufuatiliaji na Tathmini utaunganishwa na uchunguzi wa kiwango cha Kaya cha kiuchumi-jamii na mali unaofanyika kwa maendeleo ya Mpango Kazi wa Uhamisahaji wa Watu na Makazi (RAP) katika mkoa wa Kagera.

Mchakato huu pia utathibitisha viwango vya mafanikio ya hatua za urejeshaji wa ustawi wa maisha na kwa sababu hiyo Ufuatiliaji na Tathmini za athari za uhamishaji watu na makazi utaendelea kwa kipindi kinachofaa baada ya shughuli zote za uhamishaji watu na makazi kukamilika.

Aina kuu nne za ufuatiliaji na Tathmini zitafanyika:

- ☐ **Ufuatiliaji wa Machakato:** hii ni shughuli ya ufuatiliaji wa ndani ambao unafuatilia athari za mchakato wa utekelezaji wa RAP, kwa watu, kaya na jamii husika zilizoguswa na Mradi. Taarifa ya robo mwaka itaandaliwa na jopo la utekelezaji wa RAP.
- ☐ **Ufuatiliaji wa Uhakiki vigezo:** Aina hii ya ufuatiliaji itahakikisha kama utekelezaji wa RAP unakidhi malengo yaliyoelezewa kwenye RAP ya mkoa wa Kagera. Ufuatiliaji wa uhakiki vigezo unapaswa kufanyika kila baada ya robo ya mwaka wakati wa utekelezaji na kwa miaka miwili inayofuata RAP, baada ya hapo utafanyika mara mbili kwa mwaka.
- ☐ **Kumalizika kwa ukaguzi:** Kukamilika kwa ukaguzi kutafanywa na chombo huru ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa RAP ya mkoa wa Kagera unakidhi viwango muhimu, unarudisha na kuboresha Maisha ya PAPs. Muda wa kumalizika kwa ukaguzi utachochewa na vitu vingi vya utekelezaji ila inakisiwa kuwa mizunguko mitatu baada ya uanzishaji wa mfumo wa sera ya urejeshaji wa ustawi wa maisha LRP.

- ☐ **Tathmini baada ya kukamilika kwa Mradi:** Tathmini ya baada ya kukamilika kwa Mradi itafanywa na chombo huru chenye sifa ya kutathmini kwa wakati uliopangwa na baada ya ukaguzi wa kukamilika kwa Mradi.

Huduma za Kijamii na Uhamishaji Watu na Makazi kwa Ajili ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania

Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi Katika Mkoa wa Kagera

Sura ya 6

MFUMO WA STAHIKI, HAKI NA FIDIA

6.1 Utangulizi

Mfumo wa Stahiki, Haki na Fidia unaelezea vigezo vya stahiki kwa Watu Walioguswa na Mradi ili kupatiwa fidia na msaada wa uhamishaji watu na makazi, unaeleza stahiki zilizopendekezwa kwa kila aina ya athari ya uhamishwaji inayotokana na Mradi, na unaamua viwango na thamani ya fidia inayotumika.

Sura hii inajadili mambo ya yafuatayo:

- ☐ **Stahiki:** Inafafanua na kueleza “mguswa” anayestahiki kupata fidia na msaada wa uhamishaji watu na makazi;
- ☐ **Haki**: Inaeleza aina ya fidia na msaada ambao kila kategoria ya walioguswa na Mradi wanastahiki kupata, ikiwa ni pamoja na msaada wa urejeshaji wa ustawi wa maisha na stahiki za watu walio katika mazingira magumu, yote mawili yanatokana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya fedha. Kipengele hiki kinaeleza kwa kina mfumo wa haki; na
- ☐ **Uthamini na fidia:** unafafanua “namna” ambayo mali mbalimbali zilizoguswa zimethaminishwa pamoja na viwango na aina ya fidia zitakazotolewa kwa watu walioguswa na Mradi. Hii inajumuisha a) Mbinu zilizotumika katika kuamua tathmini na fidia chini ya Kanuni zote mbili za Tanzania na b) Mahitaji ya Viwango vya Fedha vya Kimataifa kuthamini hasara katika hali ya kukosekana kwa miongozo iliyowekwa au fidia iliyoamriwa. Kama ilivyotajwa hapo awali, stahiki za Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha pamoja na stahiki kwa watu waishio katika mazingira magumu ni hitaji maalumu la IFC, na kwa hiyo haki hizi zimejumuishwa katika sehemu hii.

6.2 Stahiki

Kulingana na maelezo ya Shirika la Fedha la Kimataifa, Stahiki ni “… Haki ya fidia na msaada uliotolewa kwa watu, vikundi vya watu, familia, au taasisi kwa sababu ya uhamishwaji kutokana na utwaaji wa ardhi, uondoaji wa haki, na/au kutaifishwa mali kwa ajili ya Mradi.

Matakwa ya msingi ya stahiki ni kwamba watu na mali zilizoguswa na Mradi zimetajwa wakati wa mchakato wa uthamini wa mali na uhamishaji watu na makazi. Kwa maneno mengine, stahiki zinatambulika tu kwa fidia ya ardhi na mali zilizokuwepo kabla ya tarehe ya mwisho (Tazama kifungu 6.2.2). Uandaaji na usambazaji wa awali wa vigezo vya stahiki, pamoja na utekelezaji wa Tarehe ya

Katazo, vinasaidia katika kudhibiti madai ya watu wasiostahili fursa husika na makazi.

Vigezo vya stahiki vinavyotumika katika Mpango Kazi wa Uhamisahaji wa Watu na Makazi (RAP) viliamriwa mwanzoni mwa Mradi, kama ilivyoainishwa katika Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi (RPF), na vinazingatia matakwa ya viwango vya utendaji namba 5 (PS5) vya IFC na sheria za Nchi. Viwango Stahiki vya PS5 vya IFC vinafafanua aina tatu ya watu ambao wanastahili fidia:

- ☐ Watu waliohamishwa ambao wana haki rasmi kisheria ya umiliki wa ardhi na/au mali. Hii ni pamoja na watu walio na mali ambazo zimesajiliwa rasmi katika rejista ya ramani ya umiliki wa ardhi;
- ☐ Wale ambao hawana haki za kisheria za kumiliki ardhi lakini wana madai ya ardhi yanayotaambulika chini ya sheria ya nchi. Kundi hili linajumuisha watu wenye umiliki kimila/hati za umiliki wa ardhi: kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 3(1)(g) cha sheria ya Bunge ya Ardhi na kifungu cha 3(1)(h) cha Sheria ya Bunge ya Ardhi ya Kijiji, watu walio na Hati za Kisheria za Ardhi ni pamoja na wale wenye “hati ya umiliki au kutambuliwa makazi ya muda mrefu au matumizi ya kimila ya ardhi na kanuni za Ardhi ya Kijiji zinasema kwamba mwanakijiji yeyote anayeishi kwenye ardhi iliyoguswa chini ya haki ya kimila ya kumiliki, pamoja na haki isiyoandikwa, anastahiki ya kupewa fidia; na
- ☐ Wale ambao hawana haki ya kisheria inayotambulika au wanadai ardhi na/au mali wanazomiliki au kutumia. Kundi hili linajumuisha watu waliojenga majengo au wamelima mazao kwenye ardhi inayomilikwa na wengine, bila ya idhini na/au kumfahamisha mmiliki wa ardhi. Hii inajumuisha pia watumiaji wasio rasmi kwenye ardhi iliyohifadhiwa au ardhi ya jumla. Watu kama hao wanaweza wasiwe na stahiki ya kulipwa fidia ya ardhi, kwani hawana haki rasmi ya kumiliki ardhi; hata hivyo, wanaweza kuwa na stahiki ya kulipwa fidia ya mali wanazomiliki - kwa mfano, thamani ya uhamishwaji wa majengo, miundombinu, mazao, na miti ya biashara. Stahiki ya fidia haitengenezwi au kutoa haki ambapo hapakuwa na kitu chochote kinachostahili fidia hapo mwanzo – yaani haihalalishi umiliki haramu wa ardhi. Lengo la kutoa fidia ni kuhakikisha kwamba watu walioguswa na Mradi hawaishi katika umasikini kwa sababu ya uhamishwaji.

6.2.1 Kategoria za Stahiki

Kategoria za stahiki zilizoorodheshwa hapo chini zinarejea aina ya wadau na Watu walioguswa na Mradi wenye uwezekano wa kukumbwa na aina mbalimbali za hasara zilizosababishwa na uhamishwaji au kuongezeka kwa hali hatarishi kutokana na uhamaji na / au uyumbishwaji wa kiuchumi unaotokana na uchukuliwaji wa ardhi

inayohitajiwa na Mradi kwa ajili ya Mkuza wa bomba na miundombinu juu ya ardhi, Mkoa wa Kagera.

Aina za stahiki zinazohusiana na RAP ni kama zifuatazo:

- ☐ Watu wanaomiliki ardhi kisheria au umiliki wa kimila;
- ☐ Watu wanaomiliki majengo yaliyoguswa kama vile makazi, majengo mengine saidizi ya nyumbani kama vile vyoo, miundombinu ya kilimo, nk;
- ☐ Mali zilizoguswa na mkuza wa bomba ikiwa ni pamoja na mali zinazosimamiwa na Halmashauri za Kijiji /Mtaa;
- ☐ Taasisi ambazo zinamiliki ardhi na/au majengo, na/au miundombinu ya umma ikiwemo majengo ya kidini na mali zinazomilikiwa na mamlaka za serikali (mali hizo ni pamoja na shule, vituo vya afya, barabara, ardhi iliyohifadhiwa, maeneo tengefu, nk);
- ☐ Wamiliki wa mazao ya muda mrefu na mazao ya kuvuna kwa mwaka
- ☐ Wamiliki wa mazao ya msimu (yanayopandwa na kuvunwa kila msimu);
- ☐ Wamiliki wa miti ya biashara iliyo katika maeneo yaliyoguswa, iwe kwenye ardhi yao au kwenye ardhi ya wengine;
- ☐ Wamiliki au wasimamizi wa mali ya urithi utamaduni kama vile makaburi, eneo la makaburi, nk;
- ☐ Wapangaji wa ardhi, ina maanisha, watu ambao ijapokuwa hawamiliki ardhi, lakini wanamakubaliano na wamiliki kutumia ardhi hiyo;
- ☐ Watumiaji wa ardhi wasio rasmi – kwa mfano, watu ambao wanakusanya kuni, dawa za asili, wawindaji na wanaovuna mali asili zingine;
- ☐ Watumiaji wa makazi na ardhi wasio rasmi
- ☐ Biashara zisizo rasmi/wachuuzi kama vile maduka, maduka ya nyama, pembejeo za kilimo (kama vile, mashine za kusagia nafaka) migahawa, wasusi, watengezaji wa nguo, watengezaji wa samani, vibanda vya kuuzia bidhaa, nk[15];
- ☐ Wafugaji wanaotumia ardhi kwa ajili ya kulishia mifugo; na
- ☐ Watu waishio katika mazingira magumu – yaani watu ambao upoteaji wa mali au rasilimali, na/au kuvurugika kwa mifumo ya utwaaji mali na rasilimali, kunaweza kuwasababishia kupata athari kubwa zaidi, kutokana na mazingira yao magumu na/au utegemezi wa ustawi wa maisha katika shughuli hizo.

Inafahamika kuwa Mtu aliyeguswa na Mradi anaweza kuangukia katika aina za stahiki zaidi ya moja (kwa mfano, ardhi, miundombinu na/au mazao). Tathmini ya

[15] Wakati wa uchunguzi wa kijamii na kiuchumi kulikuwa na baadhi ya kaya ambazo zilitoa taarifa ya kufanyia biashara kwenye nyumba zao. Kwenye hii RAP, hizo zimechukuliwa kama biashara zisizo rasmi.

mali vikioanishwa na Taarifa za Uthamini ndizo hutumika kuamua aina za stahiki, na haki, ambazo zinatumika kwa kila Mguswa Aliyeathiriwa na Mradi. Aidha, kuna Taasisi, Halmashauri za Vijiji (ambazo zinasimamia mali na ardhi ya jamii) na vyombo vingine vya serikali vyenye mali zilizoguswa na Mradi.

6.2.2 Tarehe ya Katazo

Tarehe ya Katazo ni kipengele muhimu wakati wa kueleza stahiki na haki. Tarehe ya Katazo inategemea mwanzo wa uthamini wa mali. Watu wanaokaa au kuhamia eneo la Mradi baada ya tarehe ya katazo hawastahiki fidia, au msaada wa uhamishaji watu na makazi. Vivyo hivyo, mali zisizohamishika (kama vile miundombinu, mazao na miti) zilizoendelezwa baada ya tarehe ya katazo hazitafidiwa.

Tarehe ya katazo si muhimu tu kwa usimamizi wa uharibifu na kudhibiti utwaaji wa makazi usio halali, bali pia ni muhimu katika kuandaa idadi kamili ya watu walioguswa na mradi ilikusaidia upangaji na kuandaa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa uhamishaji watu na makazi.

Katika Mkoa wa Kagera, tarehe ya katazo[16] iliamuliwa kutokana na mwanzo wa uthamini wa mali kama ilivvoelekezwa chini ya Sheria ya Bunge ya Usajili ya Uthamini na Wathamini ya mwaka 2016.

Aidha, tarehe ya katazo imepangwa kwa kila Kijiji kilichoguswa na mkuza wa bomba. Taarifa za tarehe hizi kama zinavyoonyeshwa katika sura ya 4, na taarifa ya uthamini ziliwekwa wazi kwa Watu Walioguswa na Mradi katika kila Kijiji na Mtaa husika.

6.2.3 Uhalali wa Uthamini

Tarehe ya Katazo inaonyesha “taswira” ya muda ambao uthamini wa mali ulifanyika. Ni wazi kuwa mabadiliko ya ‘kawaida’ yanayotokana na maendeleo jinsi muda unavyosonga ikiwa yamepangwa au hayakupangwa, yataendelea hata baada ya tarehe ya katazo.

Inatambulika kuwa Watu walioguswa na Mradi hawategemewi kusitisha mipango ya Maisha na maendeleo yao kwa kipindi kirefu kisichotambulika, na kwa hivyo ni

[16] Utaratibu huu uliongozwa na matakwa ya Sheria ya Bunge ya Usajili wa Uthamini na Wathamini ya mwaka, 2016.

muhimu kuweka kipindi maalum cha tarehe ya katazo. Hii pia imetamkwa katika mfumo wa sheria za Tanzania.

Kwa mujibu wa kifungu cha 52 sehemu ya 3 cha Sheria ya Usajili ya Uthamini na Wathamini, Ripoti za Uthamini lazima ziidhinishwe na Mthamini Mkuu ndani ya miezi (6) toka tarehe ya katazo "…uthamini utafanyika kwa kuzingatia maslahi ya mguswa wa mwisho".

Ripoti za Uthamini zitakuwa halali kwa kipindi cha miaka miwili zaidi baada ya tarehe ya kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serkali.

Tarehe ya uthamini kwa kuzingatia "maslahi ya mguswa wa mwisho" katika kila wilaya husika za Mkoa wa Kagera ilikuwa kama ifuatavyo:

- ☐ Missenyi: Tarehe 24 Octoba 2019,
- ☐ Bukoba: Tarehe 24 Octoba 2019,
- ☐ Muleba: Tarehe 25 Septemba 2019 na
- ☐ Biharamulo: Tarehe 3 Septemba 2019,

6.3 Haki

Matokeo ya uchunguzi wa kiuchumi-jamii na uthamini wa mali pamoja na vigezo vya stahiki vimetumika kutayarisha Mfumo wa Haki (Jedwali namba 6-1). Mfumo unafafanua kanuni na mbinu za fidia kwa kushirikisha haki za fidia kutegemea aina na kiwango cha mguswa.

Fursa zote za haki zimewasilishwa kupitia vikao vya wadau kama ilivyoelezwa kwa kina katika Sura ya 10, kipengele cha 10.6. Malengo ya mfumo wa haki yamebainishwa kama ifuatavyo;

- ☐ Aina zote za watu walioguswa, ikiwa ni pamoja na wamiliki wa mali na wamiliki halali wa ardhi, wapangaji, watumiaji wasio halali, wapangaji ambao hutoa sehemu ya mavuno kama kodi, wachungaji, wachungaji wa kuhama hama na watumiaji wengine wa maliasili, wauza duka, wafanyabiashara na watoa huduma wengine, jamii na makundi ya watu waishio katika mazingira magumu;
- ☐ Aina zote za hasara zinazohusiana na kila kundi, ikiwa ni pamoja na upotevu wa vitu; ukosefu wa njia ya kufikia vitu, hasara ya posho, kukosa kodi au mauzo, hasara ya miundombinu ya jamii, na upotevu wa mambo ya kiutamaduni; na

- ☐ Aina zote za fidia na msaada inayostahili kwa kila kategoria, ikiwa ni pamoja na fidia au mbadala wa ardhi na maliasili; miundombinu, kipato kinachotokana na kupangisha, nk; msaada endelevu na msaada wa urejeshaji wa ustawi wa maisha baada ya uhamishaji watu na makazi.

Mfumo wa Haki, ulionyeshwa katika Jedwali la 6-1 umejikita katika ufafanuzi wa mfumo wa haki ulioasisiwa kama sehemu ya Mfumo wa Sera ya Uhamishaji Watu na Makazi. Kwa kuwa asili na kiwango cha athari kinatofautiana katika kila mkoa, mfumo huu wa haki unajumuisha haki za athari za utwaaji wa ardhi katika njia bomba na miundombinu ya juu zilizobainishwa katika mkoa wa Kagera[17]. Upangiliaji wa kategoria za stahiki uliainishwa katika mfumo wa Sera za Uhamishaji Watu na Makazi (RPF) kwa ajili ya madhumuni endelevu.

[17] Ikiwa athari za ziada za uhamaji, ambazo hazikushughulikiwa katika mfumo wa haki wa Mpango Kazi wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP), utaainishwa wakati wa maendeleo ya mradi kwa hiyo idadi (matrix) ya haki iliyojumuishwa kwenye Sera ya Mfumo wa Uhamishaji Watu na Makazi (RPF) zitarejewa katika stahiki na haki.

Jedwali la 6-1: Mpango wa Stahiki – Mkoa wa Kagera (Njia ya Bomba na Miundombinu ya Juu ya Ardhi)

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
ARDHI					
A1	Upoteaji wa ardhi yenye makazi-kiwanja chote kilichopatikana (kwa sababu chote[20] kipo katika sehemu ya Mradi au ardhi iliyobakia imetengwa kama ardhi isiyo na mmiliki na athari za umiliki wa ardhi yote ya mguswa zinaweza kuathiri ustawi wa	Utwaaji (Upotevu wa ardhi wa kudumu).	Mmiliki wa kisheria wa ardhi. Mmiliki wa kimila wa ardhi. wamiliki wa kitaasisi.	***Fursa ya uchaguzi wa vitu mbadala namba 1:*** • Uhamishwaji wa ardhi yenye ukubwa sawa na ardhi iliyopotea (ardhi iliyotolewa inapatikana katika kata) yenye hati ya umiliki kulingana IFC PS 5 • Malipo ya gharama zote ya fedha[21] • Posho ya usumbufu;[22] na • Posho zingine kama zinavyoohusika	**G1** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi unaozingatia ardhi na usiozingatia ardhi; na • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha wa mguswa mmoja mmoja. Ambapo mbadala wa ardhi ya kilimo hauhusiki kwenye kata fursa ya kuchagua mpango mwingine wa ustawi wa maisha utatolewa kwa waguswa.

[18] Tazama Jedwali 6-6 kwa maelezo zaidi.

[19] Urejeshaji wa ustawi wa maisha umeunganishwa na mguswa na utakuwa na thamani ya jumla ya waguswa walio na ardhi na au mali zaidi ya moja zilizoguswa na Mradi.

[20] Miundombinu ya makazi ambayo ipo katika ardhi iliyoguswa katika eneo la Mradi au kwenye ardhi iliyobainika kutoguswa na Mradi. Waguswa wanaweza kuwa na shamba la ziada/ardhi nyingine nje ya eneo la Mradi ambayo bado inachukuliwa kuwa yenye faida.

[21] Kwa ununuzi au gharama za usajili takwimu halisi zitaasisiwa na serikali za mitaa.

[22] Tazama kipengele 6.4.1.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
	maisha).				
A2	Upotevu wa ardhi yenye makazi – sehemu ya kiwanja iliyotwaliwa (sehemu iliyobakia inafaa kwa matumizi ya kiuchumi)			***Fursa ya uchaguzi wa vitu mbadala namba 2:*** • Mbadala wa ardhi ya kiwanja cha makazi (kwa watu wachache) katika sehemu sahihi chenye umiliki halali kulingana na IFC PS5 kwa ajili ya ujenzi wa makazi mbadala (kama vinastaki chini ya B1/B2 na fursa ya chaguo la nyumba mbadala lililoteuliwa). • Fidia ya fedha kwa ardhi iliyoguswa na haikutolewa mbadala (kama inastahiki); • Mradi kusaidia utwaaji wa ardhi mbadala; • Posho ya usumbufu; na • Posho zingine kama inavyostahili Au **Chaguzi ya fedha**: • Fidia (kama inastahili) kwa ardhi iliyopotea kabisa katika viwango vya masoko kama ilivyoelezwa na Mthamini Aliyesajiriwa pamoja na	

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
				asilimia 10 kwa ajili ya gharama za uhamishaji fedha;[23] [24]na • Posho kama ilivyoonyeshwa hapo juu	
A3 & A4	Upotevu wa kudumu wa ardhi ya kilimo (mazao) ambapo kiwanja chote kimeguswa au eneo dogo limebaki katika ardhi iliyoguswa na mradi (ardhi yatima) na athari kwa waguswa kwa	Utwaaji (Upotevu wa kudumu).	Mmiliki wa kisheria wa ardhi. Mmiliki wa kimila, (mtu aliyeguswa na mradi atapoteza ekari sawa <AE AU AFS)[26].	• Fidia ya fedha (kama inastahili) kwa ardhi iliyopotea kabisa kwa kuzingatia viwango vya soko kama itakavyoelezwa na Mthamini aliyesajiriwa pamoja na asilimia 10 kwa ajili ya gharama za uhamishaji	**G4** Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi unaozingatia ardhi na usiozingatia ardhi; Kama mguswa atakuwa katika mazingira magumu, atapewa stahiki za ziada **G2**

[23] Pale inapowezekana, dhamana italipwa kutoka kwenye malipo ya fidia kwenda kwa taasisi ya kukopesha. Kanuni hii inatumika kwa mali yote ambayo imejumuishwa na dhamana.

[24] Viwango vya soko la ardhi vilivyofafanuliwa na Mthamini aliyesajiliwa vinawasilishwa kwa Mthamini Mkuu Ili kupata idhini. Viwango tu vya ardhi vilivyoidhinishwa hutumiwa kwenye uthamini.

[26] Uwiano sawa na Ekari (AE): kipimo cha uzalishaji ulio sawa na ardhi yenye rutuba katika wilaya iliyoguswa na Mradi. Ni uwiano wa nambari mbili: (a) idadi ya ekari ya ardhi ambayo kaya katika wilaya inahitaji kwa ajili ya kujikimu (kwa kuzingatia mazao makuu na kiwango cha upatikanaji katika katika wilaya hiyo, pamoja na wastani maalum wa mavuno ya mazao ya wilaya na wastani saizi ya kaya); na (b) idadi ya wastani wa ekari za ardhi kwa kila kaya kwa wilaya zote zilizoguswa za Mradi (kama ilivyoripotiwa kwenye

Athari	Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
			Fidia ya Vitu na /au Fedha	**Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]**
kupoteza ardhi huathiri ustawi wa maisha AU Upotevu wa kudumu ardhi ya kilimo (mazao) ambapo sehemu ya ardhi iliyotwaliwa na iliyobaki au (iliyobaki kwenye milki ya mguswa) bado inaweza kusaidia shughuli za ustawi				Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa mtu binafsi, kulingana na sababu za mazingira magumu ya mguswa wa mradi - PAP.
		Mmiliki wa kisheria wa ardhi. Mmiliki wa kimila wa ardhi (mtu aliyeguswa na mradi atapoteza >AE LAKINI <[27]AFS) **na mguswa haishi katika**	• Fidia ya fedha (kama unastahili) kwa ardhi iliyopotea kabisa kwa viwango vya soko kama ilivyoelezwa na Mthamini Aliyesajiriwa pamoja na asilimia 10 kwa ajili ya gharama za uhamishaji; na • Msaada katika kuorodhesha umiliki sahihi wa ardhi mbadala ndani ya Kata (ambapo imeombewa na ardhi kutambulishwa na PAP).	**G4** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi unaozingatia ardhi na usiozingatia ardhi;

Takwimu ya Sensa ya Kilimo ya Mwaka 2007/2008). Wastani wa Ukubwa wa Shamba (AFS): Kiwango cha wastani cha kilimo (mazao) cha ardhi kwa kila kaya katika wilaya, kama ilivyoripotiwa Sensa ya kilimo ya 2007/2008 (kwa taarifa Zaidi, rejea kipengele cha 6.4.2.9).

[27] Uwiano sawa na Ekari (AE): kipimo cha uzalishaji ulio sawa na ardhi yenye rutuba katika wilaya iliyoguswa na Mradi. Ni uwiano wa nambari mbili: (a) idadi ya ekari ya ardhi ambayo kaya katika wilaya inahitaji kwa ajili ya kujikimu (kwa kuzingatia mazao makuu na kiwango cha upatikanaji katika katika wilaya hiyo, pamoja na wastani maalum wa mavuno ya mazao ya wilaya na wastani saizi ya kaya); na (b) idadi ya wastani wa ekari za ardhi kwa kila kaya kwa wilaya zote zilizoguswa za Mradi (kama ilivyoripotiwa kwenye

Athari	Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
			Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
maisha[25] au ambapo matumizi ya awali ya ardhi yanaweza kuendelea hata baada ya ujenzi		**mazingira magumu**		
		Mmiliki wa kisheria wa ardhi. Mmiliki wa kimila wa wa ardhi (mguswa atapoteza >ES LAKINI <AFS) na wapo katika mazingira magumu	***Fursa ya kuchangua vitu:*** • Mbadala wa ardhi ilyopotea yenye ukubwa sawa (ilimradi tu ardhi ipo katika kata) yenye kumilikiwa halali kulingana na PS5 • Malipo yote ya gharama zote za manunuzi[28;] • Posho ya usumbufu;[29] na • Posho zingine zinazostahili AU ***Fursa ya kuchagua fedha:*** • Fidia (kama inastahiki) kwa ardhi iliyopotea kabisa katika viwango	**G3** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi unaozingatia ardhi na usiozingatia ardhi; • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha mtu binafsi, kulingana na sababu za mazingira magumu ya mguswa • Pale ambapo mbadala wa ardhi ya kilimo haupatikani katika kata, Mpango wa ziada wa ustawi wa maisha utatolewa kwa mguswa

Takwimu ya Sensa ya Kilimo ya Mwaka 2007/2008). Wastani wa Ukubwa wa Shamba (AFS): Kiwango cha wastani cha kilimo (mazao) cha ardhi kwa kila kaya katika wilaya, kama ilivyoripotiwa Sensa ya kilimo ya 2007/2008

[25] Kuwepo kwa Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha

[28] Kwa ajili ya gharama za manunuzi au usajili, hesabu halisi zitatolewa na serikali za mitaa.

[29] Tanzama sehemu ya 6.4.1.

Athari	Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
			Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
			vya masoko kama ilivyoelezwa na Mthamini Aliyesajiliwa pamoja na asilimia 10 kwa ajili ya gharama ya manunuzi;[30] [31]na • Posho kama ilivyoonyeshwa hapo juu.	

[30] Pale inapowezekana, dhamana italipwa kutoka kwenye malipo ya fidia kwenda kwa taasisi ya kukopesha. Kanuni hii inatumika kwa mali yote ambayo imejumuishwa na dhamana.

[31] Viwango vya soko la ardhi vilivyofafanuliwa na Mthamini aliyesajiliwa vinawasilishwa kwa Mthamini Mkuu ili kupewa idhini. Viwango vya ardhi tu vilivyoidhinishwa hutumiwa kwenye uthamini

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
A5	Upotevu wa kudumu wa ardhi ya kilimo (mazao)	Utwaaji (Upotevu wa kudumu).	Watumiaji waliothibitishwa lakini ambao siyo wamiliki (Ikijumuisha wapangaji wanaotumia ardhi[32]. Watumiaji wasio halali[33]	• Hakuna stahiki ya ardhi	**G5[34]** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi usiozingatia ardhi kama vile Mafunzo ya ujasiliamali na Usimamizi wa fedha na Mafunzo ya Ujasiriamali); na • Ambapo wapangaji wa mguswa wamepoteza >AE na wamejitambua na kuwa na uwezo wa kupata mbadala wa ardhi kwa ajili kulima, wanaweza kufanyiwa mpango wa ustawi wa maisha wa kiwango cha kundi
A6	Upotevu wa kudumu wa ardhi	Utwaaji (upotevu	Mmiliki wa kisheria wa	• Fidia ya fedha kwa ajili ya	**G4**

[32] Hii inatumika kwa ardhi ya mtu binafsi inayomilikiwa au inayomilikiwa na kukodishwa kwa mtu mwingine. Wapangaji huchukuliwa kuwa na riba, lakini sio umiliki wa ardhi chini ya kanuni za jumla za Uthamini na mthamini, 2018. Kwa ardhi ya jamii na na jamii, tazama H5 na H6.

[33] Wakazi wasio rasmi wanayo haki ya mali zao ambazo huchukuliwa kuwa za kudumu au za kipindi kifupi ambazo hazizui maslahi mengine

[34] Wapangaji wa ardhi ambao jumla ya fidia yao ni chini ya T.Shs. 100,000 hawatastahili msaada wa mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	**Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]**
	ya kuchungia	wa kudumu	ardhi Mmilikii wa kimila wa ardhi.	thamani ya ardhi iliyopotea katika thamani ya soko kama ilivyobainishwa na mthamini Aliyesajiliwa pamoja na asilimia 10 kwa ajili ya gharama za uhamishaji fedha na posho stahiki	Mipango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi kwa msingi unaozingatia na usiozingatia ardhi;
A7	Upotevu wa kudumu wa ardhi ya mashamba tupu/ardhi isiyo na kitu.[35]	Utwaaji (upotevu wa kudumu).	Mmiliki wa kisheria wa ardhi Mmiliki wa kimila wa ardhi	• Fidia ya fedha kwa ajili ya ardhi tupu ya shamba/ ardhi katika thamani ya soko pamoja na asilimia 10 kwa ajili ya gharama ya gharama za manunuzi	
Upotevu wa Makazi kwa Mmiliki[36]					
B1	Upotevu wa makazi ya msingi na maeneo mengine ya kuishi kwa ajili ya wake au wanafamilia au	Upotevu wa kudumu wa miundombinu yote au	Mmiliki wa miundombinu na mkazi bila kuzingatia umiliki wa	**Fursa ya kuchagua mbadala wa vitu** • Wamiliki wa miundombinu watapokea mbadala wa nyumba (na miundombinu mingine ya	**G1** ☐ Mipango ya kiwango cha kikundi inayozingatia ardhi au isiyozingatia ardhi kwa ajili ya kuboresha ustawi wa maisha; na ☐ Mpango wa mtu mmoja mmoja wa

[35] Ardhi tupu inamaanisha ardhi ambayo inashikiliwa lakini haijatumika mpaka wakati wa uchunguzi lakini haijatelekezwa.

[36] Waguswa waliomilikishwa wataruhusiwa kwa kutoa kwanza nafasi ya umiliki kwa Mradi kwa kuondoa nyumba zao, na vifaa vingine ikiwa ni pamoja na mali ambazo si za kudumu.

Athari	Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
			Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
ndugu (Kulingana na vigezo) nyumba ziwe zinatumika mara kwa mara pia ziwe zimekamilika wakati wa uthamini[37]	baadhi ambapo inayobakia haiwezi kutumika	makazi kisheria ikiwa ni pamoja na "Hati ya Umiliki"	nyumbani na) iliyo katika usanifu bora uliokubaliwa[38]. Usanifu na ubora huu utatakiwa kukidhi kanuni na viwango vya Tanzania na kuwa mbadala sawa au wenye viwango zaidi ya nyumba za awali • Gharama za manunuzi • Gharama za usafirishaji kwa ajili ya uondoaji wa vitu vya kaya na visivyoweza kutumika tena, kuhamishwa kwenda eneo mbadala. • Posho ya usumbufu • Na posho zingine husika Chaguo la fedha: • Gharama mbadala ya miundombinu yote; • Pale inapokusika makato ya deni	kuboresha kiwango cha ustawi wa maisha. .

[37] Makazi ya ziada na miundo mbinu saidizi ya makazi isiyoweza kuhamishika itatathiminiwa kwa kuzingatia hali ya utumikaji wake na sababu za kitamaduni - rejea kifungu cha 7.3.2 kwa ufafanuzi kamili na muktadha.

[38] Mbadala wa nyumba utatolewa sambamba na choo kimoja cha shimo cha kisasa pamoja na jiko moja.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
				yatafanyika, na kulipwa taasisi za mikipo. • Posho za usumbufu; na • Posho zingine zinazohusika.	
B3	Miundombinu midogo na majengo ya makazi, mazizi, visima, mifumo ya maji taka, stoo, maghala, uzio, baraza, ngazi, Vizimba, njia za kuingilia zisizo za lami, na pamoja na miundombinu mingine kama hiyo ya vyoo ambayo haijakamilika	Upotevu wa wa kudumu wa miundombinu mingine midogo ya majengo ya makazi	Mmiliki wa miundombinu – itambulike kuwa, huyu hawezi kuwa sawa na mmiliki wa kiwanja	• Gharama mbadala ya miundombinu yote, kama haifai kabisa tena; • Miundombinu isiyokamilika itathaminiwa kwa gharama ya Uhamishwaji kwa kuzingatia kiwango cha kukamilika cha miundombinu. • Posho za usumbufu; na usafiri kwa ajili ya uondoaji wa vitu vya nyumbani na vifaa vya ujenzi vinavyoweza kutumika tena na kusafirishwa kwenda eneo mbadala	Haihusiki

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
B4	Miundombinu ya Usafi	Upotevu wa miundombinu ya usafi	wamiliki wa majengo ya makazi, biashara na majengo mengine. Vyombo vya serikali kama wamiliki wa miundo mbinu ya jamii	☐ Gharama mbadala kwa ajili ya miundomibinu au majengo ☐ Posho ya usumbufu na ☐ Posho zingine husika Pale ambapo mguswa atapoteza miundombinu ya makazi (na anastahiki fidia chini ya kategoria B1) Kila mbadala wa nyumba utapewa choo cha shimo cha kisasa. Pale ambapo mguswa anastahili mbadala wa nyumba zaidi ya moja wanaweza kuchagua ama choo kimoja cha shimo cha kisasa (chenye lango la ukuta wa usiri) kwa kila muundo mbinu mbadala; AU • Choo kimoja cha kisasa kilichounganiswa kwa kila kaya	Haihusiki
Upotevu wa vitu vinavyochangia uchumi kwa pesa au mbadala					
G1	Upotevu wa rasilimali zilizokuwa zinapatikana katika jamii kama	Upotevu wa kudumu au wa muda	Watumiaji wa rasilimali au mtu yeyote anayepotez	• Matumizii katika ngazi ya jamii yataendela • Ardhi yoyote ya jamii na mali nyingine zinazosimamiwa na halmashauri za vijiji zilizoguswa	Haihusiki

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
	vile misitu, ardhi oevu na miti isiyo ya kibiashara.	lakini haziathiri utwaaji wa ardhi iliyobakia	a chanzo cha mapato kinachohusiana na ardhi iliyotengwa ikijumuisha watumiaji wa mali asili za msimu IFC PS5 GN 8	moja kwa moja na Mradi zinastahiki kupata fidia ya fedha taslimu ya gharama zote (kulingana na thamani ya soko pamoja na asilimia 10 ya gharama uhamishaji fedha).	
Upotevu wa miundo mbinu au ardhi inayomilikiwa na jamii au taasisi					
H1	Miundo mbinu na/au ardhi inayomilikuwa na jamii au taasisi. Hii ni pamoja na viwanja vya kijamii, ambavyo havikujengwa na serikali, makanisa, misikiti, na maeneo mengine	Upotevu wa kudumu au wa muda).	Mmiliki wa jengo na miundo mbinu.	Kwa ajili ya upotevu wa kudumu: ***Fidia ya fedha taslimu [39]AU Chaguo la fedha:*** • Gharama ya Mbadala wa ardhi na miundo mbinu; • Posho ya usumbufu na • Posho zingine kama inavyostahili ***Upotevu wa muda wa mali****:* • Mradi kusaidia utwaaji wa nafasi	Hakuna

[39]Ardhi / miundombinu inayomilikiwa na serikali, jamii au taasisi binafsi haina sifa ya kupewa fidia ya mbadala wa ardhi/ miundombinu, isipokuwa makanisa na shule ambazo zinakaguliwa kwa kutegemea msingi wa kesi na kesi.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
	ya ibada, masoko, shule za kibinafsi, vituo binafsi vya afya			au ruhusa kulingana swala lenyewe	
H4	Ardhi inayotengwa kwa matumizi ya jamii hasa ya ufugaji inayotumiwa na wafugaji wote.	Upotevu wa muda	Umiliki wa kijamii.	• Fedha taslimu kwa ajili ya thamani ya ardhi iliyotwaliwa kwa kudumu kutegemea bei ya soko na fedha iliyotolewa kwa jamii ya wafugaji (Chombo kitateuliwa na jamii na kama ni ardhi ya kijiji itakuwa halmashauri ya kijiji • Posho kama inavyostahiki na • Ukanda usio na uzio (fensi)	Hakuna.
H5	Ardhi inayotengwa kwa matumizi ya jamii hasa ya ufugaji inayotumiwa na wafugaji wote.	Upotevu wa muda	Umiliki wa kijamii.	• Msaada wa Mradi ili kulinda baadhi ya utwaaji au mpango mdadala wakati wa ujenzi na • Ukanda au upande ambao haujajengewa uzio	Hakuna.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
H6	Barabara, Njia, mifereji na njia gridi ya umeme	Upotevu wa kudumu wa miundo mbinu	Wilaya na serikali za mitaa, jamii au makampuni shiriki.	• Mradi utakuwa na makubaliano ya jumla na mamlaka husika katika kila ukanda wa mkuza kwa ajili ya barabara, umeme na miundo mbinu mingine; • Shughuli yoyote ya Mradi inayohitaji barabara katika jamii itajadiiwa na kukubaliwa na mamlaka husika na kufanywa kulinga na viwago vya usalama vya kitaifa vya ujenzi wa barabara ikiwa ni pamoja na mifereji na alama za usalama za barabarani pale inapohitajika. • Michepuko yoyote na miundombinu kulingana na viwango vya kitaifa; na • Kuweka njia nyingine za kijamii karibu ikiwa zimezibwa na miundombinu ya mradi kulingana na tahimini na upotevu wa njia	Hakuna.
Miti na mazao					

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
I1 & I2	Upotevu wa mazao – ya msimu na ya kudumu[40].	Upotevu wa kudumu au uzuiliwaji wa upatikanaji	Mmiliki wa mazao au miti yenye thamani ya biashara	• Waguswa waliopoteza mazao na miti yenye thamani kiuchumi kulingana na ilivoorodheshwa siku ya uthamini (mfano, waliokuwepo tarehe ya katazo) wanastahili kulipwa fidia ya mazao yaliyopotea kwa kiwango cha ukomavu wa mazao kwa tarehe ya uthamini wa mazao ya miti nyenye thamani kwa kulinganishwa na thamani inayoakisi mwaka wa uthamini mwaka 2018. • Posho ya Usubumbufu na posho zingine stahiki (kulingana na IFC) mazao na miti yanakuwa na marekebisho yanayoongezwa kwenye IFC vya uthamini. Rejea sehemu ya 6.4.2. hapo chini	Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa waguswa ambao ni wamiliki wa ardhi na waliohamishwa kimakazi kama inavyoelezwa hapo katika sehemu A mpaka F Kwa ajili ya wapangaji wa ardhi wanaopoteza mazao na miti ambapo hakuna upotevu wa ardhi au makazi: Thamani ya fidia ikiwa ni shilingi za Kitanzania 100,000/= au Zaidi, vifuatavyo vitatumika: **G6** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa msingi wa ardhi au kwa kuzingatia msingi wa ardhi (mfano; Usimamizi wa fedha, mafunzo ya ujasiliamili, mpango wa ufugaji wa wanyama, nyuki); na • Mpango wa ustawi wa maisha utaenda sanjari na mali iliyopotea.
I3	Upotevu wa mazao – Ya msimu na ya kudumu .	Upotezaji wa kudumu au uzuiliwaji wa upatikanaji	Mkulima mpangaji		
I4 & I5	Upotevu wa miti ya matunda yenye thamani kiuchumi ambayo ni pamoja na miti ya	Upotezaji wa kudumu au uzuiliwaji wa	Mmiliki wa miti, Mtumiaji wa miti / mpangaji		

[40] Bomba litagusa pori la akiba la Biharamulo, hifadhi ya taifa ya msitu wa Minziro na msitu wa akiba wa mto Ruiga. Imethibitishwa kuwa zote zilizotajwa ziko chini ya mamlaka ya Wakala wa huduma za misitu Tanzania (TFS). Misitu ya serikali imetathminiwa kutumia njia ya mirabaha kwa sababu misitu ya asili haiuzwi.

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
	matunda na mbao.	upatikanaji	mmiliki		Wapangaji wa mguswa amabao watapoteza >AE za mazao / na miti lakini hawakupata fidia ya adhi)
I6	Upotevu wa miti ya matunda au mbao.	Upotevu wa kudumu au kuzuiliwa kwa upatikanaji	Umiliki wa kijamii au kijiji		**G5** • Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha kundi unaozingatia msingi wa ardhi na usiozingatia msingi ya ardhi na Mfano; Usimamizi wa fedha na mafunzo ya ujasiriamali). Programu za kurejesha ustawi wa jamii katika ngazi za vikundi - Ambapo wapangaji wanaoguswa na mradi wamepoteza >AE na wana nafasi ya kupata ardhi mbadala kwa ajili ya kilimo
I7	Upotevu wa mali za kilimo	Upotevu wa kudumu.	Mmiliki asiye rasmi wa mazao na miti	• Kama ilivyo katika 11 na 16, ilivoelezwa kipengele kwa kipengele kuhakikisha Watu Wanaoguswa na Mradi (PAPs) hawabaki katika umasikini kwa sababu ya uhamishaji wa watu na makazi unaotokana na Mradi.	
Mali za kiutamaduni					
J2	Makaburi	Kudumu	Mtu binafsi au vikundi vilivyowasilisha	• Uhamishaji au ujengeaji wa makaburi kwa mashauriano na walalamikaji au wawakilishi wao. (Mradi umeandaa Utaratibu wa	Haihusiki

Athari	Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
			Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
	malalamiko kuhusu makaburi		Uhamishaji wa makaburi. Maafisa wa Manispaa / Wilaya na afya husika wanatarajiwa kusimamia uondoaji wa makaburi kulingana na kanuni za afya. Utafuata taratibu za sheria); na • Fidia zitaenda sambamba na gharama zilizotumika wakati wa uhamishaji, usafirishaji na kuzika upya na urejeshaji upya wa maandishi na ibada za faraja au sherehe zingine[41].	
Watu na vikundi katika mazingira magumu				

[41] Tazama sehemu ya 6.4.1.9

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[1819]
K1	Mpango wa ziada wa msaada wa kijamii kwa watu walio katika mazingira magumu wenye stahiki ya faida yoyote hapo juu	Upotevu wa kudumu au wa muda	Kaya ambazo zitahamishwa au uchumi wake umezorotes hwa na Mradi. Kaya itatambuliwa kuwa yenye uwezekano kuwa katika mazingira magumu kutegemea vigezo vilivyoelezwa katika sehemu ya 6.4.2	• Msaada uliotayarishwa kulingana na tathimini kwa msingi wa kila tatizo au swala kuhakikisha kuwa watu wanaoishi katika mazingira hatarishi wanapata fidia na ulinzi uliokusudiwa kulinga na kanuni za RAP. • Msaada wa kisheria, kifedha, na vitu halisi kama ilivoamuliwa kufanyika katika kila swala	Ushiriki katika mipango husika ya urejeshaji wa ustawi wa maisha kama ilivyoelezewa katika kifungu cha 6.4.2 na 8 hapo chini, mfano; kulingana na umuhimu wa athari za Mradi na sababu za mazingira magumu za waguswa: Kuwekwa kwenye mpango wa urejeshaji wa maisha wa kiwango cha kikundi unaozingatia msingi wa ardhi na usiozingatia msingi wa ardhi na (kama inavyofaa) Mipango ya urejeshaji wa maisha wa kiwango cha mtu binafsi
Mpito wa kiuchumi					

Athari		Madhara	Mguswa Mwenye Haki	Haki	
				Fidia ya Vitu na /au Fedha	Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha[18][19]
L1	Fedha nyingi za mkupuo	Uwezo mdogo wa kaya wa kutunza hela za mkupuo na matumizi mabaya ya fedha kwa kununua vitu ambavyo havikukusudiwa	Watu wote waliopokea fidia ya fedha walibainishwa kupitia sensa ya mwisho	• Msaada wa kufungua akaunti za benki[42]	Mafunzo ya usimamizi wa fedha yatatolewa (ambayo yatashabihiana na kiasi cha fedha ya fidia)

[42] Kwa malipo ya fidia kidogo sana, Mradi unakagua njia zingine za malipo kwa utoaji salama wa fedha hizo kwa waguswa. Hizi ni pamoja na fidia za waguswa ambazo jumla ya thamani ya fidia ni shilingi za Kitanzania 100,000/=. lakini, kiwango cha malipo ya 'fidia ndogo sana' kinategemea uchambuzi na mjadala unaoendelea na wadau muhimu wa benki.

6.4 UTHAMINI NA FIDIA

Kama ilivyoelezwa katika sura ya 3, Mradi unatakiwa kukidhi matakwa ya sheria ya Tanzania ya utwaaji wa ardhi, fidia na uhamishaji watu na makazi na viwango husika vya fedha vya Kimataifa - IFS, ni pamoja na Viwango vya Utendaji vya namba 5 na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa (PS5 IFC) vya utwaaji wa ardhi na uhamishaji watu na makazi usio wa hiari. Kwa kutimiza masharti haya, mchakato wa uthamini umekamilika katika maeneo yafuatayo:

- ☐ **Taarifa ya viwango**. Chini ya vifungu vya kanuni za uthamini na wathamini, katika mwongozo wa jumla wa kanuni wa, 2018, Kampuni ya Whiteknights (wathamini waliosajiliwa na Mradi) walifanya utafiti wa bei ya soko katika mkoa wa Kagera. Utafiti huo ulilenga kuainisha viwango vya bei vilivyopo sokoni na gharama mbadala ya vitu. Whiteknights waliandaa na kuwasilisha Ripoti ya Viwango (Whiteknights, 2018) kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuidhinisha akielezea kwa muhtasari matokeo ya utafiti ikiwa ni pamoja na viwango vilivyopitishwa na Mradi katika mkoa wa Kagera. Hatua hii ni muhimu inayohitajika na matakwa ya kanuni na miongozo kuhakikisha kuwa waguswa wanalipwa fidia kwa gharama mbadala zilizopo sokoni.
- ☐ **Uthamini na Fidia Chini ya Sheria ya Tanzania**. Ripoti hii inafafanua mambo yanayostahili fidia chini ya mfumo wa sheria ya nchi; inaelezwa kama fidia ya fedha; na imewasilishwa kwa ajili ya kusainiwa na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu. Utiaji saini na uidhinishwaji wa Ripoti za Uthamini, na Jedwali la Fidia chini ya Sheria ya Tanzania utazingatia matakwa ya kanuni za uthamini ya mwaka, 2018. Kwa ujumla muhtasari wa mchakato wa uthamini, ni muhimu kwa kuwa ripoti hii ya uthamini inasomwa pamoja na ripoti ya uthamini inayoelezea stahiki za ziada na vitu chini ya IFC.
- ☐ **Uthamini wa Stahiki za Ziada Kulingana na Matakwa ya Viwango vya Kifedha vya Kimataifa (IFS)**. Ripoti hii imeelezea stahiki na haki kwa fidia mbadala kama vile ardhi mbadala, nyumba mbadala, urejeshaji wa ustawi wa maisha na msaada kwa watu walio katika mazingira magumu. Haya yanahitajika ili kuhakikisha kuwa jedwali la fidia linakidhi mahitaji na matakwa ya ziada ya IFC. Ripoti hizi zimewasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu, kwa lengo la kumfahamisha na sio kuidhinishwa na kwani zina gharama za stahiki na fidia za ziada kulingana na vigezo vya Mradi na matakwa ya IFC.

6.4.1. Uthamini na Fidia Chini ya Sheria ya Tanzania

- ☐ Ili kuamua viwango vya fidia Kampuni ya Whiteknights walikamilisha zoezi[43] la uthamini na kukokotoa thamani ya vipande vya ardhi iliyoendelezwa/na mali zilizoathiriwa na ukanda wa mkuza katika Mkoa wa Kagera na hasa wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba, na Biharamulo

Mchakato wa uthamini ulizingatia mambo yafuatayo:

- ☐ Viwango vilivyotolewa na Mkaguzi Mkuu[44];
- ☐ Sheria husika
- ☐ Taarifa zilizopatikana katika maeneo husika zimeonyeshwa kwa muhtasari katika sehemu ya 4.3 pamoja na viwango vya soko; na
- ☐ Mchakato wa uthibitishaji kwa kushirikiana na Mthamini wa Wilaya husika.

Viwango vilivyotolewa na Mthamini Mkuu ni pamoja na viwango vya fidia ya:

- ☐ Ardhi[45] ; na
- ☐ Mazao ya miti ya biashara [46].

Wakati wa mchakato wa uthamini, viwango vilibadilishwa kulingana na maoni ya kitaalamu ya mthamini aliyesajiliwa ambaye alizingatia sababu mahususi za kimaeneo na uchunguzi. Viwango vilivyokubalika hatimaye vilithibitishwa na Mthamini wa Wilaya husika kabla ya kuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mchakato wa kuweka viwango vya fidia za Mradi ulianza mnamo mwaka 2017 wakati viwango vya fidia vilipoamriwa kwa ajili ya maeneo ya awali. Hii ilijumuisha pamoja na

[43] Mchakato huu umebainishwa katika Sheria ya bunge ya Ardhi Namba 4 ya 1999, Sheria ya Bunge ya Ardhi ya Vijiji Nambari 5 ya 1999, Sheria ya Bunge ya Utwaaji wa Ardhi ya 1967, Sheria za Ardhi za 2001, Sheria za Ardhi (Madai ya Fidia) 2001, Sheria ya Uthamini na mthamini 2016, Sheria ya Uthamini na mthamini ya (Jumla) Kanuni za 2018, na Sheria ya uondoaji makaburi (Utoaji) wa 1969.

[44] Viwango vya msingi vya ardhi ni ishara, hata hivyo, viwango vya mazao na miti na viwango vya ziada vilivyoidhinishwa kwa Mradi ni maagizo ya kanuni

[45] Viwango vya ardhi huchapishwa kila wakati na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHSD) na ni msingi wa uchunguzi wa kitaifa wa viwango vya ardhi ambao unazingatia mambo kama eneo na ufikiaji. Viwango vya msingi wa ardhi ni maalum kwa mikoa, wilaya na kata.

[46] Viwango vya mazao na miti ya uchumi pia huchapishwa kila mara na MLHHSD kwa kushauriana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

kutembelea maeneo husika na warsha zilizohudhuriwa DWC, wathamini wa serikali kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi MLHHSD na wathamini waliosajiliwa (RV) Viwango vya uthamini kwenye Maeneo ya Mradi viliidhinishwa na Mthamini Mkuu (CV) mnamo tarehe 11 Aprili, 2018. Mchakato huu ulilenga katika kutoa viwango vya maeneo ya kipaumbele (PA) katika Ripoti ya Uthamini na kutoa taarifa muhimu zinazohusu uthamini wa maeneo ya mkuza wa bomba.

Mchakato wa kuamua viwango vya fidia kwa ukanda wa mkuza ulihusisha uchunguzi wa thamani ya soko katika eneo lote la mkuza. Utafiti huo ulifanywa na wathamini waliothibitishwa kisheria kati ya Mei 16 na 20 Septemba 2018 na ulilenga kuweka viwango vya fidia vinavyolingana na bei ya soko ya:

- ☐ Ardhi;
- ☐ Gharama za umiliki wa ardhi;
- ☐ Majengo na miundombinu;
- ☐ Mazao na miti;
- ☐ Miti ya asili;
- ☐ Posho ya usumbufu;
- ☐ Posho ya Malazi (kukodisha);
- ☐ Gharama za usafiri;
- ☐ Upotevu wa faida; na
- ☐ Makaburi.

Timu ya wathamini wakuu kutoka Kampuni ya Whiteknights walitembelea maeneo mbalimbali yaliyoathiriwa na Mradi katika wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo ili kushauriana na kuthibisha viwango vilivyowekwa na Mkaguzi wa Wilaya. Kampuni ya Whiteknights ilifanya majumuisho ya viwango vya fidia katika mkoa wa Kagera ambavyo viliwasilishwa na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu.

Ardhi[47]

Seti za itifaki ya kuamua thamani ya soko la ardhi ambayo iko katika eneo lililoathiriwa na Mradi zilipitishwa. Vizio vya Viwango vya ardhi viliwekwa kwa kutumia Vizio msingi vya Ardhi vya mwaka 2016 kutoka katika ofisi ya Mkaguzi Mkuu na kupitia tafiti zingine

[47] Gharama za nyongeza za ugawanyaji wa majina ya wamiliki, pamoja na upimaji, kwa sababu ya matokeo ya mchakato wa ununuzi wa ardhi kwa mkuza wa bomba utashughulikiwa wakati wa utekelezaji wa RAP na kwa gharama ya Mradi.

mahususi zinazohusiana na Mradi[48]. Viwango vya Ardhi vya mwaka 2016 vinaelezea thamani ya ardhi katika ngazi za kata na vijiji. Baadaye, mashauriano yalifanywa na mthamini wa wilaya baada ya kutembelea eneo la Mradi kujua hali halisi ya thamani ya ardhi husika. Taarifa kutoka kwa mthamini wa wilaya ililinganishwa na uchunguzi wa bei ya soko uliofanywa na mamlaka za vijiji kuhusu thamani ya ndani ya ardhi. Utafiti wa soko ulijumuisha taarifa za bei ya ekari moja kwa ardhi ambayo haijaendelezwa na kukagua mauzo halisi ya ardhi kwa ajili ya kilimo yaliyofanyika hivi karibuni katika kijiji husika.

Takwimu juu ya viwango vya ardhi ya vijiji ziliunganishwa ili kupata thamani ya soko kwa kiwango cha kata. Michakato hii ya mashauriano na utafiti wa soko iliwezesha kampuni ya Whiteknights kujua Viwango vya Ardhi vinavyotumika katika Soko kwa kata mbalimbali ambazo zitaathiriwa na mkuza wa bomba na utandazaji wa bomba la Mradi[49] kwenye Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo.

Kwa kuzingatia kanuni 8, 9 na 55 (4) ya uthamini, 2018, mbinu linganifu ya uthamini ilitumiwa kupata viwango vya thamani ya ardhi kutokana na shughuli halisi za ardhi zinazofanywa katika vijiji na kata husika katika wilaya ya Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo. Viwango vya Ardhi vilivyowasilishwa kwa Mthamini Mkuu kutoka kata za wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo vimewasilishwa katika Jedwali 6-2.

[48] Utafiti wa Viwango vya Thamani ya Ardhi uliofanywa kando ya mkuza wa bomba ulipitisha njia ya utafiti uliochanganywa kwa kutumia njia ya uchukuzi ambapo hesabu zilifanywa. Mchanganuo huu wa takwimu uliimarishwa kwa njia ya ubora ambayo iliwekwa msingi wa hoja za kujitolea. Kwa habari zaidi angalia Kiambatisho B. Mussa, sina uhakika nah ii tafrisi tafadhali ipitie upya

[49] Kambi namba 05 (MCPY-5) iliyoko kata ya Kyaka na kaambi namba 06 (MCPY-06) iliyoko kata ya Karambi, zitajengwa kama sehemu ya ujenzi wa awali ili kusaidia kazi za ujenzi wa bomba.

Table 0-1: Viwango vya Ardhi kwa kata za Halmashauri husika za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo [50]

Mkoa	Wilaya	Kata	Kiwango kwa Ekari kwa Ardhi ya Kilimo (Shs.)
KAGERA	Missenyi	Mtukula	1 800 000
		Nsunga	800 000
		Kasambya	1 000 000
		Kyaka	1 000 000
		Kilimilile	700 000
	Bukoba	Kyamulaile	700 000
		Mugajwale	650 000
		Kyaitoke	650 000
		Izimbya	650 000
		Kibirizi	500 000
		Rukoma	700 000
	Muleba	Ngenge	600 000
		Mubunda	650 000
		Kasharunga	800 000
		Karambi	800 000
		Kyebitembe	750 000
		Bisheke	650 000
		Burungura	600 000
	Biharamulo	Nyarubungo	600 000
		Nyamigogo	800 000

[50] Land rates in accordance with the Market Survey for Compensation Rates Report – (Nov 2018). This was submitted for approval to the CV by WK and approved in May 2019.

Kipande kidogo kilichobaki katika ardhi iliyoguswa (Ardhi yatima)

Ardhi yatima (ardhi isiyoguswa na Mradi) ni kipande cha ardhi ambacho hakijakumbwa na athari za Mradi na pia kinatambulika kuwa ni eneo lisilo na manufaa ya kiuchumi. Ardhi hii ilitambuliwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- ☐ Ikiwa asilimia 20 au chini ya hapo ya sehemu ya kipande cha ardhi cha mguswa itabaki bila kuathiriwa na Mradi, pendekezo litafanyika la kutwaa ardhi hiyo (iwapo tu mmiliki wa ardhi yupo tayari kuiachia).
- ☐ Vipande vya ardhi chini ya nusu ekari (0.5) ambavyo viko nje ya mipaka ya kiutawala ya jiji, manispaa, au miji itachukuliwa kulingana na Sheria ya Bunge ya Utwaaji Ardhi ya mwaka 1967 chini ya kifungu cha 10 ambayo inaainisha kuwa kiasi cha nusu ekari (0.5) ndiyo kiwango cha mwisho cha ukubwa wa ardhi isiyoguswa na Mradi inayoruhusiwa na sheria ya Tanzania.

Majengo na Miundombinu

Mbinu ya uthamini wa gharama mbadala (Contractor's Test Method of Valuation) imetumika katika uthamini wa majengo na miundombinu. Hii inaambatana na kanuni ya 55 (3), ambayo inahitaji mthamini, katika kupima viwango vya gharama za ujenzi (miundombinu), azingatie gharama za ufidiaji wa majengo au miundombinu inayofanana na hiyo, ubora wa viwango vya ujenzi wa kukamilisha kazi - inayoendelea, na ukubwa kulingana na bei ya soko la ndani la vifaa na malipo ya kazi.

Katika uthamini wa mali wakati wa ujenzi wa mkuza, aina kuu nne (4) za viwango vya ujenzi /miundombinu zilitambuliwa na kutumika:

Kwanza, aina za Viwango vya ujenzi vya jumla, ya aina za majengo yanayofanana au yenye muundo unaofanana na yaliyojegwa kwa kutumia malighafi za ujenzi zinazofanana, ubora, na ustadi wa utenda kazi. Aina saba za majengo ziliorodheshwa (kutumia nambari BA hadi BF) kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho B).

Aina za viwango tofauti vinavyotumika kwa kategoria tofauti za miundombinu na vifaa vya ujenzi ambavyo vinaonyeshwa katika Kiambatisho B: Muhtasari wa Viwango vilivyowasilishwa kwa Mthamini Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa (Desemba 2018) hutambuliwa kwa msimbo/alama kama vile BA.1 au BE.4 n.k, vyote kwa pamoja hukamilisha asilimia100 ya aina za viwango vya bei. Vile vile, kuna miundombinu au uendelezaji mwingine wa ardhi kama vile: uzio, mpaka au ukuta, mitaro, turubai nk,

ambapo vizio vyake vipo katika mita na hutumia viwango hivyo hivyo. Kwa aina hii ya miundombinu, pia viwango vya ujenzi vinavyotumika vimekategorishwa na kupewa misimbo kama SI.1 au SJ.2 au SK.3 nk.

Pili, kuna seti ya viwango ambazo kimoja kimoja zimerekebishwa kutoka katika kategoria ya viwango vya ujenzi kwa majengo/miundombinu vilivyoorodheshwa hapo juu. Viwango hivi vinatumika kwa majengo/miundombinu ambayo vinginevyo miundombinu hiyo ingewekwa katika mojawapo ya kategoria ya viwango vya ujenzi vilivyoainishwa hapo juu, lakini miundombinu au majengo hayo yalikuwa katika hali ya kutokamilika wakati uthamini na/au kukosa baadhi ya vitu vya kimuundo. Marekebisho ya viwango hivi yamefikiwa kwa ajili ya kupunguza gharama/thamani ili kuweka uhusiano unaofaa na kiwango kamili kilichopendekezwa (msimbo B au S kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho B), kilichoonyeshwa kama asilimia, ya kategoria ya Kiwango cha ujenzi. Kwa mfano, pale ambapo kiwango kilichorekebishwa ni asilimia 75 ya Bei ya kategoria ya kiwango cha ujenzi BE.4 jengo au muundombinu utakuwa na asilimia 25 pungufu ili kufikia hatua tarajiwa za ukamilishaji kwa kuzingatia thamani ya nguvu kazi iliyotumika wakati wa uthamini, ambao ungekuwa umekamilika kwa aslimia 100.

Tatu, kuna Viwango sambamba vya ujenzi vinavyochukuliwa kama vizio kamili vya gharama, vinavyotumika kwenye miundombinu ambayo ni midogo, rahisi na yenye gharama au thamani ya chini. Viwango hivi vimegawanywa katika makundi mahususi ya gharama au thamani ndogo, kwa ujumla vinagawanywa kulingana na ukubwa, saizi ya kati na ndogo. Kwa kawaida viwango hivi hutumika kwa miundombinu sahili na midogo kama vile majiko, vyoo au vyoo vya shimo, mabanda ya wanyama/boma/zizi, mabanda ya kuku, visima, mabwawa, bafu, nk. Viwango sambamba vya ujenzi huzingatia matumizi au madhumuni ya muundombinu, ni kwa kiasi gani miundombinu husika ni ya muhimu, viwango vya ujenzi, vifaa vilivyotumika na saizi (kubwa, kati au ndogo).

Nne, miundombinu ambayo ni ya kipekee kulingana na vifaa vya ujenzi, umbo au mtindo na kwamba hauhusiani na kategoria nyingine zozote zilizoelezewa hapo awali. Miundombinu hii inahitaji mbinu tofauti ya uthamini, ambayo hupelekea gharama kulingana na vifaa vya ujenzi na nguvu kazi inayotumika, kama inavyoonyeshwa katika saizi ya jengo au muundombinu, mtindo na viwango vya ujenzi. Kwa mtazamo huu, kila jengo au muundombinu unashughulikiwa na kuthaminiwa kipekee kwa kutegemea kiwango cha ujenzi ambacho ni tofauti na mahususi kwa jengo au muundombinu husika.

Viwango vya ujenzi wa majengo na miundombinu vimeonyeshwa katika Kiambatisho B: Muhtasari wa Viwango vilivyoidhinishwa na Mthamini Mkuu (vilikusanywa Novemba 2018 na kuidhinishawa Mei, 2019).

Mazao na Miti

Thamani ya soko la mazao na miti inategemea aina ya mazao/miti, umri na hatua ya ukuaji na idadi ya mazao au mti fulani. Timu ya wathamini ilitumia Viwango vya Mazao ya Kanda ya Kaskazini, 2012 iliyotolewa na Mthamini Mkuu.

Awali "mazao na miti" ambayo haikuwa imeorodheshwa (ambayo haiko kwenye Kiwango cha Mazao ya Kanda ya ziwa, 2012) inapatikana katika orodha ya viwango vya fidia vilivyoidhinishwa (yasiyotangazwa rasmi kwenye gazeti la serikali) kwa mazao na miti ya ziada iliyotolewa na Mthamini Mkuu kwa Mradi mnamo Agosti, 2018[51].

Viwango vya fidia kwa mazao na miti kama hiyo inategemea ama: i) viwango vya fidia vilivyopendekezwa ambavyo vilitolewa kwa Kampuni ya Whiteknights na Wathamini wa Wilaya au; ii) makadirio ya viwango vya fidia kwa miti na mazao yaliyofanyika kwa kuzingatia viwango vya fidia vya aina ya mazao na miti inayopatikana katika jedwali la fidia la mwaka 2012 na kusababisha kupanda kwa viwango vya bei kati ya mwaka 2012 na 2018[52].

Viwango vya mazao ya Kanda ya Ziwa, 2012 na viwango vilivyopitishwa baadae vimeonyeshwa katika Kiambatisho B. Muhtasari uliidhinishwa na Mthamini mkuu (vilikusanywa Novemba 2018 na kuidhinishawa Mei, 2019).

[51] Rejea Barua Kumbukumbu Nambari: BA.391 / 466/01/58 ya tarehe 15 Agosti 2018.

[52] Kiwango chakilimo cha mazao mseto huhesabiwa kwa msingi wa dhana kwamba kilimo cha mseto cha mazao anuwai kimesambazwa kwa usawa katika kipande cha ardhi. Kufikia kiwango cha mazao mseto, kwa kila moja ya zao, kiwango cha fidia kwa mmea mmoja huzidishwa na eneo lililopimwa la mazao na kiwango cha ukomavu wa mmea. Viwango vinavyotokana na zao moja huongezwa baadaye na jumla ya viwango hugawanywa na eneo lililojumuishwa kwa jumla kufikia kiwango cha ekari cha mazao mseto. Pale tu ambapo eneo lililojumuishwa la mazao mseto linapatikana, kiwango cha mazao mseto huhesabiwa kulingana na dhana ya uzani sawa wa maeneo ya mazao maeto

Posho za Usumbufu

Kifungu cha 15 cha kanuni ya Uthamini na Wathamini (jumla), Kanuni za mwaka 2018 kinaelekeza posho za usumbufu kukokotolewa kwa “kuzidisha thamani ya riba ya ardhi kwa kiwango cha wastani cha asilimia ya riba iliyotolewa na Benki Kuu kwa amana za kudumu kwa miezi 12 kwa wakati wa upotezaji wa riba katika ardhi”.

Taarifa iliyotolewa na Benki ya Tanzania ilionyesha kuwa Benki Kuu haitoi riba juu ya akiba ya amana zilizohifadhiwa badala yake hutoa taarifa kuhusiana na viwango vya riba inavyotoza kwa mabenki ya biashara yanapokopa benki kuu au wakati wawekezaji wanapouza hati fungani zao kwa benki kuu. Viwango hivi vinajulikana kama viwango vya punguzo. Kiwango cha punguzo kilichopo kwa sasa ni asilimia 7 ambacho kilianza kutumika kutoka Agosti 2018.

Kwa kuzingatia tofauti iliopo baina ya Kanuni ya Uthamini na Wathamini (Jumla) ya 2018 na amana zilizotolewa na Benki Kuu, mashauriano yalifanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHSD). Kufuatia mashauriano haya kiwango cha riba cha saba (7%) kilipitishwa kwa ajili ya uthamini wa mkuza wa njia ya bomba na miundombinu ya juu kwa Mradi.

Posho ya Malazi

Posho ya malazi ni malipo ya kodi inayotozwa kwa jengo kwa muda wa miezi 36 kwa mujibu wa kanuni ya 13 ya Nyongeza Na. 11, 2018 Sheria ndogo ya Bunge ya uthamini ya mwaka, 2016. Chini ya kanuni ya 12 (2) ya kanuni za uthamini, 2018, mmiliki wa mali atakuwa na haki ya posho ya malazi, pale tu wakati nyumba iliyojengwa kwenye ardhi yake inatumika wakati wa uthamini. Viwango vya kodi vya kila mwezi vya soko vimetolewa katika Kiambatisho B. (vilikusanywa Novemba 2018 na kuidhinishawa Mei, 2019).

Gharama za Usafiri

Gharama za Usafiri zinakokotolewa kwa kuzingatia gharama halisi za kusafirisha tani 12 za mizigo kwa njia ya reli au barabara iliyo ndani ya kilomita 20 kutoka mahali pa kuhamishwa kama ilivyo katika kanuni ya 16 ya Nyongeza ya 11, 2018 Sheria ndogo ya Bunge ya uthamini ya mwaka, 2016. Hii imekokotolewa kwa kiwango cha Shilingi Laki tatu za Kitanzania (Shs 300,000/=). Chini ya kanuni ya 12 (2) ya kanuni ya

uthamini, 2018, mmiliki wa mali atakuwa na haki ya posho tu wakati nyumba iliyojengwa kwenye ardhi yake inatumika wakati wa uthamini[53].

Upungufu wa Faida

Upungufu wa Faida unatathiminiwa kwa kukokotoa faida ya jumla kwa mwezi iliyothibitishwa na akaunti zilizokaguliwa pale inapohitajika au faida iliyothibitishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuzidisha mara 36 (yaani; Upungufu wa Faida = Faida ya jumla / mwezi x 36). Hakuna upungufu wa stahiki wa biashara au mali inayohusiana na biashara iliyopo katika mkuza wa njia ya bomba au katika maeneo ya miundombinu ya juu ya bomba katika wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo, kwa hivyo, kwa uthamini huu, kipengele hiki hakihusiani.

Makaburi

Viwango vya fidia kwa kaburi vilikadiriwa kulingana na mahitaji ya Sheria ya Bunge ya (Kuondoa) Makaburi, 1969. Sehemu ya 9 ya Sheria ya Bunge ambayo inasema:

> "*Fidia inayolipwa chini ya kifungu hiki itafanyika tu kwa matumizi ya msingi yaliyotumika kwa uondoaji, usafirishaji, kurejesha eneo katika hali ya kawaida, maelezo ya kumbukumbu na uzikaji upya wa kaburi au mwili na ibada zozote za mazishi au sherehe nyingine inayoambatana na kuondolewa na kuzika tena".*

Kwa kuzingatia hayo, Kampuni ya Whiteknights iliandaa makisio ya gharama zinazohusiana na kuondolewa kwa kaburi na kuzikwa upya, kwa kutegemea kaburi kama limejengewa au halijajengewa. Kwa ujumla, kiasi kinacholipwa kwa familia kwa ajili ya "ibada za mazishi au gharama za ufariji au sherehe nyingine inayoambatana na kuondoa na kuzika upya" ni T.Shs. 300,000/=. Zaidi ya hapo, kiasi ambacho kingelipwa kwa Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) au Mkandarasi ambaye angeshirikiana na Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) ni T.Shs. 200,000/= kwa kila kaburi kwa kaburi la kawaida. Kwa kaburi lililojengewa nyongeza ya Tshs. 200,000/= inatumika kujenga kaburi, na kufanya bajeti yote ya kuondolewa kwa kaburi kuwa jumla ya Sh. 400,000/=, ukiondoa T.Sh. 300,000/= ambayo hulipwa kwa familia ya marehemu au mwangalizi wa kaburi.

[53] Kifugu cha 12 (2) cha Kanuni ya Uthamini na Mthamini (Jumla), 2018.

Ardhi na Mali za Serikali

Ardhi na mali zinazohusiana na Vijiji Zinasimamiwa na Halmashauri ya Kijiji / Mtaa.

Ardhi na mali inayohusika na vijiji inasimamiwa na halmashauri ya kijiji/mtaa imekadiriwa kulingana na utaratibu wa uthamini ilivyoainishwa katika sheria za Tanzania na kuorodheshwa tofauti katika Ripoti ya uthamini.

Ardhi na Mali Nyingine zinazohusiana na Serikali.

Ardhi na Mali Nyingine zinazohusiana na Serikali zimethaminiwa kulingana na utaratibu wa uthamini ulivyoainishwa katika Sheria ya Tanzania (mfano ardhi katika viwango vya soko vilivyotafitiwa na wathamini wa Mradi na kukubalika kwa Mthamini Mkuu), na kuorodheshwa tofauti katika Ripoti ya Uthamini, kama kumbukumbu ya ukubwa na thamani ya ardhi na mali zilizoguswa na Mradi.

6.4.2 Uthamini wa Fidia Kwa Haki za Ziada kwa Mujibu wa IFC

Ripoti za Uthamini haki za nyongeza chini ya IFC na majedwali mengine ya fidia husiani yanajumuisha uthamini wa haki za ziada, vigezo vya stahiki vya fidia ya vitu (kama urejeshaji wa Ustawi wa Maisha , nyumba mbadala nk) na fursa za fidia ziliendelezwa ili kukidhi viwango hivi. Wakati mambo haya yote yanapozingatiwa na mthamini mkuu, haikusudiwi kwamba yote yataidhinishwa na mthamini mkuu kwa kuwa yanajumuisha haki mahususi za ziada za Mradi na chaguo la fidia, kulingana na matakwa ya IFC.

Hii inajumuisha vipengele vifuatavyo ambavyo vimefafanuliwa zaidi:

- ☐ Asilimia kumi (10%) gharama ya manunuzi kwa thamani ya bei ya ardhi[54];
- ☐ Kiwango cha mfumuko wa bei wa asilimia 45.44 kwa mazao na miti yenye thamani ya kutumia jedwali la viwango vya mazao[55] la mwaka 2012;
- ☐ Posho ya usumbufu wa asilimia 7 (7%) kwa vitu vyote vya fidia haki za ziada [56];
- ☐ Kipande kidogo kilichobaki katika ardhi iliyoguswa (ardhi yatima);

[54] Gharama ya 10% ya mchakato inatumika kwa thamani ya ardhi kama ilivyoamuliwa chini ya Sheria ya Tanzania.

[55] Orodha ya Viwango vya Mazao ya mwaka 2012 hutolewa na Serikali ya Tanzania.

[56] Kiwango cha (asilimia 7) cha riba kinachotumiwa kwa Idhini ya Usumbufu ni kama ilivyo Ripoti ya Tathimini ya Tanzania. Kama ilivyo kwa Sheria ya Tanzania kiwango hiki cha riba kinatumika kwa ardhi yoyote / mali / vitu vya ziada vilivyotolewa chini ya viwango vya Kampuni ya Kiataifa ya Fedha (IFC).

- Mali (yaani mazao na miti) yaliyopo ndani ya hifadhi ya barabara, njia ya gridi ya umeme nk (vilivyothibitika na si vya kufikirika na vinapokidhi vigezo vya stahiki viliyotolewa hapa chini);
- Stahiki za urejeshaji wa ustawi wa maisha;
- Stahiki kwa Watu/Kaya wanaoishi katika mazingira magumu Walioguswa na mradi (hii inahusisha msaada na sio fidia ya nyongeza ya fedha);
- Chaguo la Fidia ya ardhi na nyumba mbadala kwa waguswa wanaostahili; na
- Ardhi na mali mahususi zisizostahiki chini ya sheria ya Tanzania lakini zinazostahiki chini ya IFC.

Gharama za Manunuzi Zinazohusishwa na Ardhi

IFC PS5 inaeleza hasara ya mali kulipwa fidia kwa gharama mbadala. PS5 inafafanua gharama mbadala kama "Thamani ya Uuzaji wa mali pamoja na gharama ya manunuzi". Thamani ya soko ni thamani inayohitajika kuiwezesha jamii au watu walioguswa kubadilisha mali zilizopotea na mali zenye thamani sawa. Gharama ya ununuzi wa 10% inayohusiana na ardhi inayopatikana italipwa fidia chini ya IFS na iko ndani ya Ripoti ya Uthamini kwa Haki za ziada chini ya IFS.

Jedwalila 6 - 3: Viwango vya Ardhi na Gharama za Ununuzi kwa Kata Husika katika Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo

Mkoa	Wilaya	Kata	Kiwango kwa Kila Eneo la Mita za Mraba kwa Viwanja vya Ujenzi (Shs.)	Kiwango kwa Ekari Moja kwa Ardhi ya Kilimo (Shs.)	10% Gharama ya Manunuzi (Shs.)	Viwango kwa Kila Ekari ya Ardhi ya Kilimo Pamoja na Gharama ya Ununuzi (Sh.)[57]
Kager	Missenyi	Mtukula	Haihusiki	800 000	80 000	880 000

[57] Kiasi hicho kinawakilisha Thamani ya Soko la ardhi pamoja na gharama ya ununuzi wa 10%.

Mkoa	Wilaya	Kata	Kiwango kwa Kila Eneo la Mita za Mraba kwa Viwanja vya Ujenzi (Shs.)	Kiwango kwa Ekari Moja kwa Ardhi ya Kilimo (Shs.)	10% Gharama ya Manunuzi (Shs.)	Viwango kwa Kila Ekari ya Ardhi ya Kilimo Pamoja na Gharama ya Ununuzi (Sh.)[57]
a		Nsunga	Haihusiki	1 000 000	100 000	1 100 000
		Kasambya	Haihusiki	1 000 000	100 000	1 100 000
		Kyaka	Haihusiki	700 000	70 000	770 000
		Kilimilile	Haihusiki	800 000	80 000	880 000
	Bukoba	Kyamulaile	Haihusiki	700 000	70 000	770 000
		Mugajwale	Haihusiki	650 000	65 000	715 000
		Kyaitoke	Haihusiki	650 000	65 000	715 000
		Izimbya	Haihusiki	650 000	65 000	715 000
		Kibirizi	Haihusiki	500 000	50 000	550 000
		Rukoma	Haihusiki	700 000	70 000	770 000
	Muleba	Ngenge	Haihusiki	600 000	60 000	660 000
		Mubunda	Haihusiki	600 000	60 000	660 000
		Kasharunga	Haihusiki	650 000	65 000	715 000
		Karambi	Haihusiki	650 000	65 000	715 000

Mkoa	Wilaya	Kata	Kiwango kwa Kila Eneo la Mita za Mraba kwa Viwanja vya Ujenzi (Shs.)	Kiwango kwa Ekari Moja kwa Ardhi ya Kilimo (Shs.)	10% Gharama ya Manunuzi (Shs.)	Viwango kwa Kila Ekari ya Ardhi ya Kilimo Pamoja na Gharama ya Ununuzi (Sh.)[57]
		Kyebitembe	Haihusiki	800 000	80 000	880 000
		Bisheke	Haihusiki	800 000	80 000	880 000
		Burungura	Haihusiki	750 000	75 000	825 000
	Biharamulo	Nyarubungo	Haihusiki	600 000	60 000	660 000
		Nyamigogo	Haihusiki	800 000	80 000	880 000

Marekebisho ya Mfumuko wa Bei mwaka 2012 na Viwango vya Mazao / Miti

Viwango vya Utendaji namba 5 vya Mashirka ya Fedha ya Kimataifa (IFC PS5) – kuhusu Utwaaji wa Ardhi na uhamishaji wa watu na makazi bila hiari yao vinapendekeza mali iliyopotea kulipwa kwa gharama mbadala. Inafafanua Gharama mbadala kama Thamani ya Soko la mali pamoja na gharama ya manunuzi. Thamani ya Soko ni dhamana inayohitajika kuruhusu jamii zilizoguswa, na watu kuweza kufidia mali iliyopotea, kulingana thamani ya mali hiyo. Ili kukidhi viwango hivi na kutoa gharama mbadala kwa upotezaji wa mazao na miti, jedwali la Thamani la Fidia ya mazao la 2012 yameongezwa kwa kutumia viwango vya mfumuko wa bei ulioongezeka kutoka 2013 hadi Oktoba 2018. Viwango vya mfumuko wa bei vinaonyeshwa kwenye Jedwali 6-4. Kiwango cha mfumko wa bei kwa miaka 2013 hadi Oktoba-2018 ni 45.44%. Marekebisho haya ya mfumko wa bei hutumiwa katika jedwali la Fidia la Viwango vya Kifedha vya Kimataifa (IFS Compensation Schedules).

Jedwali 6- 4: Viwango vya Mfumuko wa Bei (2013-2018)[58]

Mwaka	Kiwango cha Mfumuko wa Bei wa kila Mwaka (%)
2013	12.00
2014	5.75
2015	4.75
2016	6.25
2017	6.50
Januari - Octoba 2018	3.6
Mfumuko wa bei uliojumuishwa (2013-2018	**45.44**

Posho ya Usumbufu

Posho ya usumbufu (kama ilivyokokotolewa chini ya mfumo wa Bunge la Tanzania) imetumika kwa thamani ya ardhi na mali iliyothaminiwa chini ya stahiki za ziada chini ya Viwango vya Kifedha vya Kimataifa (IFS) katika misingi sawa ya ardhi na mali chini ya sheria ya Tanzania. Kiwango cha asilimia saba (7%) kimetumika kwa posho hii.

Kipande kidogo kilichobaki katika ardhi iliyoguswa (ardhi yatima)

Ardhi ambayo haijaguswa na Mradi ni sehemu ya eneo la ardhi ambalo limebaki bila kuguswa na Mradi na hivyo linatambulika kuwa ni eneo lisilo na manufaa ya kiuchumi katika Mradi. Kwa mujibu wa sehemu ya 6.4.1 Vipande vya ardhi chini ya nusu ekari

[58] Viwango vya Mfumuko wa bei vya kila mwezi kwa mwaka wa 2018 ni kama ifuatavyo: Januari (4.0%), Februari (4.1%), Machi (3.9%), Aprili (3.8%), Mei (3.6%), Juni (3.4%), Julai (3.3 %), Agosti (3.3%), Septemba (3.4%) na Oktoba (3.2%). Kiwango cha wastani cha mfumuko wa bei kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2018 kwa hiyo ni 3.6%. Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya kitaifa. Viwango sawa vya mfumuko wa bei kwa mwaka 2013 hadi 2018 ni: 2013 (12.0%), 2014 (5.75%), 2015 (4.75%), 2016 (6.25%) na 2017 (6.5%). Kiasi cha kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka 2013 hadi Oktoba 2018 ni, kwa hiyo, 45.44%.

(0.5) ambazo ziko nje ya Jiji, Manispaa, Miji au mipaka ya kiutawala[59] itachukuliwa kulingana na Sheria ya Bunge ya Upataji Ardhi.

Ardhi yatima nje ya vigezo hivi itafidiwa chini ya Mashirika ya fedha ya Kimataifa (IFC) kama ifuatavyo:

- ☐ Ikiwa asilimia 20 au chini ya hapo ya sehemu ya kipande cha ardhi cha mguswa itabaki bila kuguswa na Mradi, pendekezo litafanyika la kupata ardhi hiyo (iwapo tu mmiliki wa ardhi atakuwa yupo tayari kuiachia).
- ☐ Pale ambapo ardhi yatima inapozidi nusu ekari na/au ipo ndani ya Manispaa au mamlaka ya mipaka ya Mji[60].

Maeneo Bomba linapokatisha

Mkuza wa njia ya bomba katika wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Biharamulo utakatisha jumla ya barabara 32 (6 chini ya TANROAD na 26 chini ya TARURA) na hifadhi zake, sehemu 13[61] za Gridi ya umeme na hifadhi yake kwa mkoa wa Kagera. Maeneo haya yanakatishwa na mkuza hayatageuzwa kuwa ardhi ya jumla, aidha haitakodishwa kwa ajili ya Mradi bali itabaki kuwa chini ya umiliki wa mamlaka husika (k.m. TANROADS, TARURA, TANESCO nk). Mradi unashirikiana na mamlaka husika kufanya makubaliano ya ukatishaji wa mkuza katika miundombinu hii. Mbinu ya uthamini iliyotumika kwa miundo mbinu hii imefafanuliwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

[59] Sheria Bunge ya Utwaaji Ardhi, 1967 sehemu ya 10-2 inaeleza kuwa upatikanaji ardhi wa chini ya nusu ekari hautatumika chini ya kifungu 10-1 ndani ya mji, manispaa au mipaka ya kiutawala ya mji.

[60] Katika Sheria Bunge ya Utwaaji Ardhi, 1967, kifungu cha 10 kinasema kwamba eneo lenye ukubwa nusu ekari ndiyo ukubwa wa mwisho ardhi nje ya Mji, manispaa usiohitajika na Mradi ambao unaruhusiwa chini ya Sheria za Tanzania.

[61] Kuna mitandao kadhaa ya nyaya za umeme za TANESCO 132 kV ambayo hueda sambamba na mkuza wa bomba wa katika wilaya ya Muheza. Baadhi ya njia za umeme kati ya hizi hukatisha mkuza wa bomba katika baadhi ya maeneo.

Barabara kuu na Barabara za Mikoa

Inafahamika bayana kuwa upana wa barabara kuu na hifadhi za barabara za mkoa uliongezwa na mamlaka ya barabara kutoka mita 20/22.5 za awali hadi mita 30 pande zote kutokea mstari wa katikati unaoigawa barabara pande mbili zilizo sawa ili kuendana na kanuni zilizopo. Uainishaji wa hadhi ya sehemu ya ardhi ya barabara iliyoathiriwa na upanuzi huu (hata kama sehemu hiyo imethaminiwa na kulipiwa fidia kwa mamlaka husika) ulihitajika wakati wa mchakato wa uthibitishaji na wakala husika.

Barabara zilizopo ambazo zinaathiriwa na ukanda wa mkuza zimechunguzwa ili kufanya uthamini. Kanuni za stahiki zilizoorodheshwa hapo chini zinatoa mwongozo wa uthamini wa ardhi na mali zinazohusiana na barabara zinazokatiza mkuza:

- ☐ Ni pale tu ambapo Wakala wa Barabara (TANROADS / TARURA) inawasiliana kwa maandishi ndani ya kipindi cha uthamini, kwamba ardhi ndani ya sehemu yoyote ya hifadhi (yaani, mstari wa katikati unaoigawa barabara pande mbili zilizo sawa kwa sheria ya awali na sasa iliyobadilishwa ya hifadhi za barabara) ambayo haijalipwa fidia inaweza kuwa ardhi stahiki na mali zisizohamishika na kuingizwa katika Ripoti ya Uthamini chini ya Sheria ya Bunge ya Tanzania;
- ☐ Wakati sehemu ya ardhi ya mguswa na mali zingine (mfano mazao) zimo kwenye hifadhi ya barabara na wakala husika hajathibitisha ndani ya kipindi cha uthamini kwamba eneo lote la hifadhi limelipwa fidia basi ardhi (ndani ya mstari /mpaka husika tu), na mali zinaweza kuingizwa kwenye Ripoti ya Uthamini kwa ajili ya stahiki za ziada chini ya Viwango vya Kifedha vya Kimataifa (IFS).). Hata hivyo, ardhi itaingizwa tu kwenye stahiki za ziada chini ya IFC pale tu ambapo matokeo ya uchunguzi yatathibitisha hili; na
- ☐ Pale ambapo Wakala husika (mfano TANROADS/TARURA) inathibitisha kwa maandishi ndani ya kipindi cha uthamini kwamba hifadhi ya barabara imelipwa fidia basi mali zisizohamishika tu (k.m. mazao na miti) (sio ardhi), itathaminiwa chini stahiki ya ziada chini ya Viwango vya Kifedha ya Kimataifa (IFS).. Inatarajiwa kwamba barabara nyingi zitaangukia chini ya kanuni hii.

Barabara zingine – Zinazoingia na Kutoka, na Barabara za Jamii

Pale ambapo mkuza unaingiliana na hifadhi za barabara za kuingia na kutoka na barabara za jamii[62], inafahamika kwamba hifadhi hizi za barabara kwa ujumla zimefanyiwa uchunguzi na/au kulipwa fidia hapo awali na mamlaka husika. Katika hali kama hii, kanuni zilezile zitatumika kama ilivyo katika hifadhi ya ardhi za barabara za mikoa ambazo zimechunguzwa na kulipwa fidia yake, yaani mali isiyohamishika tu (kwa mfano mazao na miti, sio ardhi), ambapo imethibitishwa siyo vya kufikirika, vitathaminiwa chini ya stahiki za ziada chini ya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa (IFC). Mali ambazo zimethibitika kwamba ni za kufikirika hazilipwi fidia.

Kanuni za jumla za Barabara zote

Pale ambapo hakuna mwongozo uliopo wazi kutoka katika chombo husika kwenye kipindi cha uthamini juu ya upana wa hifadhi unaotumika, ukubwa wa hifadhi mbili umetumika na tofauti iliyowekwa chini ya stahiki za ziada chini ya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa (IFC). Kwa hali yoteyote, mali katika hifadhi ya barabara ambazo zimethibitishwa kuwa ni za kufikirika hazitastahili fidia.

Misitu na Hifadhi

Bomba litapita hifadhi ya msitu wa Minziro (MNFR), hifadhi ya msitu wa mto Ruiga na pori la akiba la Biharamulo katika mkoa wa Kagera. Hifadhi ya msitu wa Minziro (MNFR) na hifadhi ya msitu wa mto Ruiga ziko kwenye mamlaka ya Wakala wa huduma ya misitu Tanzania (TFS) na na pori la akiba la Biharamulo liko chini ya mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori (TAWA).

Misitu ya serikali inatathiminiwa kwa njia ya kifalme (royalty method) kwa sababu misitu ya asili haiuzwi. Malipo haya ni mapato ya serikali ikiwa imekosa miti au misitu.

[62]Barabara ndogo zinazoingia barabara kuu - hifadhi ya mita 40 (mita 20 kila upande kutoka mstari wa katikati), barabara za hifadhi ya mita 30 (mita 15 kila upande kutoka mstari wa katikati) na barabara za jamii - hifadhi ya mita 25 (mita 12.5 kila upande kutoka mstari wa katikati).

Gridi za Umeme

Kuna mashirika mawili (2) yenye jukumu la kutoa huduma za umeme nchini Tanzania, Shirika la Umeme na Usambazaji, Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Ni wazi kuwa, mtandao wa umeme ulio chini ya mamlaka ya TANESCO, kwa ujumla njia zake zote tayari zimelipwa fidia. Kwa mali ambazo haziwezi kuhamishika tu (k.m. mazao na miti) (sio ardhi), ambapo hazijathibitishwa kuwa ni za kufikirika, zimethaminiwa chini ya haki za ziada chini ya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa (IFC). Mali ambayo imethibitishwa kuwa ya kufikirika hailipwi fidia.

Njia ambazo hazijalipwa fidia, au pale ambapo matokeo ya uchunguzi mahususi yanaonyesha kuwa waguswa wanatoa madai ya fidia ya ardhi ndani ya hifadhi ya njia ya umeme, zimepitiwa moja baada ya nyingine. Katika mazingira haya, iwapo madai hayo yataonekena kuwa ni halali (na sio ya kufikirika) kanuni za mbinu za uthamini zilizotumika kwa Hifadhi ya Barabara kuu zitatumika sanjari na maoni yoyote yaliyopokelewa kutoka kwa wakala husika (kama TANESCO au REA). Viwango tofauti vya ukubwa wa njia za hifadhi za umeme vimetolewa kwa ajili ya Mipango Miji (Viwango vya Nafasi ya Mipango Miji), kanuni, 2018 kama ilivyo kwenye Jedwali 6-5 hapa chini itatumika.

Jedwali 6-5: Haki ya Njia za Ugavi wa Umeme

Aina ya Njia ya Usambazaji wa Umeme katika Kilovoti (KV)	Haki ya Njia katika Mita/ Gridi ya Umeme	Umbali Kutoka Mstari wa Katikati kwa Mita
11	5.0	2.5
33	10.0	5.0
66	20.0	10.0
132	40.0	20.0
220	60.0	30.0
400	60.0	30.0

Stahiki za Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha

Mradi utatoa msaada wa urejeshaji wa ustawi wa maisha, kulingana na ukubwa wa athari zinazowapata waguswa/kaya husika, kwa mujibu wa matakwa ya Viwango vya Kifedha vya Kimataifa (IFS).. Stahiki za urejeshaji wa ustawi wa maisha zimeunganishwa na waguswa na zitakuwa na thamani ya ongezeko kwa waguswa walio na vipande vingi vya ardhi vilivyoguswa na mradi. Vigezo vya msaada wa urejeshaji wa ustawi wa maisha vimeainishwa katika Jedwali 6-6 na kwa undani katika Sura ya 8.

Jedwali 6-6: Viwango vya Msaada wa Marejesho ya Maisha

Kikundi	Kategoria ya Stahiki ya Ardhi Mbadala[63]	Vigezo	Aina ya Msaada ya urejeshaji wa ustawi wa maisha
G1	0	Mtu Aliyeguswa na Mradi (Mguswa atapoteza makazi yake kabisa.	☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi ☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa mtu binafsi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi
G2	1a	Mtu Aliyeguswa na Mradi atapoteza kabisa ardhi yake na atatambuliwa kama aliye kwenye mazingira magumu.	☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi ☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa mtu binafsi unaozingatia na usiozingatia

[63] Angalia sehemu hapa chini juu ya ardhi mbadala.

Kikundi	Kategoria ya Stahiki ya Ardhi Mbadala[63]	Vigezo	Aina ya Msaada ya urejeshaji wa ustawi wa maisha
			msingi wa ardhi (inayoendana na sababu ya mazingira magumu kwa mguswa)
G3	2a	Waguswa watapoteza zaidi ya ekari ya ardhi (zaidi ya ekari moja lakini chini wastani wa ukubwa wa shamba (chini ya wastani ya ukubwa wa shamba) katika Wilaya hutambuliwa kama mtu aliye katika mazingira magumu [64]	☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi Maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi ☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa mtu binafsi kulingana na sababu za mazingira magumu ya Waguswa
G4	1 na 2	Mtu Aliyeguswa na Mradi atapoteza kabisa uwezo wa kupata sehemu tu ya ardhi au sehemu nzima	Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi

[64]Ekari Uwiano Sawa (AE): kipimo cha uzalishaji mzuri wa ardhi unaofaa katika wilaya iliyoguswa na Mradi. Ni uwiano wa nambari mbili: (a) idadi ya ekari ya ardhi ambayo kaya katika wilaya inahitaji kujiendeleza (kwa kuzingatia mazao makuu na kiwango cha juu cha Wilaya hiyo, na mavuno ya mazao maalum ya wilaya na wastani saizi ya kaya); na (b) idadi ya wastani ya ekari ya ardhi kwa kila kaya kwa wilaya zote zilizoguswa za Mradi (kama ilivyoripotiwa data ya sensa ya kilimo ya 2007/2008). Wastani wa Ukubwa wa Shamba (AFS): Kiwango cha wastani cha kilimo (mazao) cha ardhi kwa kila kaya katika wilaya, kama ilivyoripotiwa sensa ya kilimo ya 2007/2008.

Kikundi	Kategoria ya Stahiki ya Ardhi Mbadala[63]	Vigezo	Aina ya Msaada ya urejeshaji wa ustawi wa maisha
G5	2b	Mtu Aliyeguswa na Mradi ambaye ni mpangaji wa ardhi atapoteza > Ekari sawa (AE) ya mazao na/ au miti, lakini hatapoteza fidia ya ardhi.	☐Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi (kama vile usimamizi wa fedha na mafunzo ya ujasiliamali) ☐Mipango wa ustawi wa maisha kwa ngazi ya kundi ambapo vibarua wa mguswa wa mradi atapoteza > ekari sawa na kupata ardhi mbadala kilimo
G6	3	Waguswa waliolipwa fidia ya mazao, miti na mali zingine ikijumuisha miundombinu mingine isiyokuwa ya makazi, yenye thamani ya TShs. 100,000 au zaidi.	☐ Mipango ya urejeshaji wa ustawi maisha kwa vikundi unaozingatia na usiozingatia msingi wa ardhi (kama vile usimamizi wa fedha na mafunzo ya ujasiliamali, mipango ya ufugaji wa wanyama, ufugaji wa nyuki; na ☐ Mpango ya urejeshaji wa ustawi wa maisha itakuwa sawa na mali iliyopotea.
(G7) Waguswa wenye fidia ya fedha zenye thamani chini ya laki moja (T.Sh. 100,000/=) au wanaopokea fidia ya makaburi tu, hawatastahili mipango ya urejeshaji wa ustawi wa maisha.			

Haki za Watu Walio katika Hali Hatarishi

Msaada wa ziada wa uhamishaji watu na makazi utatolewa kwa kaya zilizo katika hali hatarishi ambazo ama zimehamishwa kutoka kwenye makazi yao au zimeyumbishwa kiuchumi na Mradi. Tukitambua kwamba hakuna sababu/kigezo kimoja ambacho moja kwa moja kinaziweka kaya katika hali hatarishi, sababu zifuatazo zilibainika[65] kuzifanya kaya kushidwa kustahimili athari za mtikisiko na majanga toka nje hivyo kuwafanya kuwa wenye uwezekano mkubwa wa kuwa kwenye mazingira magumu kutokana na athari za kuchukuliwa ardhi zinazohusishwa na Mradi:

- ☐ Umri wa mkuu wa kaya (ukijumuisha kaya zinazoongozwa na watoto);
- ☐ Jinsia ya mkuu wa kaya;
- ☐ Kiwango cha elimu ya mkuu wa kaya;
- ☐ Kaya zinazotunza mtu asiyejiweza mmoja au zaidi;[66]
- ☐ Asilimia ya matumizi ya kaya kwenye chakula;
- ☐ Idadi ya wategemezi katika kaya na rasilimali zilizopo za kusaidia wategemezi hao;
- ☐ Idadi ya watoto kati ya miaka 6-14 ambao hawasomi shule; na
- ☐ Majuimuisho ya athari moja au zaidi kati hizo hapo juu.

Kaya zimetengwa kuwa kwenye kundi la kaya zilizo katika mazingira magumu baada ya uchambuzi wa jumla wa sababu zinazopelekea mazingira magumu, kaya hizo zimegundulika kuwa ziko kwenye uwezekano wa kuwa katika mazingira magumu. Uchambuzi wowote wa mazingira magumu unahitaji kutambua kuwa mazingira magumu sio dhahiri bali ni kiwango cha daraja kinachotofautisha kati ya watu maskini na walio katika hali hatarishi.

[65] Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, 2012. "Uchambuzi Kabambe wa Upatikanaji wa Chakula na hali hatarishi (CFSVA), Tanzania,2010" na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, 2012. "Uchambuzi Kabambe wa Upatikanaji wa Chakula na hali hatarishi (CFSVA), Tanzania, 2012.

[66] Ulemavu ni upotevu au upungufu wa fursa za kushiriki katika maisha ya kawaida ya jamii kwa kiwango sawa na wengine kwa sababu ya mwili, kiakili au kijamii. Ni neno la jumla, linalojumuisha ulemavu, kushindwa kushiriki katika wa shughuli, na vizuizi vya ushiriki. Sera ya Taifa ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004.

Ili kujumuisha tofauti hizi, aina tatu za hali hatarishi zimependekezwa:

- ☐ **Aina ya 1: (Mazingira magumu),** Kaya zitawekwa kwenye Orodha ya Kaya zilizo katika hali hatarishi na kukidhi vigezo vya kupewa msaada wa vitu na ustawi wa maisha, kadhalika, msaada stahiki utatolewa kulingana na aina ya hali hatarishi.
- ☐ **Aina ya 2 (Wanaoweza kuwa katika hali hatarishi)**, kaya zitastahili msaada wa vitu na ustawi wa maisha lakini zitahitaji uthibitisho zaidi kabla ya kuwekwa kwenye orodha ya kaya zilizo katika mazingira magumu.

- ☐ **Aina ya 3** (**Zilizo katika hali hatarishi**), kaya zitawekwa kwenye orodha ya kaya zilizo katika hali hatarishi na inalazimika ziingizwe kwenye kila tathimini au uchunguzi ili kufuatilia waguswa, hazitahesabiwa kama kaya zilizo katika hali hatarishi kwa minajiri ya msaada wa vitu lakini zitakidhi kupewa msaada wa ustawi wa maisha.

Sura ya 9 inaeleza Mpango wa Watu walio katika hali hatarishi (VPP) na maelezo zaidi ya ubainishaji wa watu walio katika hali hatarishi na msaada unaoweza kutolewa kwao.

Chaguzi za Fidia

Ili kuendana na Viwango vya Kiutendaji namba 5 vya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa (PS5 IFC), kaya zinazostahiki tu ndizo zitakazopewa fursa ya kuchagua fidia kati ya fedha au vitu (kama vile nyumba au ardhi mbadala).

Pale ambapo waguswa waliostahili watachagua Mbadala wa nyumba au ardhi, kiasi cha fedha cha fidia stahiki kwa miundombinu iliyoguswa na/au ardhi itakayo badilishwa kwa gharama ya Mradi na baadaye itapunguzwa kutoka kwenye fidia ya fedha ya mguswa iliyowasilishwa katika Ripoti ya Uthamini chini ya Sheria ya Tanzania ya Jedwali la Fidia. Haki zingine za ziada chini Jedwali la fidia ya IFC vina dokeza kwa muhtasari "Jumla ya Fidia ya Fedha iliyobaki" ikiwa mguswa atachagua mbadala wa miundombinu na /au ardhi.

Kanuni ya jumla ya kusisitiza wakati wote wa kufanya chaguzi zilizoainishwa hapa chini na kujumuishwa katika mfumo wa haki, kipaumbele cha Mradi ni kulipa pale inapowezekana kwa sababu ya athari za Mradi kwa masuala yanayohusu ustawi wa maisha yanayotokana na ardhi, kama fidia ya ardhi na mali zilizoguswa kulingana na Viwango vya Kiutendaji namba 5 vya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa (PS5 IFC)

Mbadala wa Ardhi[67]

Utwaaji wa ardhi na matumizi ya ardhi iliyopo pembezoni mwa ukanda wa mkuza yalizingatiwa wakati wa kuamua Stahiki na vigezo vya utoaji ardhi mbadala na katika kufanya tathimini ya mazingira magumu, kutokana na kuwa haya yataathiri eneo la ardhi inayohitajika kuweza kuzalisha chakula cha kutosha kwa mguswa. Katika maeneo yote ambako bomba linapita, eneo hutofautiana katika wilaya na mkoa uliyoguswa, kwa kuzingatia mavuno ya mazao ya chakula kikuu yanayopatikana na idadi ya wastani ya wanafamilia ambao wanahitaji kusaidiwa. Kutokana na uchambuzi wa kiutaalam uliofanywa na DWC ni eneo dogo linalohitajika kusaidia wastani wa kawaida wa kaya katika wilaya ili kuvuka mstari wa ukomo wa umasikini, kama ilivyoamuliwa na Mpango wa Chakula Duniani[68] (WFP). Hii imetajwa kuwa ni Mgawanyo Sawia wa Ekari katika Wilaya (District Acre Equivalent Coefficient (DAEC) or AE).[69]

Vigezo vilivyoorodheshwa katika Jedwali 6-7 vilitumika kuamua Stahiki wa kupewa fursa kuchagua fidia kati ya fedha au ardhi mbadala ya kilimo (Shamba).[70]

Uwiano Sawa wa Ekali (AE) na Wastani wa Ukubwa wa Shamba (AFS) katika wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba, na Biharamulo ni kama ifuatavyo.

- ☐ Missenyi: AE = ekari 0.82 na AFS = ekari 2.27;
- ☐ Bukoba: AE = ekari 1.24 na AFS = ekari 1.50
- ☐ Muleba: AE = ekari 1.24 na AFS = ekari 1.41; and
- ☐ Biharamulo: AE = ekari 1.31 na AFS = ekari 2.87.

[67] Ardhi ya vijiji na ardhi ya inayomilikiwa na serikali au taasisi binafsi haina sifa ya kupewa fidia ya wa ardhi, isipokuwa makanisa na shule ambazo zinakaguliwa kwa kutegemea msingi wa kesi na kesi.

[68] World Food Program, 2012. Comprehensive Food Security and Vulnerability Analysis. Tanzania

[69] Kwa maelezo ya zaidi, rejea notisi ya Kiufundi: Viwango vya Stahiki vya EACOP, Februari 2019.

[70] Ardhi inayotumika kwa madhumuni ya jamii, haswa ardhi ya malisho inayotumiwa kwa pamoja italipwa fidia fedha taslimu kwa upotevu wa ardhi iliyochukuliwa kwa kuzingatia viwango vya soko pamoja na 10% ya gharama ya manununuzi na fidia iliyolipwa kwa jamii ya wafugaji (chombo kitateuliwa na jamii au ikiwa ni ardhi ya vijiji itakuwa ni Baraza la Kijiji / Mtaa). Msaada wa Mradi katika kudumisha ufikiaji wa huduma au mpango mbadala katika kipindi cha ujenzi.

Jedwali la 0-2: Vigezo Stahiki na Haki kwa Ardhi

Aina ya Stahiki ya Ardhi mbadala	Vigezo	Haki ya Ardhi Mbadala	Haki ya Msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha
0	Waguswa waliohamishwa ambao makazi yao yaliguswa na mradi na wanastahili mbadala wa nyumba	☐ Watachagua kupewa fidia ya fedha taslimu au fidia ya vitu kama ardhi (ili Mradi tu ardhi ipo katika kata yao) au sivyo mpango wa mbadala wa ustawi wa jamii wa Maisha (fidia ya fedha taslimu) na ☐ Pale ambapo mguswa atachagua nyumba mbadala atapewa katika kiwanja cha makazi tu.	☐ Mpango wa urejeshaji ustawi wa maisha kwa ngazi ya kundi unaozingatia kiwango cha ardhi na usiozingatia kiwango cha ardhi ☐ Mpango wa Urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha mtu binafsi (G1).
1	Mguswa anapoteza<AE[71] OR >AFS[72] (AFS) (Ukubwa wa shamba wastani)	☐ Fedha taslimu ya kwa ajili ya fidia ya ardhi	☐ Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi unaozingatia msingi wa ardhi na usiozingatia msingi wa ardhi(G4).
1a	Mguswa wa Mradi atapoteza <AE na amebainishwa kama aliye katika mazingira magumu	☐ Fedha taslimu ya kwa ajili ya fidia ya ardhi.	☐ Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi unaozingatia msingi ardhi na kutozingatia msingi ardhi na ☐ Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa

[71] Uwiano Sawa wa Ekari (AE), huzingatia uzalishaji wa ardhi katika wilaya na wastani wa idadi ya wanakaya katika katika kaya zote ndani ya wilaya.

[72] AFS – Wastani wa ukubwa wa shamba.

Aina ya Stahiki ya Ardhi mbadala	Vigezo	Haki ya Ardhi Mbadala	Haki ya Msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha
			maaisha kwa kiwango cha mtu binafsi (kama inavofaa katika sababu mazingira magumu ya mguswa wa mradi (G2).
2	Mguswa atapoteza >AE lakini <AFS na anatabulika kama aliye katika mazingira magumu	☐ Atachagua kupewa fidia ya fedha taslimu na ☐ kupewa fidia mbadala ya ardhi (Ili Mradi tu ardhi inapatikana katika kata), au mpango wa ustawi maisha (kwa fidia ya fedha taslimu).	☐ Mpango wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi, au ☐ Mpango wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha mtu binafsi (G3).
2a	Mguswa atapoteza >AE lakini <AFS na anatabulika kama aliye katika mazingira magumu	☐ Atachagua kupewa fidia ya fedha taslimu au kupewa fidia mbadala ya ardhi (Ili Mradi tu ardhi inapatikana katika kata), au mpango wa ustawi maisha (kwa fidia ya fedha taslimu).	☐ Mpango wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi, au ☐ Mpango wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha mtu binafsi (G3).
2b	Wapangaji wa ardhi ya mguswa ambao watapoteza mazao, miti na mali zingine zenye thamani chini ya Tsh 100,000 isipokuwa ardhi na makazi ya mguswa wa mradi >AE	☐ Hawana stahiki ya ardhi	☐ Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi usiozingatia misingi ya ardhi (mf. Matumizi bora ya fedha na mafunzo ya ujasiliamali; na ☐ Mpango wa urejeshwaji wa ustawi wa maisha kwa makundi ambapo Wapangaji wa ardhi wa waguswa wamepoteza wastani wa ekari >AE

Aina ya Stahiki ya Ardhi mbadala	Vigezo	Haki ya Ardhi Mbadala	Haki ya Msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha
			na mguswa wa mradi anaejitambua na kuweza kupata ardhi mbadala (G5).
3	Mtu aliyeguswa na Mradi aliyepewa fidia ya mazao, miti na mali zingine pamoja na mali zote zisizo miundombinu ya makazi yenye thamani ya Tsh 100,000 au zaidi	☐ Hawana stahiki ya ardhi	☐ Mpango wa urejeshaji wa ustawi wa maisha kwa kiwango cha makundi usiozingatia misingi ya ardhi (mf. Usimamizi wa fedha na mafunzo ya ujasiliamali, ufugaji wanyama, nyuki), na; ☐ Mpango wa Urejeshwaji wa maisha utashabihiana na kiwango cha mali kilichopotea (G6).
3a	Mguswa atapoteza mazao, miti na mali zingine pamoja na mali zote zisizo miundombinu ya makazi na thamani ya fidia itakuwa chini Tsh 100,000	☐ Hawana stahiki ya ardhi	☐ Hastahili urejeshwaji wa ustawi wa maisha (G7).

Mbadala wa Makazi

Vigezo vifuatavyo vilitumika kubaini Stahiki wa kupewa fursa ya kuchagua fidia kati ya fedha taslimu au makazi mbadala, (rejea sura ya saba kwa maelezo zaidi).

☐ Kaya itapoteza kabisa makazi yake na vyote vinavyohusiana na makazi.

Aina ya nyumba mbadala itategemea ukubwa wa kiwanja cha makazi yanayobadilishwa. Utaratibu ufuatao utatumika kuchagua aina ya nyumba mbadala:

- Kiwango cha chini cha nyumba inayobadilishwa itakuwa ni Kipimo cha mita za mraba 25 (25m^2 - Aina A). Vipimo vyote chini ya au sawa na mita za mraba 25 (25 m²), bila kujali idadi ya vyumba, vitabadilishwa na nyumba Aina A. Ikiwa nyumba mbili zozote za mguswa ni chini au sawa na mita za mraba 25 (25m²), mguswa atapewa fidia ya nyumba hizi mbili, fidia moja ya aina A na fidia ya fedha kwa nyumba ndogo:
- Aina B – mita za mraba 33 (33m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa wa zaidi ya mita za mraba (25m²) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 33 (33m²);
- Aina C – mita za mraba 39 (39m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 33 (33m²) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 39 (39m^2);
- Aina D – mita za mraba 47 (47m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 39 (39m²) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 47 (47m²);
- Aina E – mita za mraba 58 (58m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 47 (47m²) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 58 (58m²);
- Aina F – mita za mraba 75 (75m²) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 58 (58m²) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 75 (75m^2);
- Aina G – mita za mraba 105 (105m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 75 (75m^2) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 105 (105m^2); na
- Aina H – mita za mraba 145 (145m^2) itakuwa mbadala wa makazi yote yenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 105 (105m^2) lakini chini ya au sawa na mita za mraba 145 (145m^2).

Kumbuka: Eneo la sakafu na eneo la baraza hayakujumuishwa.

Kwa kila nyumba mbadala mguswa atapatiwa choo kimoja cha kisasa na jiko moja.

Pale ambapo mguswa anastahili miundo mbinu ya nyumba zaidi ya moja, anaweza kuchagua kati ya:

- Nyumba moja nyenye choo cha kisasa na jiko moja kwa kila mbadala au
- Choo cha shimo kilichoboreshwa, jiko na stoo kwa kila nyumba

Miundo mbinu ambayo haitabadilishwa itastahiki fidia ya fedha.

Kumbuka: Makazi ya kuishi lazima yawe majengo yaliyokamilika na yawe yanatumika na sio yaliyotelekezwa na mguswa ili yaweze kustahili kwenye kupewa fursa ya kuchagua mbadala wa makazi.

Ardhi (kiwanja cha makazi) kinachohusishwa na mbadala wa makazi ya watu yaliyopendekezwa na Mradi huo kimefafanuliwa katika kanuni za Mipango miji (viwango vya nafasi vya upangaji miji), kanuni ya 2018, kama ilivyoainishwa katika Jedwali 6-8. Wastani wa ukubwa wa kiwanja unaotumika na Mradi ni mita za mraba 1000 (1000m^2) katikati ya maeneo ya makazi ya watu wachache. Ukubwa wa kiwanja utafanyiwa marekebisho kulingana na hali ya makazi ya awali ya nyumba inayobadilishwa. (i.e. makazi ya watu wengi = mita za mraba 300 hadi 600 (300 – 600m^2). Kiwango stahiki cha eneo la makazi kitatengwa sanjari na Sheria ya Mipango Miji ya Tanzania ya 2016, ambapo mguswa anachagua mbadala wa fidia ya vitu au Makazi[73]

[73]Hata hivyo, Kiwanja cha makazi kitakuwa kati ya sehemu itakayotengwa ya mbadala wa ardhi wa waguswa wa Mradi (i.e. hakuna nyongeza juu yake). Ambapo mali za mguswa aliyehamishwa atapoteza shamba la ukubwa chini ya ukubwa wa kiwanja cha makazi bado atastahiki kupewa kiwanja cha makazi ya watu.

Jedwali - 0-3: Viwango Stahiki vya Maeneo ya Makazi kwa Ajili ya Nyumba Iliyojitenga na Masheni ("Maisonette")

No.	Aina	Ukubwa wa kiwanja katika mita za mraba (m^2) maeneo ya mjini	Idadi ya juu ya kaya.	Idadi ya juu ya majengo	wastani wa juu viwanja
i.	Eneo maalum na makazi yasiyopangwa (kesi maalum)	90 – 300 m^2	1	1	80
ii.	Makazi ya watu wengi	301 – 600 m^2	1	2	60
iii.	Makazi ya kati	601 – 800 m^2	1	2	55
iv.	Makazi ya watu wachache	*801 – 1,200 m^2*	*1*	*2*	*50*
v.	Makazi ya watu mahususi	*1201 – 2,000 m^2*	*1*	*2*	*45*

6.5 Muhtasari wa Haki

Jedwali la 6-9 hadi 6-13 yanaonyesha mgawanyo wa haki katika Mkoa mzima wa Kagera. Hii ni pamoja na stahiki zote za urejeshaji wa ustawi wa maisha na msaada zaidi kwa watu walio katika mazingira magumu.

Jedwali la 6 – 9: Muhtasari wa Haki za Waguswa wa Mradi katika Wilaya ya Missenyi

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na Kij...	Hifadhi za Misitu na Wanyama pori	Makazi ya Mguswa yaliyopotea	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao	Biashara (Mpangilio wa Viwango vya Mazao na Ui... 2018)	Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi ya Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika														
Kategoria ya Stahiki (Kama katika Jedwali la 6-1)		**A1 – A7**		**H2**	**G1/ H1, H4, H5**			**B1 – B5**			**I1 – I7**			**J 2**	**CAT1**	**CAT2**	**CAT3**	**G1**	**G2**	**G3**	**G4**	**G5**	**G6**	**G7**
MISSENYI																								
Mutukula	Mutukula	60	1	0	9	0	2	3	7	1	2.97	6021	6769	6	4	10	18	2	12	1	45	0	0	1
Nsunga	Byamutemba	22	2	0	3	0	0	0	0	0	15	31	1340	0	1	5	3	0	0	4	18	0	1	1
	Igayaza	36	1	0	2	1	2	2	1	0	2.67	1321	17466	0	5	7	2	2	7	1	24	0	1	2
Kassa	Mabuye	61	15	0	2	0	7	7	9	1	4.1	969	8460	9	12	13	12	7	1	3	3	0	9	9

[74] Ni pamoja na Miti na Viwango vilivyokubalika na Mthamini Mkuu mwaka 2018 pamoja na viwango vya nyongeza vilivyoidhinishwa kama inavyoonyesha katika kiambatisho B.

mbya											2	2							5		1		
	Kassambya	27	7	0	2	0	1	1	3	0	3.38	5262	2869	7	5	9	5	1	8	1	13	1	4	7
	Nyabihanga	62	16	0	6	0	7	7	11	2	5.14	15982	9285	14	14	10	14	7	10	3	39	0	10	9
Kyaka	Bulifani	36	15	1	2	0	0	0	1	0	4.27	3753	3968	19	8	16	11	0	15	3	15	2	6	10
Kilimilile	Kilimilile	61	2	0	7	0	3	3	0	0	14.12	5431	4814	6	10	17	15	3	12	11	29	0	2	5
JUMLA		**365**	**59**	**1**	**33**	**1**	**22**	**23**	**32**	**4**	**51,67**	**47493**	**5497 1[75]**	**61**	**59**	**87**	**80**	**22**	**79**	**27**	**214**	**3**	**33**	**44**

[75] Haijajumuisha miti iliyoathiriwa na Hifadhi ya Misitu ya Minziro – Tizama kipengele cha 5.5.2.

Jedwali 6 – 10: Muhtasari wa Haki za Waguswa wa Mradi katika Wilaya ya Bukoba

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na Kijiji	Hifadhi za Misitu na	Makazi ya Mguswa	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao	Biashara (Mpangilio wa Viwango vya Mazao na	Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi ya Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika														
Kategoria ya Stahiki		**A1 – A7**		**H2**	**G1/H 1, H4, H5**		**B1 – B5**				**I1 – I7**			**J2**	**CAT1**	**CAT2**	**CAT3**	**G1**	**G2**	**G3**	**G4**	**G5**	**G6**	**G7**
(Kama katika Jedwali la 6-1)																								
BUKOBA																								
Kyamulaile	Kyamulaile	19	1	0	3	0	2	3	2	1	0.31	640	709	0	3	6	6	2	3	1	12	0	1	1
Mugajwale	Kobunshwi	89	5	0	5	0	3	3	0	1	4.08	10150	5685	0	12	26	19	3	31	0	40	0	4	15
	Mugajwale	96	24	0	6	0	7	8	5	5	3.10	12221	10403	8	17	21	32	7	32	0	53	0	11	17
Kyaitok	Kyaitoke	11	29	0	7	0	1	12	1	5	1.8	700	179	18	1	2	2	1	24	0	71	0	8	3

[76] Ni pamoja na Miti na Viwango vilivyokubalika na Mthamini Mkuu mwaka 2018 pamoja na viwango vya nyongeza vilivyoidhinishwa kama inavyoonyesha katika kiambatisho B.

e		6					2		6		0	9	55		6	2	4	2						0
Izimbya	Izimbya	1	0	0	3	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1	0	0	0
Kyaitoke	Rugaze	1	0	0	2	0	1	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1	0	0	0	0	0	0
Kibirizi	Kamuli	54	9	0	6	0	1	1	0	2	0.93	1169	3411	3	9	11	12	1	14	2	34	0	3	9
Rukoma	Nshesh e	2	15	0	3	0	0	0	0	0	3.70	19	0	0	2	4	4	0	0	0	2	0	7	8
JUMLA		**378**	**83**	**0**	**35**	**0**	**26**	**28**	**23**	**14**	**13.92**	**31208**	**38163**	**29**	**59**	**90**	**97**	**26**	**104**	**3**	**213**	**0**	**34**	**80**

Jedwali 6 – 11: Muhtasari wa Haki za Waguswa wa Mradi katika Wilaya ya Muleba

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Hifadhi za Misitu na	Makazi ya Mguswa	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao	Biashara (Mpangilio wa Viwango vya Mazao na Mimea, 2012) na miti	Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi va Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika														
Kategoria ya Stahiki (Kama katika Jedwali la 6-1)		A1 – A7		H2	G1/ H1, H4, H5		B1 – B5				I1 – I7			J 2	CAT1	CAT2	CAT3	G1	G2	G3	G4	G5	G6	G7
MULEBA																								
Ngenge	Rwigembe	61	13	0	8	0	1	1	3	0	4.24	1146	2367	5	11	18	16	1	23	0	32	0	8	10
	Nyakanyasi	88	7	0	3	0	8	9	16	2	3.63	1510	4726	12	19	29	12	8	36	0	37	0	0	14
	Ngenge	121	9	0	3	0	5	5	5	1	7.34	2109	4112	12	8	28	31	5	33	0	73	0	3	16
	Kishuro	86	6	0	10	0	6	6	14	0	1.84	151	3022	8	1	2	18	6	29	1	45	0	2	9

[77] Ni pamoja na Miti na Viwango vilivyokubalika na Mthamini Mkuu mwaka 2018 pamoja na viwango vya nyongeza vilivyoidhinishwa kama inavyoonyesha katika kiambatisho B.

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Hifadhi za Misitu na	Makazi ya Mguswa	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao	Biashara (Mpangilio wa Viwango vya Mazao na Mimea, 2012) na miti	Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi va Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika														
Kategoria ya Stahiki (Kama katika Jedwali la 6-1)		A1 – A7		H2	G1/ H1, H4, H5		B1 – B5				I1 – I7			J 2	CAT1	CAT2	CAT3	G1	G2	G3	G4	G5	G6	G7
												7			0	2								
	Rukindo	54	5	0	3	0	3	3	3	0	2.18	1757	2151	5	11	19	13	3	23	0	24	0	1	7
Burungura	Kakoma	112	9	0	4	0	8	8	1	1	7.72	1697	3385	10	27	49	17	8	60	0	34	0	2	17
Mubunda	Kikagate	34	8	0	4	0	3	5	6	1	3.95	341	178	0	8	13	8	4	17	1	13	0	5	3
	Kikagate PS-3	17	1	0	1	0	4	5	7	0	3.65	352	102	2	0	7	5	4	3	0	10	0	0	1
Bisheke	Milanda	25	7	0	1	0	3	4	6	0	4.62	1011	540	0	0	13	6	3	5	1	12	0	5	5
Kasharunga	Kiteme	170	42	0	5	0	8	8	20	0	20.41	8191	3502	9	31	30	45	8	49	1	104	0	25	30
Karambi	Kiguzi	112	6	0	1	0	6	6	8	1	7.56	4938	4298	6	23	24	11	6	38	0	62	0	4	8

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Hifadhi za Misitu na	Makazi ya Mguswa	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao		Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi ya Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika			Biashara (Mpangilio wa Viwango vya Mazao na Mimea, 2012) na miti											
Kategoria ya Stahiki (Kama katika Jedwali la 6-1)		**A1 – A7**		**H2**	**G1/ H1, H4, H5**		**B1 – B5**				**I1 – I7**			**J 2**	**CAT1**	**CAT2**	**CAT3**	**G1**	**G2**	**G3**	**G4**	**G5**	**G6**	**G7**
	Karambi	44	2	0	2	0	1	1	1	0	2.99	2028	901	0	3	16	9	1	15	0	23	0	1	6
	Kanyamika	80	10	0	5	0	1	1	5	0	12.41	1492	661	3	23	20	8	1	27	5	42	1	6	8
Kyebitembe	Kasinda ga	11	1	0	0	2	0	0	1	0	1.92	122	35	0	0	5	4	0	2	1	8	0	1	0
JUMLA		**1015**	**126**	**0**	**50**	**2**	**57**	**62**	**96**	**6**	**84.46**	**28211**	**29980**[78]	**72**	**180**	**293**	**202**	**58**	**360**	**10**	**519**	**1**	**63**	**134**

[78] Excludes trees affected within Ruiga River Forest Reserve and Biharamulo Game Reserve – see Section 5.5.2.

Jedwali 6 – 12: Muhtasari wa Haki za Waguswa wa Mradi katika Wilaya ya Biharamulo

Kata	Kijiji / Mtaa	Idadi ya PAPiliki wa Ardhi	Idadi ya Wapangaji	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na	Majengo mengine na /au Ardhi inayomilikiwa na Kijiji	Hifadhi za Misitu na	Makazi ya Mguswa	Miundo mbinu na Majengo			Ekari za Mazao	Mashina ya Mazao Biashara (Mpangilio wa	Viwango vya Mazao na	Idadi ya Makaburi	Mazingira Magumbu			Urejeshaji wa ustawi wa Maisha						
								Makazi ya Watu	Miundo mbinu mingine	Miundo mbinu isiyokamilika														
Kategoria ya Stahiki		**A1 – A7**		**H2**	**G1/H 1, H4, H5**		**B1 – B5**				**I1 – I7**			**J2**	**CAT1**	**CAT2**	**CAT3**	**G1**	**G2**	**G3**	**G4**	**G5**	**G6**	**G7**
(Kama katika Jedwali la 6-1)																								
BIHARAMULO																								
Nyamigogo	Nyamigogo	8	0	0	0	1	0	0	0	0	0.22	11	10	0	3	1	2	0	3	0	5	0	0	0
	Kasozibakaya	20	9	0	5	0	2	3	1	0	12.71	381	120	3	6	5	7	2	3	4	13	1	6	0
JUMLA		**28**	**9**	**0**	**5**	**1[80]**	**2**	**3**	**1**	**0**	**12.93**	**392**	**130[81]**	**3**	**9**	**6**	**9**	**2**	**6**	**4**	**18**	**1**	**6**	**0**

[79] Ni pamoja na Miti na Viwango vilivyokubalika na Mthamini Mkuu mwaka 2018 pamoja na viwango vya nyongeza vilivyoidhinishwa kama inavyoonyesha katika kiambatisho B.

[80] Ni pori la akiba la Biharamulo ndani ya kata ya Nyarubungo.

[81] Haihusishi miti iliyoguswa na mradi kwenye pori la akiba la Biharamulo – Rejea kifungu 5.5.2.

KIAMBATISHO

Orodha ya Vifupisho

DLO	Afisa Ardhi wa Wilaya
AE	Uwiano Sawa kwa Ekari
PAC	Jamii Iliyoguswa na Mradi
PAH	Kaya Zilizoguswa na Mradi
DWC	Kampuni Tanzu ya Digby Wells
IFC	Mashirika ya Fedha ya Kimataifa
PAs	Maeneo ya Kipaumbele
CV	Mthamini Mkuu
EACOP	Mradi wa Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki
IGA	Mkataba Baina ya Serikali Mbili
RPF	Mfumo wa Sera wa Uhamishaji wa Watu na Makazi
RAP	Mpango wa Uhamishaji wa Watu na Makazi
LRP	Mpango wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha
FGD	Majadiliano ya vikundi Lengwa
NT	Nyaraka za Taarifa
IFC	Shirika la Fedha la Kimataifa
GoT	Serikali ya Mungano wa Tanzania
GoU	Serikali ya Uganda
PS	Viwango vya Utendaji
PAP	Watu Walioguswa na Mradi
MLHHSD	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
KII	Watoa Taarifa Wakuu
RV	Wathamini Waliosajililwa

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

MRADI WA EACOP - TANZANIA

TEAM - Total East Africa Midstream,
Msasani Peninsula,429 Barabara ya Mahando D,
S.L.P. 38568, Dar es Salaam - Tanzania.
Simu: 0800 780 068 (Isiyo na Makato) au +255 22 2214100/4102/4103
Barua pepe: EACOP.info@total.com
www.eacop.co.tz

MRADI WA EACOP - UGANDA

TEAM - Total East Africa Midstream,
Kiwanja Namba 2, Barabara ya Yusuf Lule
S.L.P. 34867, Kampala - Uganda.
Simu: 0800 216 000 (Isiyo na Makato) au +256 (0) 204 916 000
Barua pepe: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

@2020, Haki zote zimehifadhiwaHaki zote zimehifadhiwa
Ripoti hii au sehemu yoyote ya ripoti hii hairuhusiwi kuchapishwa, kuhaririwa, kuhifadhiwa au kusambazwa kwa namna yoyote ile bila ya kuwa na idhini ya maandishi ya Utawala wa Bomba la Mafuta Ghafi - Afrika Mashariki.